JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Kitini cha Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Kuhusu Mfumo Jumuishi wa Kitaifa wa Kusimamia Mashauri ya Watoto

Oktoba 2017

SHUKRANI

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI tunatoa shukrani za dhati kwa wadau, na Taasisi zilizoshiriki katika kuandaa mwongozo huu wa Kitaifa wa Mafunzo ya Mfumo Jumuishi wa Mashauri ya Watoto kwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii. Kwa namna ya pekee shukrani ziwaendee Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kushughulikia masuala ya UKIMWI kwa kuwezesha kuandaa mwongozo huu. Aidha, bila kuwasahau Shirika la John Snow Inc/World Education Inc./Bantwana Initiative kwa msaada wa kitaalamu ambao wameutoa wakati wa kuandaa mwongozo huu.

Wizara inapenda kutoa shukrani maalum kwa uongozi na usimamizi wa kitaalam uliofanywa na Wizara, Shirika la John Snow, Inc. (JSI), World Education, Inc./Bantwana Initiative, PACT Tanzania/ USAID Kizazi Kipya, na MEASURE Evaluation ambao pia walitoa msaada wa kitalamu wa jumla kuhusu mwongozo huu wa mafunzo.

Mwongozo huu umekamilika kwa juhudi kubwa zilizofanywa na kikosi kazi ambacho kilijumuisha wataalam mbalimbali kutoka Wizara, Mashirika ya Kimaendeleo na watalamu kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Shukrani za pekee ziwaendee wafuatao kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto: Rabikira Mushi (Kaimu Kamishina Ustawi wa Jamii), Daniel Masunzu (Kamishina Msaidizi wa Huduma za Familia na Watoto), Philbert Kawemama (Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi) na Abasi Makalanga (Afisa Ustawi wa Jamii). Aidha, shukrani za dhati ziwaendee wataalam wafuatao kutoka kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI: Naibu Katibu Mkuu Dkt. Zainab Chaula, Dkt. Ntuli A. Kapologwe (Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe), Rasheed Maftah (Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe), na Zuhura Karya (Afisa Ustawi wa Jamii Mkuu, TAMISEMI).

Wizara inapenda kuwashukuru wafanyakazi wa USAID ambao wamechangia kwa namna mbalimbali kuandaa mwongozo huu. Wizara inatambua juhudi za wafuatao, Dkt. Tulli Tuhuma, Mkurugenzi Mtendaji wa CHSSP, Christine Lalobo, Mshauri Mwandamizi, Natasha Vartapetova, Mshauri Mwandamizina Paschal Wilbroad, Mshauri Mkuu wa ufundi CHSSP kutoka JSI, kutoka World Education Inc./Bantwana Initiative, Gill Garb, Naomi Reich (WEI/B HQ-Boston), Precious Muwoni na Washington Jiri (WEI/Bantwana Zimbabwe), Peter Massesa, Vailet Mollel, Christina Mdemu, na Lilian Badi, WEI/Bantwana Tanzania, na Beth Gragg, WEI/Bantwana, Mshauri mwandamizi wa Mafunzo.

SIHABA NKINGA
Katibu Mkuu
Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto

MHANDISI MUSSA I. IYOMBE
Katibu Mkuu
Ofisi ya Rais - TAMISEMI

YALIYOMO

SHUKRANI	i
MAANA YA VIFUPISHO	iii
Sehemu ya 1- Utangulizi	1
Muhtasari	1
Malengo ya Kitini	1
Sehemu ya 2 - Tafsiri ya Dhana	2
Maana ya WWKMH	2
Maelezo Kuhusu Utoto	3
Jinsi ya Kufanya Kazi na WWKMH Pamoja na Familia zao	5
Ukiwa kama Msaidizi wa Ustawi wa Jamii wa Kujitolea /Mhudumu Mashauri ya Watoto Katika Ngazi ya Jamii	6
Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Wazingatie Kanuni Zifuatazo Wakati wa Kuhudumia Mashahuri ya Watoto	7
Sehemu ya 3 – Usimamizi wa Mashauri ya Watoto	8
Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ni Nini	8
Mchakato wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto	9
Wajibu na Majukumu ya Wataalam/Watekelezaji Katika Usimamizi wa Mashauri ya Watoto	13
Afisa Ustawi wa Jamii Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa	13
Polisi (Dawati la Wanawake na Watoto)	14
Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii	15
Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea	15
Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii	16
Kutembelea Nyumbani na Kufanya Mahojiano	17
Kutoa Msaada kwa Watoto wenye Maambukizo ya VVU	20
Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Huduma za Upimaji na Unasihi	21
Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii Katika Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Huduma za Matibabu na Matunzo	21
Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ngazi ya Jamii Katika Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Famila Zao katika Huduma za Kuondoa Maambukizo ya VVU Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto	22
Rufaa na Ufuatiliaji	23
Kuwasaidia Watoto Katika Kupata Huduma Nyingine za Kijamii	26
Uhakika wa Chakula na Lishe	29
Ulinzi wa Mtoto	46
Tathmini, Sehemu Ya Kwanza	69
Tathmini Sehemu Ya Pili	70
Rufaa ya huduma ya unasihi na kupima VVU	82

MAANA YA VIFUPISHO

ART	Matibabu ya Kufubaza VVU
CBO	Shirika Lisilo la Kiserikali la Kijamii
CHF	Mfuko wa Afya wa Jamii
CHW	Muhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii
CP	Ulinzi wa Mtoto
CSO	Asasi za Kiraia
CTC	Kituo cha Matunzo na Msaada
DSWO	Afisa Ustawi wa Wilaya
ECD	Makuzi ya Utotoni
EMTCT	Kuondoa Maambukizi kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto
FBO	Shirika la Kidini
FGM	Ukeketaji wa Wanawake
HBC	Huduma za Matunzo Nyumbani
HES	Uimarishaji wa Uchumi wa Kaya
HTC	Unasihii na Upimaji wa VVU
IGA	Shughuli za Kujiletea Kipato
JSI	John Snow, Inc.
KWWKMH	Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto
LCW	Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea Ngazi ya Kijiji/Mtaa
LHIV	Kuishi na Uambukizo wa VVU
MMWJ	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii
MMW	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto
NACS	Tathmini ya Lishe, Unasihi na Msaada
NCPA	Mpango wa Taifa wa Kushughulika na Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi
NGO	Shirika Lisilo la Kiserikali
OVC	Yatima na Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi
PEP	Tiba ya Dharura ya Kuzuia Maambukizi ya VVU
PEPFAR	Mpango wa Dharura wa Raisi wa Marekani wa Kudhibiti UKIMWI
PSW	Msaidizi Ustawi wa Jamii
SWO	Afisa Ustawi wa Jamii
TASAF	Mfuko wa Kusadia Jamii Tanzania
UNCRC	Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto
USAID	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani
VAC	Ukatili Dhidi ya Watoto
VEO	Afisa Mtendaji ya Kijiji
VMMC	Tohara ya Hiari Hospitalini
WEO	Afisa Mtendaji wa Kata
WWKMH	Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

Sehemu ya I - utangulizi

Muhtasari

Wadau wamendelea kutambua kuwa ili kuhakikisha kuwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (WWKMH) kwa sababu za ukatili, umaskini, VVU/UKIMWI na sababu nyinginezo wanapata huduma ni lazima kuziwezesha kaya na jamii kupata huduma za jamii kwa usawa. Mfumo wa usimamiaji mashauri ni muhimu katika kuhakikisha kwamba WWKMH na kaya zao wanatambuliwa, tathmini ya mahitaji yao inafanyika kwa usahihi na wanapata huduma kutoka sekta mbalimbali ili kukidhi matarajio ya mtoto na familia.

Kumekuwepo na jitihanda mbalimbali nchini Tanzania zinazolenga kuimarisha mifumo na miundo katika jamii ikiwemo uanzishaji wa timu za ulinzi za watoto ambazo zinafanya kazi katika baadhi ya Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa nchini. Ingawa siyo kaya zote zenye WWKMH hupata huduma kutoka kwenye timu hizo, hata zile kaya zinazopata huduma huzipata zile zinazolenga ulinzi zaidi na si huduma zote kwa ujumla kwa mfano huduma nyingine za ustawi na afya. Katika kushughulikia mapungufu haya serikali imeazisha mfumo wawasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii wenye uwezo wa kutoa huduma shirikishi katika kukabiliana na uhatarishi kwa kutumia mafunzo, kujenga stadi na uragabishi.

Malengo ya Kitini

Kitini hiki kimetengenezwa ili kuwaongoza wasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii katika kutoa huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na familia zao.

Sehemu ya 2-tafsiri ya dhana

Maana ya WWKMH

Maana ya "Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi": "Ni watoto wenye umri chini ya miaka 18 ambao wapo katika hali mbaya inayohatarisha afya, ustawi na makuzi yao."[1]

Kwa maana hiyo WWKMH wapo katika hali zifuatazo:

- Watoto wanaoishi katika kaya zenye umaskini wa kipato na haziwezi kukidhi mahitaji yake kwa kujitosheleza kama vile elimu, huduma za afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za makuzi ya awali ya watoto, ulinzi na usalama wa kimwili na hisia.
- Watoto wenye walezi ambao ni wana ulemavu unaowazuia kutoa huduma na ulinzi kwa WWKMH.
- Watoto wanaolelewa kwenye kaya za wazee (wenye miaka 60 na kuendelea) na wanaokosa huduma ya elimu, afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za makuzi ya awali ya watoto na ulinzi wa kimwili na kihisia.
- Watoto yatima wanaokosa huduma ya elimu, afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za malezi na makuzi ya awali ya watoto na ulinzi wa kimwili na kihisia.
- Watoto wanaokaa kwenye kaya zenye walezi wenye magonjwa sugu wanaokosa elimu, huduma za afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za malezi na makuzi ya awali ya watoto na ulinzi wa kimwili na kihisia.
- Watoto wenye ulemavu wanaokosa elimu, huduma za afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za malezina makuzi ya awali ya watoto, ulinzi wa kimwili na kihisia.
- Watoto wenye magonjwa sugu (ikiwemo VVU) wanaokosa elimu, huduma za afya, chakula na lishe, makazi, huduma za VVU na UKIMWI, huduma za makuzi ya awali ya watoto na ulinzi wa kimwili na kihisia.
- Watoto ambao ni wakuu wa kaya.
- Watoto wanaoishi na kufanyakazi mitaani.
- Watoto walio kwenye hatari ya kufanyiwa ukatili, kunyanyaswa na/au kutelekezwa.
- Watoto walio kwenye hatari ya kuhusika au kukinzana na sheria.
- Watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto.
- Watoto waliozaliwa gerezani au walioambatana na mama zao gerezani au waliopo rumande.
- Watoto wanaotumikishwa katika ajila mbaya (unyonyaji wa kingono, shughuli za kijinai, ajila za majumbani na wahanga wa usafirishaji watoto) ambayo uathiri mahudhurio shuleni.
- Watoto amabo wako kwenye hatari ambazo hazisababishwi na yaliyotajwa hapo juu (kama vile utumiaji dawa za kulevya, watoto wanaohama makazi kwa sababu ya majanga ya asili).

[1] Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuhudumia Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (NCPA II 2013-2017).

Yatima na Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi ni kina nani?

Miradi inayofadhiliwa na PEPFAR inawatambua yatima na Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kama ifuatavyo:

- Watoto yatima kwa sababu ya VVU/UKIMWI (kwa kupoteza mzazi mmoja au wote)
- Watoto walioathika na magonjwa sugu
- Watoto wenye maambukizi ya VVU
- Watoto wanaoishi kwenye kaya yenye mtu mwenye VVU
- Watoto wanaoweza kupata maambukizi ya VVU (wakiwa tumboni, wakati wa kujifungua, au wakati wa kunyonya)
- Watoto walio kwenye uhatarishi kwa sababu ya VVU au athali zake za kijamii na kiuchumi katika maeneo ambayo kiwango cha maambukizi kipo juu (mfano wasichana balehe walio kwenye hatari ya kupata maambukizo ya VVU na UKIMWI)

Maelezo Kuhusu Utoto

Utoto ni hatua muhimu katika makuzi ya mwanadamu. Wasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii na viongozi wao (Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii) wakielewa masuala ya utoto itawasaidia kufanya kazi na watoto na vijana balehe kwa ufanisi hususani Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi wakiwemo wenye maambukizi ya VVU.

Tafsiri ya Mtoto

Kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (UNCRC): Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Sehemu ya 4(1) ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pia inamtafsiri mtoto hivyohivyo.

Utoto na Majukumu

Masuala ya utoto hutofautiana kwa kutegemea mazingira ambayo mtoto hulelewa. Mtoto hutambua amali na desturi za jamii yake kadri anavyo lelewa na kuchangamana na jamii. Mtoto anaweza kuwa na wajibu na majukumu mbalimbali kwa kutegemea malezi na tamaduni zilizopo.

Ustawi wa Mtoto

Mtoto kama walivyo binadamu wengine, ana mahitaji na haki. Mfano wa mahitaji na haki ni pamoja na: hitaji/haki ya kuishi, makazi, mavazi, afya, elimu, ulinzi na upatikanaji wa maji safi na salama. Jamii, wazazi na walezi ni lazima wahakikishe watoto wanapata haki na huduma hizi. Pale ambapo familia na kaya zitashindwa kutoa huduma hizi jitihada zifanywe na watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto kwenye Jamii na Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto kwenye Jamii wengine ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata haki na huduma bila kubaguliwa.

Maendeleo ya Mtoto

Maendeleo ya mtoto ni makuzi yanayoendelea katika kipindi chote cha maisha ya mtoto. Mwanadamu hubadilika sana katika kipindi cha utoto. Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto kwenye Jamii wakielewa masuala ya maendeleo ya mtoto itawasaidia kufanya kazi na watoto kwa ufanisi hususani watoto walio kwenye mazingira hatarishi na wenye maabukizi ya VVU. Maendeleo ya mtoto wakati wa uchanga ni hatua muhimu katika makuzi ya mwanadamu.

Hatua za Makuzi ya Awali ya Mtoto

Hatua	Mawasiliano	Kiakili	Kijamii	Kimwili
Miezi 3	Huitikia sauti na sura alizozizoea Hushtushwa na sauti za ghafla au mitikisiko	Humtambua mlezi wake mkuu Analia akisikia njaa au akijisikia vibaya	Anaweza kubembelezwa kwa sauti au kuguswa Ukicheza naye anatabasamu	Anaitambua mikono ya mzazi/ mlezi Ananyonya Ana uwezo wa kunyanyua kichwa
Miezi 6	Anafanya matendo madogo madogo na sauti Anageuza kichwa kufuatilia sauti au mtikisiko	Anachukua vitu na kuviweka mdomoni Anacheza na midori kwa njia mbalimbali Anapenda vitu vya rangi tofauti tofauti	Anaogopa watu wapya kwake Anahitaji aangaliwe Anatambua baadhi ya watu	Hujizungusha kwa tumbo na mgongo Anakaa bila kusaidiwa na kutambaa
Miezi 12	Anatambua maneno rahisi na ishara Anaigiza neno mojamoja na ishara	Anaelewa kuwa kuna kitu hata kama hakioni Anajaribu kutatua matatizo madogo madogo Anaanza kutambua vitu vinasababishwa na nini	Anatumia ishara Mlezi wake akiondoka analia Anaanza kufurahia michezo	Anakaa mwenyewe bila kusaidiwa Anajaribu kusimama
Miaka 2	Anafahamu kati ya maneno 50 hadi 200 au ishara Anaweza kuongea kwa maneno 2 au 3 au ishara Unatumia maneno machache au ishara	Anajaribu kulinganisha vitu Anatumia vitu vinavyo fanana/ husiana Anatumia muda mrefu katika jambo fulani	Anamuigiza mlezi wake Anacheza na watoto wengine Anawaomba wengine akihitaji msaada	Anatembea Anaweza kuchuchumaa

Miaka 3	Anayalewa zaidi maneno rahisi Anajua na anatumia kati ya maneno 500 hadi 1000 au ishara Anawasiliana	Anapanga vitu kadiri ya eneo linavyo fanana au kuigiza kwenye vishimo Anachambua vitu Anatapanya na kukusanya vitu	Anafurahia kusaidia shughuli nyumbani Anapenda apongezwe akifanya kishughuli fulani Anatambua watu wanajisikiaje	Anakimbia, anaruka, anapanda Anatumia mikono kwa kufanya shughuli ngumu Anarusha mpira
Miaka 5	Anaongea au anaonyesha kuhusu alichokifanya Anatumia takribani maneno 2000 au ishara Anauliza maswali mengi (udadisi)	Anaweza kwenda kwenye maeneo fulani Anatatua vikwazo rahisi Anajua kuhesabu	Anacheza na watoto wengine Anajua taratibu Anaelezea kwa njia nyingi anavyo jisikia	Kunakili maumbo mepesi Anaweza kusimama kwa mguu mmoja Anaweza kutembea kwa kurudii nyuma kwa urahisi

Utoto wa Kati

Ni kati ya miaka 6-11umri wa shule ya msingi hupimwa kwa kuzingatia uwezo wa kufanya michezo; mantiki katika mchakato wa kufikiri; maarifa ya msingi ya awali; kujitambua nafsi, maadili na urafiki; kuwa mshirika katika kundi rika.

Umri Balehe

Ni kati ya miaka 10 hadi 17, umri wa kubalehe hutambulika kwa makuzi na mabadiliko yaliyo wazi, mtu hupenda kujitegemea zaidi, uhatarishi uliopo na uzoefu, mabadiliko makubwa ya kisaikolojia na kimwili, mabadiliko makubwa katika mahusiano na kushirikiana na jamii.

Malezi

Malezi ni mchakato unao muwezesha mtoto kukua kimwili, kihisia, kijamii na kiakili kutoka akiwa mchanga hadi mtu mzima. Kila mtoto ana haki ya kupata malezi kutoka kwa wazazi wake au kuasiliwa.

Jinsi ya Kufanya Kazi na WWKMH Pamoja na Familia zao

Kufanyakazi na watoto hususan WWKMH ni kazi inayoweza kuwa na mambo yote mawili kufurahisha au kuleta changamoto. Inakuwa na changamoto kutokana na ukweli kuwa watoto hawa wamekuwa kwenye uhatarishi kimwili, kijamii, kihisia na kisaikolojia, hali hii inahitaji stadi maalum katika kuhudumia mashauri ambapo kuna umuhimu wa kushirikisha mtoto na jamii kwa ujumla.

Ni muhimu kufahamu uzoefu wetu na imani kuhusu masuala ya utoto kwa sababu hii huathiri mawazo yetu kuhusu jambo gani ni sawa na linahitajika wakati wa kuhudumia mashauri.

Aidha, Watoa Huduma za Mashauri Katika Jamii lazima watambue kuwa katika jamii nyingine watu huamini kuwa "mtoto ni wa jamii" hususan katika jamii zenye koo na familia kubwa zenye ushirikiano mzuri. Kwa mantiki hiyo Watoa huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii wanaweza kushirikiana na watu na taasisi nyingine katika kushughulikia matatizo ya mtoto.

Ni muhimu kwa Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii kuelewa maeneo ya kuyashughulikia wakati wa kutoa huduma kwa watoto. Kwa hiyo Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima waweze:

- Kutambua na kuheshimu tofauti za watu katika jamii;
- Fahamu kuwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii zinatofautiana;
- Elewa utamaduni mila na desturi zinazotakiwa kuzingatiwa katika kutoa huduma;
- Tambua mbinu asilia zinazotumiwa na jamii husika katika kulea/kulinda zinazoendana na amali na imani ya mtoto na familia;
- Fanya tathmini jumuhishi ya hali ya mtoto na yenye taarifa za kutosha;
- Tengeneza mpango shirikishi wa huduma unaokubalika na kutekelezeka;
- Mara zote zingatia kanuni za kuhudumia mashauri, mfano usiumize/kutomdhuru mtu, kutunza siri na kuzingatia masilahi ya mtoto kwanza.

Ukiwa kama Msaidizi wa Ustawi wa Jamii wa Kujitolea /Mhudumu Mashauri ya Watoto Katika Ngazi ya Jamii

Moja ya nia ya Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni kuwalinda watoto ambao wapo katika hatari ya kutenganishwa na wazazi pamoja na walezi (familia) katika umri wowote wa awali. Ingawa kumtenganisha mtoto inaweza kuwa ni kwa ajili ya maslahi ya mtoto, lazima uamuzi ufanyike kwa makini. Hii ni kwasababu tangu kuzaliwa hadimiaka 2 watoto hutengeneza hisia mwambata walau kwa mtu mmoja mzima wanayekuwa karibuu naye katika familia. Watoto pia huigiza matendo ya watu wazima walio karibu nao na mara nyingi matendo ya wazazi au walezi.

Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii wawasaidie wazazi/walezi kuelewa kuwa:

- Matendo kama ya kukumbatia, kunyonyesha na kupakata hutengeneza hisia mwambata na mtoto ambazo husaidia kukua kwa ubongo.
- Kukosekana kwa hisia mwambata huathiri makuzi, na hii husababisha kukosa kujiamini, uwezo mdogo katika kujenga mahusianao, afya ya akili na tabia, shauku ya kujifunza na kufanikiwa. Watoto wahudumiwe wakiwa kwenye familia zao au katika jamii ikiwezekana.
- Malezi ya watoto katika vituo iwe ni ufumbuzi wa muda tu wakati utaratibu wa kuwalea watoto katika familia unafanyika. Na hii ifanyike pale tu ambapo jitihada zote zimeshindikana.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Wazingatie Kanuni Zifuatazo Wakati wa Kuhudumia Mashahuri ya Watoto

1. **Epuka kudhuru:** Kila Msimamizi wa Mashauri ya Watoto aepuke kuwaingiza watoto katika hatari nyingine.
2. **Zingatia usiri**: Taarifa zote atakazopata Msimamizi wa Mashauri ya Watoto azitunze kama siri na asizitoe kwa mtu yeyote ambaye hana kazi nazo na wala mamlaka ya kuzihifadhi.
3. **Zingatia kipaumbele cha maslahi ya mtoto kwanza:** Maamuzi yote na huduma anazopatiwa mtoto yazingatie maslahi mapana ya mtoto kwa kuzingatia vipaumbele.
4. **Zingatia uwajibikaji:** Msimamizi wa Mashauri ya Watoto mara zote awe tayari kuwajibika kwa matendo yake.
5. **Huduma ziheshimu na kuzingatia tamaduni:** Heshimu tamaduni, imani na dini ya mtoto unaye mhudumia. Toa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii kwa kupitia kiongozi wa Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto pale ambapo utagudua kuwa matendo ya tamaduni, imani au dini ya kikundi flani yanakinzana na haki za watoto.
6. **Usibague:** Msimamizi wa mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima awahudumie watoto wote kwa usawa bila upendeleo wa kabila, rangi, jinsia au hali ya kijamii waliyo nayo.
7. **Omba ridhaa:** Mara zote Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii aombe ridhaa ya familia na/au makubaliano ya mtoto kila anapotaka kutembelea familia. Pale amabapo familia ipo kwenye mgogoro na unahisi kuna unyanyasaji wa mtoto toa taarifa kwa mamlaka ili uchunguzi ufanyike haraka.
8. **Zingatia mipaka ya kazi na mara zote epuka mgongano wa kimaslahi:** Kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto epuka matumizi mabaya ya nafasi yako kwa kuwanyanyasa watoto na familia zao. Pale amabapo majukumu ya Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii yatavurugwa kwa sababu ya mahusiano yake na mtoto au familia, basi mtoa huduma mwingine achuke jukumu la kuhudumia familia hiyo.

Sehemu ya 3 - Usimamizi wa Mashauri ya watoto

Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ni Nini

Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ni njia nzuri ya kufanya kazi na watoto pamoja na famila zao ili wapate huduma bora wanazohitaji na kwa wakati toka kwa watu sahihi au mashirika ndani ya mfumo ulio ratibiwa vizuri.

Ni muhimu kutumia njia ya Usimamizi wa Mashauri ya Watoto wakati wa kufanya kazi na WWKMH kwa sababu:

- Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na familia zao wana matatizo mbali mbali yanayohitaji huduma nyingi na tofauti.
- Familia zilizo katika mazingira hatarishi haziwezi kujitegemea katika kupata huduma kwa sababu hazina taarifa juu ya huduma zilizopo nakukosa rasilimali
- Huduma nyingine ni vigumu kupatikana (mfano: zinaweza kuwa zinatolewa katika maeneo tofauti na muda ambao si muafaka kwa familia).
- Wakati mwingine famila hazitambui chanzo cha matatizo ya watoto na familia zao na namna wanavyoweza kusaidiwa.

Ingawa usimamizi wa mashauri ya watoto huitaji njia sahihi katika kutunza taarifa, uratibu wa huduma na rasilimali kwa Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii (au Mtaalam wa Ustawi wa Jamii) ambaye pia anawajibika kufanya tathmini ya mahitaji na utekelezaji wa mpango wa huduma.

Katika usimamizi wa mashauri ya watoto wote wa kike na wakiume wenye mahitaji ya dharura ya ulinzi na ustawi ni lazima:

- Watambuliwe na wapate taarifa sahihi kadiri ya umri na utamaduni wao.
- Wapate mwitikio wenye ufanisi, toka sekta mbalimbli na ambao ni rafiki kwa mtoto toka kwa watoa huduma wanaostahiki, ulio ratibiwa na kuzingatia uwajibikaji.

Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ni Lazima uwe:

RAFIKI KWA MTOTO

- Unahusisha na kutoa huduma sahihi na zinazopatikana kwa urahisi kwa watoto.
  - Kwa mafano kwa kutoa taarifa katika muundo/lugha amabayo inaweza kueleweka na watoto wa umri tofauti.

- Unahusisha kupangilia na kutoa huduma na kufanya maamuzi kwa njia mbayo inazingatia mahitaji na maslahi ya mtoto kwanza.
  - Kwa mfano ni lazima kuzingatia muda amabo ni muafaka kwa watoto na familia zao wakati wa kufanya vikao na mapitio mbalimbali badala ya kuzingatia muda unao mfaa mtumishi.

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii (MMWJ) ni mtu amabye jukumu lake la msingi ni kuwezesha mchakato wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto. MMWJ ni kiongozi wa kila **hatua ya** mchakato wa mashauri ya watoto amabaye kwa makini anazingatia mahiataji tofauti na maalum ya mtoto na familia, yakiwemo matarajio yake ya maisha ya baadaye, uchaguzi, motisha, vipaumbele, amali, rasilimali zilizopo, huduma na misaada.

Mchakato wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

Mchakato wa usimamizi wa mashauri ya watoto unahusisha wajibu na majukumu yanayoeleweka kwa sekta mbalimbali jinsi wanavyoshirikiana ndani ya mfumo unao walinda watoto na vijana balehe. Mchakato huu unaweka viwango vya maneno ya kutumia, vigezo vinavyokubalika, viwango na michakato inayotumiwa na wadau tofauti ili kuwezesha ushirikiano kati ya taasisi na taasisi katika kusimamia mashauri ya watotona familia.

Mashauri ya watoto yanaweza kugawanywa katika makundi mawili, mashauri ya dharura na ya kawaida. Katika mashauri ya kawaida maisha ya mtoto hayapo hatarini hii inahusisha masuala kama hitaji la ada ya shule. Mashauri ya dharura ni yale ambayo maisha ya mtoto yatakuwa hatarini kwa mfano aina zote za unyanyasaji mtoto kingono, unyonyaji, kudhuru mwili na ukatili wa kisaikolojia/kihisia. Mashauri yote ya dharura ni lazima yawekwe katika maadishi na kutolewa rufaa/au taarifa ndani ya kipindi cha saa 24 kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Polisi au kwenye Vituo vya kutolea Huduma za Afya. Mashauri yote yanayotolewa taarifa katika taasisi nyingine kama polisi ni lazima yawekwe kwenye kumbukumbu za maadishi na kutolewa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaakwa ajili ya ushughulikiaji na ufuatiliaji.

Ni muhimu kutambua ni kwa kiasi gani tathmini ya hatari na matarajio imefanywa katika taratibu za mashauri ya watoto kwa kuzingatia muda wa kuchukua hatua. Ni lazima Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii azingatie kuwa viwango tofauti vya hatari katika mashauri ya kumlinda mtoto.

Kutambua Kiwango cha Madhara ya Ukatili

Kiwango	Tafsiri	Maelezo	Muda	Mifano
Kiwango hatarishi cha juu	Maisha ya mtoto yapo hatarini kwa kiasi kikubwa au mtoto amepata madhara makubwa kiasi cha kuathiri maendeleo na ustawi wake endapo hatua za dharura hazitachukuliwa	Mtoto anahitaji huduma za dharura za afya au msaada wa kisheria. Mtoto yupo katika hatari ya kupata majeraha ya kimwili, kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono au anaendelea kufanyiwa vitendo hivyo, aidha, mtoto yupo katika hatari ya kupata ulemavu wa kudumu, kuingizwa katika biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu au pengine hata kufa endapo ataachwa katika mazingira aliyopo kwa sasa bila kuchukua hatua zozote.	Hatua lazima zichukuliwe haraka iwezekanavyo. Toa taarifa haraka kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya au Kituo cha Polisi ili kunusuru maisha ya mtoto.	• Ndoa za utotoni • Ukatili wa kingono • Ukatili wa kimwili • Mtoto anayeishi na VVU na ameacha kutumia dawa lakini anaumwa sana • Watoto wanaoishi nje ya mazingira ya familia • Wahanga wa vitendo vya Ukeketaji

Kiwango hatarishi cha kati	Mtoto yupo katika hatari ya kupata madhara ya kiwango cha kati na hakuna mpango mahsusi wa kumlinda	Hakuna uthibitisho wowote kama mtoto yupo katika kiwango cha uhatarishi unaoweza kusababisha majeraha au kifo/Hakuna dharura	Huduma itolewe ndani ya masaa 24 hadi masaa 72	• Utelekezwaji unaoweza kuathiri maendeleo ya mtoto kama hautashughulikiwa mapema, hata hivyo, hakuna athari kwa usalama na uhai wa mtoto • Ukatili wa kihisia • Ufuasi hafifu wa dawa za kupunguza makali ya VVU • Magonjwa sugu, kuchelewa kukua kulingana na umri au ulemavu • Ajira mbaya kwa watoto
Kiwango hatarishi cha chini	Mtoto hayupo katika hatari kwa sasa na kama kuna hatari madhara yake ni madogoingawa kuna viashiria vya kupata madhara endapo hatua hazitachukuliwa	Nyumbani ni mahali salama kwa watoto hata hivyo, endapo kuna viashiria kwamba mtoto anaweza kupata madhara kama huduma hazitatolewa mapema ni muhimu kuwa afua za ulinzi	Huduma zianze ndani ya siku 14	• Watoto walio nje shule • Vyeti vya kuzaliwa • Watoto wanao tumikishwa kazi nyingi za nyumbani zinazoweza kuathiri ukuaji wao • Kukosekana kwa mahitaji ya shule kama ada na sare za shule • Huduma za kawaida za afya

*Mashauri yote ya kisheria lazima yachukuliwe kuwa ni ya kiwango cha juu au cha kati kulingana na madhara aliyopata mtoto. Kama mtoto yupo katika madhara makubwa zaidi, muongozo wa kiwango hatarishi cha juu utatumika

Hatua za Mchakato wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

Hatua	Maelezo ya hatua	Fomu zitakazo tumika
Hatua ya 1: Utambuzi na usajili	Hatua hii inaanza wakati MMWJ anapotaarifiwa juu ya shauri. Taarifa inaweza toka kwa mwanakamati wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto mwananchi wa kawaida, mwanafamilia, kituo cha upimaji na unasihi juu ya VVU au kituo cha afya, pamoja na watoa huduma za VVU kwenye jamii na Wahudumu wa Afya wa Jamii, Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya, Afisa Ustawi wa Jamii wa Kata, Msaidizi Ustawi wa Jamii, timu ya ulinzi wa mtoto, wasamalia wengine, vituo vya kulelea watoto/yatima, shule/mwalimu, n.k. Taarifa hizi zinaweza kutoka kwa yeyote ila ni wajibu wa MMWJ kuchukua hatua.	Fomu ya Usajili
Hatua ya 2: Tathmini	Huu ni ukusanyaji wa taarifa kwa kina juu ya hali ya maisha ya mtoto kwa ujumla. Mahususi kwa masuala yanayohusu huduma za matibabu, hali ya kimwili na kisaikolojia rasilimali na mahitaji. Lengo la tathmini ni kutambua matatizo na mahitaji ya huduma, mahitaji yapi yamepatiwa huduma na ni nani aliyetoa huduma na ni mahitaji gani hajapatiwa huduma za kutosha. Aina mbili za tathmini zinaweza kufanyika: 1. Tathmini ya awali: Hii hufanyika pale kunapokuwa na mahitaji ya haraka au imetambulika kuwa kuna kutishia maisha, inafanyika wakati wausajili na ni ndani ya saa 24. 2. Tathmini ya kina: Hufanyika ili kujua hali halisi ya mtoto, familia na mazingira yanayomzunguka	Tathmini ya Familia na Mtoto
Hatua ya 3: Kupanga huduma	Mpango wa shauri unaeleza hatua gani ichukuliwe, nani, na lini ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya huduma yamepatikana na mtoto amepata ulinzi.	Tathmini na Mpango wa Huduma
Hatua ya 4: Utekelezaji wa mpango wa huduma	Utekelezaji wa mpango wa huduma unahusisha kufanya shughuli za mpango wa shauri, hii inaweza kuhusisha utoaji wa huduma moja kwa moja au rufaa kwenda kwa watoa huduma wengine kwa kuwaunganisha watoto na huduma nyingine wanazozihitaji. Rufaa hizi zinaweza kufanyka katika hatua yoyote ya mchakato wa usimamizi wa mashauri ya watoto, lakini zinatakiwa kuzingatia mahitaji ya mtoto na familia kama yalivyotambuliwa wakati wa tathmini na inavyoelezwa kwenye mpango wa shauri.	Fomu ya Mpango wa Huduma na Fomu ya Kufuatilia Huduma

Hatua ya 5: Ufuatiliaji na kufanya mapitio	Huu ni mchakato wa kuangalia kama mpango wa shauri unatekelezwa kama ilivyopangwa na mtoto anapata mahitajii yake. Unatoa fursa ya kupata picha ni kwa kiasi gani utekelezaji wa mpango unafanyika, kama bado unawiana na mahitaji na kama siyo kuweza kufanya marekebisho kwenye mpango ambayo yatawekwa kwenye kumbukumbu kwa maadishi katika jalada la shauri.	Fomu ya Rufaa na Fomu ya Ufuatiliaji wa Huduma
Hatua ya 6: Kuhitimisha shauri au kulihamisha	Shauri linaweza kufungwa wakati ambapo tunafikia mwisho wa kufanya kazi na mtoto ikiwa hali imetengamaa, kwa maana hiyo mpago wa shauri umetekelezeka kwa ukamilifu, mahitaji ya ulizi ya mtoto yametekelezwa na mtoto haitaji tena msaada kutoka kwa Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii. Shauri linaweza kufungwa pia pale mtoto anapofariki au kitimiza miaka 18, vinginevyo kuwe na sababu za msingi za kuendelea kumuhusisha kama kuna hali nyingine ya uhatarishi iliyojitokeza. Wakati mwingine mtoto anaweza kuhudumiwa vizuri zaidi shauri lake likipelekawa kwenye ofisi au shirika lingine. Watoto na vijana balehe wenye Maabukizo na walioathirika na VVU wana mahitaji tofauti tofauti amabyo hayawezi kukamilishwa na chanzo kimoja cha huduma. Ni lazima WMWJ kuwaunganisha watoto na huduma na kutoa rufaa kwa masuala ambayo hawayawezi au hawaruhusiwi kuyatolea huduma kadiri ya mahitaji ya WWKMH na vijana balehe.	Fomu ya Kuhitimisha Shauri

Wajibu na Majukumu ya Wataalam/Watekelezaji Katika Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

Msaidizi Ustawi wa Jamii/WMWJ ni lazima wawatambue wataalam/watekelezaji mbalimbali pamoja na wajibu na majukumu yao katika usimamizi wa mashauri ya watoto. Kufahamu wajibu na majukumu ya wahusika wa utekelezaji wa kusimamia mashauri ya watoto itasaidia kutambua mipaka ya WMWJ juu ya nini wanachotakiwa kufanya. Uelewa huu utasadia pia katika kutoa rufaa. Wataalam/wahusika wa utekelezaji wafuatao wanaweza kuhusishwa katika usimamizi wa mashauri ya watoto katika wakati/hatua tofauti:

1. Afisa Ustawi wa Jamii wa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (au Afisa Ustawi wa Jamii mwingine anayewajibika na masuala ya Ustawi wa Familia na Mtoto)
2. Mtaalam wa Afya
3. Dawati la Polisi la Masuala ya Jinsia na Watoto
4. Msimamizi wa Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea/WMWJ
5. Mwenyekiti/Mtendaji wa Kijij/Mtaa/Kata
6. Asasi za kiraia (mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kijamii)
7. Wazazi au walezi
8. Majirani
9. Viongozi wa dini

Afisa Ustawi wa Jamii Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Huyu ni mtumishi wa serikalii ambaye wajibu wake ni kusimamia shughuli zote zinazohusu ustawi na ulinzi wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi/yasiyofikiwa na huduma kama Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi, Wazee, Watu wenye Ulemavu, na watu wenye magonjwa ya kusendeka. Wajibu wao ni pamoja na:

- Kufanya uchunguzi wa awali kuhusu masuala ya ukatili kwa watoto
- Kuelekeza na kutoa ushauri wa kitaalam juu ya usimamizi wa mashauri ya watoto
- Kuwajengea uwezo na kuwasaidia Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii
- Kufanya usimamizi saidizi kwa wasimamizi ngazi ya kata
- Kupokea taarifa na kuthibitisha takwimu
- Kupitia majalada ya mashauri
- Kukusanya taarifa ili kupata picha ya kijamii, kimwili na kihisia ya hali ya mtoto na familia
- Kuandaa mikutano ya mashauri ya watoto kwa kuzingatia taarifa zilizotolewa na wajumbe wa timu, wanafaya maamuzi kuhusiana na shauri na huduma za baadaye kwa mtoto
- Kutoa huduma za kisaikolojia kwa mtoto
- Kusimamia mashauri yote yanayopelekwa katika ngazi ya wilaya
- Kuwawakilisha watoto mahakamani
- Kuishauri mahakama jinsi ya kushughulikia shauri kwa kuzingatia maslahi ya mtoto kwanza
- Kufanya unasihi kwa wazazi/walezi, jamaa na watoto panapokuwa na uhitaji wa kufanya usuluhishi
- Kufunga mashauri
- Kupokea rufaa na kutoa mrejesho wake
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma kwa vipindi maalumu

Watoa Huduma za Afya

Hawa nia wataalamu wa tiba walioajiriwa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali au vya watu binafsi kwa ajili ya kutoa huduma za tiba na ushauri kwa watu wenye matatizo ya kiafya. Majukumu yao ni pamoja na:

- Kufanya uchunguzi wa awali kuhusu masuala ya ukatili kwa watoto
- Kutoa huduma za VVU na UKIMWI, ikiwemo huduma za upimaji, unasihi na matibabu
- Kutoa tiba ya haraka ili kuzuia na kutibu ugonjwa alioupata mtoto
- Kujaza taarifa kwenye fomu namba 3 (PF 3) ya polisi juu ya kilichoonekana kwa ajili ya ushahidi. Lazima kurasa zote katika nyaraka zisainiwe na kuandikwa tarehe. Michoro na picha vinaweza kutumika ikibidi
- Kutathmini na kutibu kwa kuzingatia hatari za kitabibu zinazoambata na ugumu wa masuala ya unyanyasaji
- Kuhakikisha mtoto anapewa rufaa (kwa wakati) kwenda kwenye huduma nyingine atakazohitaji
- Kuwa tayari kutoa ushahidi mahakamani amabapo kuna umuhimu kwa kuwasilisha ushahidi kutasaidia kumlida mtoto asiendelee kunyanyaswa Kukusanya sampuli kwa ajili ya ushaidi wa uchunguzi

Polisi (Dawati la Wanawake na Watoto)

Hawa ni watumishi wa serikali amabo wana jukumu la kulinda usala wa watu na mali zao. Majukumu yao mahususi ni pamoja na:

- Kupokea na kusikiliza matatizo ya kijinai yanayoletwa katika vituo vyao
- Kuweka mikakati ya kuzuia matatizo ya ukatili wa kijinsia
- Kuwaondoa watoto katika hali ya hatari
- Kuisaidia mahakama kutekeleza sheria ya kuwalinda watoto
- Kufungua majalada ya mashauri yanapotolewa na kutoa rufaa kwa mtoto kwa ajili ya huduma nyingine pale zinapohitajika
- Kuwasiliana na kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii wa eneo husika na kumpatia taarifa juu ya shauri lililoletwa kituoni na Afisa Ustawi atafanya maamuzi kama kuna shauri na hatua gani za haraka zinatakiwa kuchukuliwa
- Kufanya upelelezi wa mashauri ya watoto wanayoyapokea katika vituo vyao
- Kuwakamata watuhumiwa na kuandaa mashtaka kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo kupeleka mashauri mahakamani
- Kuhakikisha kuwa fomu namba 3 za polisi (PF 3) zinapatikana kwa urahisi kwa wahanga wa unyanyasaji wa watoto
- Kukusanya ushahidi wa kiuchunguzi
- Kutoa unasihi kwa wazazi/walezi kadiri inavyostahiki
- Kukuza uelewa kwenye jamii juu ya kutii sheria bila shuruti, hususan kulinda haki za watoto

Nchini Tanzania katika jeshi la Polisi vituo vingi vina kitengo kinachojulikana dawati la jinsia na watoto. Vitengo hivi vinasimamiwa na polisi waliopatiwa mafunzo na wenye wajibu wa kushughulikia mashauri ya ukatili wa kijisia na unyanyasaji wa wanawake na watoto. Kukiwa na shauri, polisi atakabidhi ushahidi wote kwa mwendesha mashitaka wa serikali ambaye ataamua kuwa mashitaka yaandaliwe katika mfumo upi.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Wasimamizi katika ngazi ya kata ni kiungo kati ya jamii na Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri. Ni watumishi wa Serikali kutoka katika sekta zenye mahusiano ya moja kwa moja na masuala ya watoto, hasa Maafisa Ustawi wa Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii Wasaidizi. Kama hawapo Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri anaweza kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Elimu wa Kata. Majukumu mahususi ni pamoja na:

- Kutoa msaada wa moja kwa moja na kuwajengea uwezo viongozi wa wasimamizi wa Mashauri ya Watoto katika Jamii vijijini na kuwasaidia wasimamizi wa Mashauri ya Watoto katika Jamii kupitia viongozi wao.
- Kupokea rufaa kutoka ngazi ya jamii na kutoa rufaa kwenda kwa watoa huduma wengine.
- Kuratibu watoa huduma katika ngazi ya kata.
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kazi za Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii.
- Kuweka pamoja na kuwasilisha muhtasari wa mashauri katika kikao cha kila mwezi cha ustawi na ulinzi wa mtoto.
- Kuandaa na kutuma taarifa ya kila mwezi juu ya Usimamizi wa Mashauri ya watoto kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri.
- Kuratibu utafutaji wa rasilimali katika ngazi ya kata kwa ajili ya kuwasaidia WWKMH.

Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea

Msimamizi kiongozi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii (Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea ngazi ya Kijiji) ni kada ya watu wanaojitolea waliofundishwa kufanya kazi ya kuhudumia Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi pamoja na familia zao. Wanapata mafunzo ya siku 10 juu ya stadi za msingi za ustawi wa jamii na stadi za kufanya kazi ya kuhudumia watoto. Pia wanapatiwa mafunzo ya siku 5 juu ya kusimamia mashauri ya watoto.

Majukumu ya wa Msimamizi Kiongozi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni pamoja na:

- Kufanya usimamizi saidizi na kuwapa mafunzo ya kazi Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii
- Kuratibu utafutaji wa rasilimali katika ngazi ya jamii
- Kufanya mikutano ya kujenga uelewa katika ngazi ya jamii kwa kushirikiana na wadau wengine
- Kuthibitisha mashauri yaliyofanywa na Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii
- Kutoa ushauri kwa wasimamizi wa mashauri ngazi ya jamii
- Kutoa taarifa za mashauri kwa Msimamizi wa kata/Afisa Ustawi wa Wilaya

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni wahudumu wa kujitolea walio mstari wa mbele wanaofanya kazi moja kwa moja na Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi, vijana balehe, vijana wenye umri mdogo na familia zao. Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni pamoja na:

- Kuwatambua watoto walio katika mazingira hatarishi wenye mahitaji ya huduma za ustawi na ulinzi kwa kutumia jamii.
- Kutoa taarifa za mashauri juu ya ulinzi na ustawi wa mtoto kwa wakati kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya kwa ufumbuzi zaidi.
- Kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji vya kimwili, kingono, unyonyaji wa kingono, usafirishaji wa watoto, utumikishaji wa watoto, unyanyasaji nyumbani, shuleni, kwenye jamii na mila zenye madhara kama ukeketaji na ndoa za utotoni.
- Kutunza kumbukumbu za watoto na familia zilizotambuliwa zenye uhitaji na kuhuisha taarifa za watoto wakati wote.
- Kulinda haki za watoto kwa kuendesha kampeni za kukuza uelewa kwenye jamii.
- Kutambua rasilimali katika maeneo yao na kujenga uhusiano na watoa huduma wengine kwenye jamii.
- Kutoa rufaa kwa watoto kwenda kwenye huduma za wataalam stahiki kama vile vitengo vya huduma rafiki kwa wahanga na huduma za haki kwa watoto, afya, elimu na usajili wa vizazi.
- Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa mashauri yaliyotolewa rufaa ili kujua maendeleo.
- Kufuatilia utumiaji wa huduma zilizotolewa kwa watoto na kutoa taarifa za kuboresha kama kutakuwa na mapungufu.
- Kuwanganisha walezi na familia kwenye huduma za kijamii kama vile shughuli za kuingiza kipato na vikundi vya malezi.
- Kuwatambua na kuwashawishi watoto, vijana balehe na vijana wadogo kujua hali zao kuhusu VVU kwa kwenda kwenye upimaji na unasihi wa hiari wa VVU.
- Kuwasindikiza Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na familia zao kwenda kupata huduma za msingi ikiwemo upimaji wa VVU, unasihi na matibabu.
- Kuwasaidia watoto ili wazingatie ufuasi wa dawa na tiba ya VVU.
- Kuzijengea uwezo familia ili zitatue matatizo yake kwa kutumia rasilimali walizo nazo katika maeneo yao.
- Kutembelea mara kwa mara familia zenye Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na taasisi nyingine zinazohusika na kushughulikia ustawi na ulinzi ili kukagua hali za ustawi wa watoto.
- Kutembelea kaya zilizo kwenye hatari ya kukosa huduma za ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa mtoto, kama vile kaya ambazo wakuu wake ni watoto au kaya zenye walezi ambao ni walevi.
- Kusambaza taarifa rafiki kwa watoto.
- Kuandaa taarifa za mwezi juu ya watoto waliopatiwa huduma na kitengo cha Ustawi wa Jamii katika Ngazi ya Halmashauri kwa kupitia Msimamizi Kiongozi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii. Ni lazima piakumpatia Taarifa hizi Mtendaji wa kijiji, Mtendaji wa Kata na mashirika ya kiraia.

Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Mara nyingi katika miradi, Wasimamizi wa mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii watakuwa na majukumu yanayo jumuisha yafuatayo:

Toa huduma kwenye jamii:	Shiriki au saidia huduma katika jamii kutambua mtu mmoja mmoja aliye katika mazingira hatarishi au familia.
Fanya tathmini:	Tathmini wateja kujua mahitaji na uwezo wao.
Panga huduma:	Tengeneza mpango wa huduma pamoja na wateja wao kadiri ya tathmini ilivyoonyesha. Hii inahusisha wateja kutambua mahitaji yao ya muhimu, kuweka malengo ya kuboresha na kutambua huduma na msaada utakaokidhi mahitaji ya mteja.
Ratibu huduma:	Wasaidie wateja kupata huduma na rasilimali wanazozitaka (kutoa rufaa, kuwasindikiza wateja, n.k). Fanya uratibu na watoa huduma kama inavyobidi, n.k.
Tetea:	Wafanye utetezi kwa niaba ya wateja wao ili kuhakikisha kuwa wanapata huduma na msaada wanaohitaji.
Elimisha na jengea uwezo:	Wasaidie wateja kujenga maarifa na stadi ili waweze kupata huduma bila kusaidiwa na hivyo kujisadia wenyewe.
Fuatilia:	Wafuatilie wateja mara kwa mara kutambua mabadiliko na/au kuboreka kwa hali.
Ruhusu:	Watambue ni wakati gani wateja wamefikia malengo na kuwasaidia kuacha kutumia huduma.
Saidia kuhitimisha huduma:	Wasaidie wateja kufikiwa viwango mbalimbali katika maeneo ya ustawi na hivyo waweze kutoka katika huduma.
Weka taarifa katika maadishi/tunza kumbukumbu:	Weka mawasiliano yote ya watejakatika maadishi kwa kujaza fomu, kuadika, n.k.

Kutembelea Nyumbani na Kufanya Mahojiano

Kuwatembelea nyumbani ni hatua muhimu katika mchakato wa kusimamia mashauri ya watoto. Kuona mazingira anayoishi mteja (hali ya nyumbani na mazingira yake pamoja na ya majirani) ili kupata hali halisi ya mteja ambayo itasaidia kuandaa mpango wa huduma. Ufuatao ni mchakato wa kuwatembelea nyumbani hatua kwa hatua.

Kuweza Kuingia Kwenye Familia na Kujenga Mahusiano

1. Kupanga tarehe na muda wa kutembelea familia.
2. Kuwaulizia watu wanaoijua familia mfano mwenyekiti wa serikali ya mtaa, kiongozi wa dini ni wakati gani mzuri kwenda nyumbani kuongea na watu muhimu kuhusu maisha ya mtoto.
3. Ukiingia nyumbani hakikisha unafahamu nani yupo ndani kwa wakati huo.
4. Zingatia taratibu za hapo nyumbani (Kuacha viatu mlangoni, kutoweka miguu juu ya meza, kwa mfano). Waelezee wateja kuwa Msimamizi wa Mashauri ya watoto Katika Jamii ni mgeni na kama kuna kwenda kinyume na taratibu za nyumba hiyo.
5. Jitambulishe na onyesha kitambulisho ikiwezekana.
6. Omba ukae. Hii huonyesha heshima na husaidia kujenga mahusiano.
7. Elezea madhumuni ya safari yako, elezea kwa ufasaha mteja atarajie nini kwa ujio wako. Epuka ahadi ambazo Msimamizi wa Mashauri ya watoto Katika Jamii hawezi kuzitekeleza (mfano: "Nitahakikisha mtoto anapata matibabu wanayostahili").
8. Kuwa na uhakika ni nini Msimamizi wa mashauri ya Watoto Katika Jamii anaweza kufanya katika kutoa huduma (mfano: "Naweza kuwasaidia kuwaunganisha na kituo cha afya, ambapo mtoto ataweza kupata matibabu anayohitaji).
9. Waeleze wanafamilia kuwa tathmini itasaidia kutambua matatizo yanayomuathiri mtoto. Familia itashirikishwa juu ya matatizo haya ili kwa pamoja kuweza kutengeneza mpago wa kuyashughulikia.
10. Ikiwezekana kwa ruhusa ya mlezi, panga kuongea na mtoto peke yake. Waelezee wanafamilia kwa nini ni muhimu kuongea na mtoto peke yake.
11. Mara zote ihakikishie familia na mtoto kuwa kila kitakachojadiliwa kitatunzwa kama siri na taarifa hizo wanaweza kupewa watu tu wanaohusika na utoaji wa huduma katika shauri hilo pale inapowezekana.

Jinsi ya Kufanya Mahojiano na Mtoto

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii anatakiwa kujishusha mpaka kwenye kiwango cha watoto ili aweze kuelewa mitazamo yao. Watoto hawapo huru kujielezea kwa ufasaha juu ya nini kinachowasumbua, lakini wanaweza kuonyesha kwa njia ya michezo na njia nyingine zisizo za maongezi. Zifuatazo ni njia nzuri wakati wa kumuhoji mtoto:

- Mara zote uliza maswali rahisi na yanayostahili kulingana na umri wa mtoto.
- Tumia sauti ya upole isiyo tisha.
- Inashauriwa mara zote watoto wa kike wahojiwe na wanawake na watoto wa kiume wahojiwe na wanaume.
- Muda wa mahojiano uwe ni mfupi na uhusishe michezo; mahojiano ya muda mrefu yanaweza kumkera mtoto na kufanya akose umakini.
- Kutumia michezo, picha na midoli inavutia na inaweza kutumika katika kujenga mahusiano na mtoto.
- Usimcheke au usimdharau mtoto.
- Mara zote tengeneza mazingira wezeshi na rafiki ili mtoto afunguke.
- Muonyeshe mtoto kuwa upo wazi na upo tayari kusikiliza maongezi yake.
- Usikasirike na usimuhukumu mtoto. Usibishane na mtoto.
- Heshimu mawazo ya mtoto.
- Usilie wakati mtoto anaelezea habari zake, hii inaweza kupunguza uwezo wako wa kumsaidia mtoto.

ZINGATIA: Pale ambapo anayemnyanyasa mtoto ni mlezi wake, ni dhahiri hatokuruhusu kuongea na mtoto peke yake hivyo toa taarifa mara moja kwa polisi au viongozi wa serikali ya mtaa husika.

Kuchunguza na Kusikiliza

Kuchunguza ni stadi muhimu ambayo Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii anapaswa kuitumia ili kusaidia kuelewa vitu katika njia ambayo haifungwi na mambo waliyoyazoea. Kila mtu hufungwa na mazoea ya jinsi yeye mwenyewe anavyoyaona mambo; Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ngazi ya Jamii wanaweza kutakiwa kuangalia ni masuala gani ya nyuma yanayoweza kuathiri mitazamo yao ya sasa na kujaribu nini wanaweza kukikosa wanapoonana mara ya kwanza.

Wakati wa matembezi ya nyumbani ni muhimu kutazama masuala muhimu yanayoweza kuboresha tathmini yako:

- Chunguza mtoto anahusiana vipi na mlezi.
- Angalia kama kuna rasilimali muhimu kwenye familia ambazo zinaweza kutumika kusaidia mtoto.
- Angalia kama mtoto ana jeraha la kimwili au michubuko inayo weza kuashiria unyanyasaji wa mtoto.
- Angalia mazingira ya nyumba kiujumla (mfano: je idadi ya watu inaendana na ukubwa wa nyumba? Usafi wa nyumba hukoje?)
- Angalia muonekano wa kimwili wa mtoto ili kutathmini hali yake ya kiafya na lishe.

Ni muhimu kutambua kuwa si mara zote kuwa muonekano lazima uonyeshe kitu kilichopo. Kwa mfano dalili za unyanyasaji wa mtoto nyingine ziko tofauti, (michubuko na mifupa iliyo vunjika) ambapo wakati mwingine muonekano wa mtoto si lazima uonyeshe kinacho mkuta. Si mara zote unyanyasaji unaweza kuonekana kwa viashiria vya wazi. (Kwa maelezo zaidi angalia taarifa za awali juu ya mada ya usimamizi wa Mashauri ya watoto.)

Kuhakiki Taarifa Toka Vyanzo Vingine Katika Jamii

Maarifa binafsi, uzoefu au mazingira vinaweza kuathiri jinsi msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii anavyoichukulia hali fulani, na watu wanaweza kumpa taarifa zisizo sahihi kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Ni vizuri kuthibitisha taarifa kutoka vyanzo vingine kwenye jamii, kwa mfano shuleni, Kituo cha Afya, majirani, viongozi wa eneo husika, watoto wengine na wahudumu wengine wa kujitolea. Hii inaweza kufanyika kwa:

- Kutembelea shule na kujadiliana na mwalimu anayehusika, mahudhurio ya mtoto, uwezo wa jumla wa kitaaluma wa mtoto, mabadiliko yoyote ya tabia yaliyojitokeza, jinsi anavyo jichanganya na watoto wengine, n.k.
- Kuogea na viongozi wa eneo husika na majirani juu ya hali ya familia kwa ujumla (kama kuna hali ya matendo ya ukatili waliyo yatambua, kama kupiga watoto, kutelekeza, hali ya maisha kiujumla, n.k.)

Mambo ya Kukumbuka

- Mara zote weka kumbukumbu ya mikutano ya watoto na familia zao katika jalada la shauri. Tumia shajala yako kuweka kumbukumbu muhimu za mawasiliano, majina, tarehe na matukio.
- Fanya ufuatiliaji walau mara moja kila baada ya wiki mbili.

- Jalada la kutunza kumbukumbu na nyaraka za siri, usimpatie mtu mwingine isipokuwa wale tu wenye jambo lakufanya katika shauri la mtoto.
- Hakikisha unaweka kumbukumbu za huduma zilizotolewa katika fomu ya kufatilia huduma za kila mwezi kwa ajili ya utoaji wa taarifa.

Kutoa Msaada kwa Watoto wenye Maambukizo ya VVU

Watoto wenye maambukizo ya VVU na UKIMWI siyo tu wanatakiwa kushughulikia madhara ya mwili bali pia wanakuwa na hisia zenye mkanganyiko. Changamoto nyingine zinzowakabili watoto wenye maabukizo ya VVU na UKIMWI ni:

- Kushughulikia unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya VVU na UKIWMI.
- Kukosa uwezo kuelezea msongo wanaoupata na kuwa na hisia za kujitenga.
- Kuwachukia wazazi. Hii ni kawaida kama mtoto amepata maambukizi wakati wa kuzaliwa.
- Kifo cha mzazi. Kwa kawaida mtoto hupitia hatua tano za maombolezo (kukana, kujutia, hasira, kujadili, kukubali na sononi).
- Maswali yasiyo na majibu.
- Kujihisi mnyonge mwenye hadhi ya chini, ambayo humfanya ajihisi ni tofauti.
- Matatizo ya kitabia yanayojitokeza ni kwa sababu ya kushindwa kuelezea hisia. Watoto wanaweza kuonyesha hizi hisia kwa kuwa na hasira, kutumia vilevi au kujitenga.
- Kukosa matumaini na uwezo wa kupanga kwa ajili ya maisha ya baadaye kuhusu elimu na mahusiano.
- Kupata shida katika ufuasi wa dawa za tiba ya VVU.

Fursa Zilizopo kwa Watoto wenye Maambukizoni Pamoja na:

- Kuwajengea uwezo watoto wengine wenye maabukizo ya VVU na UKIMWI
- Kinga chanya
- Kuwa watoa huduma za VVU na UKIMWI majumbani
- Kujiunga na vikundi vya kusaidiana ili kuishi maisha yenye ufanisi
- Kuwa wazi ili kuboresha uzoefu na taarifa
- Kufanya utetezi na kuwa chanzo cha motisha kwa wengine
- Kujiunga na klabu za watoto, vikiwemo vituo vya michezo mbalimbali
- Kushiriki katika michezo shuleni

Umuhimu wa WWKMH na Vijana Balehe Kupima VVU

Kila mtoto ana haki ya asili ya kuishi, ya kupata taarifa zinazo muhusu, kupata huduma msaada sahihi wa Huduma za Afya (stahiki za kisheria kwa mujibu wa mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya haki za mtoto na Sheria ya Mtoto ya Tanzania)

- Kuwezesha ufahamu wa mapema juu ya hali yao ya VVU.
- Kuboresha upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizo ya VVU, tiba, huduma na matunzo.
- Kuongeza uwezo wa kuishi kwa WWKMH na vijana balehe wenye maabukizo.
- Kuboresha hali ya kisaikolojia na afya ya akili kwa kiwango kinachostahili.
- Kuwatambua WWKMH ambao wanahitaji huduma ya kuziua maambukizi baada ya kugusana/kuingia kwenye mazingira yanayoweza kusababisha maambukizi.

Faida za Wazazi/Walezi wa WWKMH na Vijana Balehe Kufahamu Umuhimu wa Kupima VVU

- Kuwasaidia wazazi kuwalea watoto kwa kuwapatia huduma za VVU za kinga, tiba na matunzo.

- Kufahamu hali zao juu ya VVU na kupata huduma zinazostahili inasaidia kuboresha hali ya mtoto na kupunguza msongo kwa walezi.
- Msaada wa unasihi unasaidia watoto kujenga mbinu za kukabiliana na matatizo yanayotokana na VVU.
- Hii pia huwashawishi wazazi kutaka kujua hali zao juu ya VVU.

Umuhimu wa WWKMH na Vijana Balehe Kupima VVU kwa Jamii

- Kuifanya jamii ikubali kuwa ni kweli kuna WWKMH na vijana balehe wenye maabukizo ya VVU.
- Kufanya utetezi kwa ajili ya huduma bora kwa WWKMH na vijana balehe na familia zao.
- Kusaidia kupunguza unyanyapaa na ubaguzi.

Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Huduma za Upimaji na Unasihi

WWKMH/vijana balehe mara nyingi hawapati huduma za upimaji na unasihi za VVU kwa sababu ya unyanyapaa, ubaguzi, mila na desturi. Kupata vipimo mapema vya VVU husaidia kujisajili mapema kwenye huduma za tiba na kuwa na ufuasi mzuri wa tiba ya kufubaza VVU amabayo husaidia kuzuia maambukizi ya mapya. Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii wanaotoa huduma kwa WWKMH/vijana balehe walio katika hatari ya kupata maambukizo ya VVU ni lazima kuwezesha utambuzi kupitia tathmini ya hatari ya VVU na kuunganishwa na mpango wahuduma za upimaji na unasihi wa VVU ambao unatoa huduma kwa kuzingatia umri na utamaduni wa eneo husika.

Watoa Huduma za Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima wajenge uelewa kwenye jamii na uhitaji wa huduma za kupima na unasihii wa VVU kwa WWKMH/vijana balehe na famiia zao. Mchakato utahusisha utambuzi wa wanufaika walio katika hatari ya kupata maambukizo kwa kutumia nyenzo ya kufanya tathmini ya uhatarishi wa VVU, Kutoa taarifa juu ya wapi huduma zinakopatikana na kusaidia kupata huduma hizo kwa kuwaunganisha na familia na jitihada nyingine zinazowawezesha kupata huduma kama usafiri. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima afanye ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa rufaa zinafanikiwa.

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima atambue kuwa kuzuia maambukizo ya VVU kunaanza kwa mtu kufahamu hali yake juu ya maambukizi ya VVU. Kwa hiyo ni vizuri wafanye kazi na wadau wengine kufanya utetezi kwa ajili ya huduma za VVU za upimaji na unasihi katika jamii.

Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii Katika Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Huduma za Matibabu na Matunzo

Huduma na matibabu ya VVU ni muhimu kwa ustawi wa WWKMH na vijana balehe hususani wale wanye maambukizo na walioathiriwa na VVU. Ni lazima wahudhurie kliniki za upimaji na unasihi na kuwa wafuasi wazuri wa maelekezo ya tiba. Ingawa WWKMH na familia zao hawapati huduma za upimaji na unasihi, na wale wanaopata huduma wanaweza kuwa hawahudhurii kliniki ipasavyo au kuchukua na kutumia dawa kama inavyoelekezwa. Kuahakikisha kuwa wanaendelea kuunganishwa na kubaki katika huduma za VVU za matunzo na tiba kwa WWKMH, Msimamizi wa Mashauri kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi ni lazima afanye yafuatayo:

- Kwa kushirikiana na watoa huduma wengine asajili WWKMH na vijana balehe walio athirika na maabukizo ya VVU kwenye huduma za unasihi na upimaji.
- Fanya ufuatiliaji wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na familia zao waliosajiliwa na kupewa rufaa ili kuhakikisha kuwa wameanza kutumia dawa na ni wafuasi wazuri wa dawa na huduma za kufubaza virusi vya UKIMWI.

- Fanya utetezi wa kila WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU na UKIMWI ili wawe na mtu anaye aminika kumsadia kuwa mfuasi mzuri wa matibabu.
- Ukitembelea familia wakumbushe wazazi na walezi wawasaidie WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo kuwa wafuasi wazuri wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI.
- Waunganishe WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU kwenye huduma nyingine zinazosaidia kuwa na ufuasi mzuri wa tiba ya VVU zikiwemo huduma za kijamii.

Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Katika Kuwaunganisha WWKMH na Vijana Balehe na Familia Zao katika Huduma za Kuondoa Maambukizo ya VVU Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto

Mpango wa Kuondoa Maambukizo ya VVU Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto unalenga kuondoa maambukizo mapya kwa wanawake na watoto wao wanaojifungua. WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU wana mahitaji ya huduma za kuondoa maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima afanye ufuatiliaji na kuwasaidia wanawake wajawazito pamoja na familia zao kuwa wafuasi wazuri wa miongozo ya kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni lazima kufanya yafuatayo:

- Kufanya kazi na wadau wengine ili kujenga uelewa juu ya umuhimu wa huduma za kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kwa wanawake wajawazito, wenye umri mdogo na familia zao.
- Kushirikiana na wataalam wa afya katika kuwezesha upimaji wa VVU kwa wanawake wajawazito hasa wakilengwa vijana balehe, WWKMH, wanawake walio zaa katika umri mdogo na wazazi wao.
- Kufanya kazi na wahudumu wa afya katika jamii kuwezesha watu kubaki katika huduma ya kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.
- Kufanya kazi na wataalam ili kuwasaidia wanawake wajawazito kuwa wawazi juu ya hali zao za VVU kwa familia na wenzi wao.
- Kusaidia kuwauganisha na kutoa rufaa kwenye mipango ya kijamii ya kuwasaidia wajawazito walio katika mazingira hatarishi na wenye maambukizo ya VVU.
- Kuwaunganisha vijana balehe kwenye mipango ya ngono salama/huduma za kinga inayojumuisha mikakati ya kinga, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kondomu na tohara ya hiari kwa wanaume inayofanyika hospitalini.
- Kufanya utetezi na kuwataarifu WWKMH, vijana balehe, wakina mama wenye umri mdogo na walezi juu ya haki zao na utaratibu wa kisheria katika kushughulikia masuala ya ubaguzi na unyanyapaa.
- Kwa kushirikiana na watoa huduma za afya na watoa huduma wengine, kuwasaidia wanawake kuendelea na unyonyeshaji pekee kwa watoto wachanga kwa kipindi cha miezi sita.

Rufaa na Ufuatiliaji

Mfumo wa Rufaa ni Upi?

Mfumo huu unawezesha utoaji wa rufaa kwa WWKMH na walezi wao kwenda kwenye maeneo sahihi ya kutolea huduma na kufanya ufuatiliaji kuona kama WWKMH au walezi waliopewa rufaa wamepatiwa huduma zilizotarajiwa. Mfumo wa Rufaa unazingatia taarifa zote kutoka kwenye jamii kwenda kwa mtoa huduma na taarifa kutoka kwa mtoa huduma kwenda kwa jamii.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii hawatarajiwi kutoa huduma zote ambazo WWKMH na familia zao wanazihitaji. Stadi ya msingi wanayo takiwa kuwa nayo ni jinsi ya kutoa rufaa kwa mteja kwenye huduma inayoweza kupatikana na baadaye kufuatilia ili kuhakikisha kuwa mtoto anapata msaada anaohitaji.

Mfumo wa pande mbili unaoeleweka ni kiini cha mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ili kuweza kutoa huduma jumuishi. Mfumo huu uunganisha jamii na taasisi muhimu, mashirika na miundo mingine husika na husaidia ushirikiano na ubadilishanaji wa taarifa, huwezesha Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kupata huduma jumuishi zinazohusu afya, ustawi na ulinzi. Mfumo wa rufaa wa pande mbiliunahusisha yafuatayo:

- Rufaa zilizotolewa kwenda kwenye taasisi za afya na rufaa toka taasisi za afya kwenda kwenye huduma za kijamii kama ilivyoelezwa hapo juu.
- Rufaa zilizotolewa kutoka kwenye jamii kwenda shuleni, mashirika mengine na watoa huduma wengine na kutoka shuleni, mashirika/watoa huduma kwenda kwenye jamii mahala popote na wakati wowote suala likijitokeza.
- Kutambua na kuondoa vikwazo vinavyozuia ubadilishanaji wa taarifa muhimu kwa huduma jumuishi.
- Kujenga mahusiano yenye mpangilio na kubadilishana taarifa kwa kupitia mikutano ya mara kwa mara walau kwa kiwango cha chini kila mwezi ikihusisha taasisi/mashirika ya kiraia na watoa huduma katika jamii (Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii).
- Mfumo wenye muundo wa ufuatiliaji katika rufaa zote ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukamilifu katika mchakato mzima wa rufaa.

Chini ya mfumo wa kitaifa wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto, Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ya Watoto Katika Jamii watajenga uhusiano na taasisi au mashirika. Mfano taasisi za afya, mashirika ya kiraia na shule. Kwa kuwa na Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii wenye uhusiano na zahanati, shule na mashirika mengine inakuza uhusiano unaodumu na kuwafanya waonekane kama rasilimali kwenye jamii na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa watoto na kufanya mawasiliano juu ya uhatarishi uliopo kwa lengo la kufanya tathmini na kutoa huduma.

Rufaa inaweza kuhitajika katika hatua mbili za mchakato wa usimamizi wa mashauri:

- Wakati wa Usaili - Mtu yeyote anayewasilana na mtoto na/au familia kwa ajili ya kupata msaada ni lazima ajue jinsi ya kutoa rufaa kwa taasisi inayotoa huduma za ulinzi kwa mtoto. Ikiwa kutakuwa na unyanyasaji wa kingono au jinai nyingine dhidi ya mtoto shauri hilo la mtoto litolewe taarifa mara moja kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya; na
- Wakati wa utekelezaji wa mpango wa huduma.

Kama kanuni kuu, Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima watoe rufaa kama:

- Shauri ni la ulinzi wa mtoto na linahitaji afua ya kisheria mfano unyanyasaji wa kingono.
- Wana mashaka na uwezo wao juu ya kushughulikia shauri husika.
- Suala la mtoto linahitaji utaalam fulani.
- Wana wasiwasi na hali ya mtoto kimwili, kijamii au kihisia.
- Kuna mabadiliko katika hali ya mtoto kimwili, kihisia au kijamii na kuna haja ya kufanya tathmini ya kitaalam ili kupata huduma mpya, tofauti au zaidi. Hii ni muhimu hasa kwa watoto wanaotumia huduma za tiba ya kufubaza VVU.
- Mtoto anahamia sehemu mpya na anatakiwa kuunganishwa kwa wafanyakazi wapya na taasisi.
- Kuna masuala ya kimaadili kuhusiana na mtoto na wanaamini kuwa mtu mwingine anaweza kutoa huduma nzuri zaidi.

Kabla ya kutoa rufaa yoyote ni muhimu kupata taarifa zilizohuishwa kuhusiana na huduma zilizopo katika eneo linalo hudumiwa na Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii. Huduma hizo ni pamoja na:

- Afya
- Ustawi wa Jamii
- Ulinzi Elimu
- Msaada wa kisheria Elimu ya Malezi Makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto
- Kupima VVU na ukimwi Unasihi
- Msaada wa kiroho Msaada wa kisaikolojia
- Makazi ya muda n.k

Mifano Mizuri ya Rufaa

- Fahamu huduma zinazotolewa na watumishi wanaozitoa. Huisha kitabu chenye maelezo ya watoa huduma mara kwa mara.
- Tambua vigezo vinavyotumiwa nashirika/taasisi katika kutoa huduma - siyo kila mtu anastahili kuhudumiwa.
- Tafuta ni wapi kwingine ambapo familia pamoja na watoto wamewahi kupata huduma. Haitakuwa sahihi kuwapa rufaa wateja kwenda kwenye maeneo yaleyale ambayo hawakupata huduma au hawakukidhi vigezo.
- Kuwa makini na taarifa zinazotolewa wakati wa kutoa rufaa; suala la usiri ni muhimu zaidi
- Chunguza utayari wa mtoto au mlezi kupewa rufaa. Mjadala uliowazi na ukweli kuhusu rufaa vitawafanya mtoto na walezi wajisikie kuwa jambo hilo wanalimudu. Kama kutakuwa na kuchagua huduma zilizopo, ni lazima Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ahakikishe kuwa mtoto aumlezi wana taarifa kuhusu kila huduma na wanaweza kufanya maamuzi ya jambo wanalolifahamu.
- Wasindikize mtoto/familia kwenda kwenye huduma kama inawezekana.
- Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii mara zote ni lazima ajaze fomu ya rufaa kila anapotoa rufaa kwa watoto kwenda kwenye huduma na kuadika matokeo ya huduma katika shajala zao.
- Rufaa zote ziandikwe katika kitabu/ukurasa wa kumbukumbu za mashauri.

Kanuni muhimu za usimamizi wa mashauri katika kutoa rufaa:

- Zingatia usiri
- Mshirikishe mtoto na familia katika kufanya maamuzi
- Hakikisha wanaelewa kuhusu maamuzi yaliyofikiwa

Changamoto Zinazojitokeza Mara kwa Mara Katika Kutoa Rufaa

Changamoto (mifano)	Suluhu (mifano)
Shauri kuhusisha taasisi nyingi/ linahusisha mahojiano mengi	Kama shauri linahusisha taasisi nyingi au watoa huduma za mashauri ya watoto, toa jukumu hili kwa "Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Kiongozi" ili kufanya tathmini na mpango mmoja wa huduma na kuhakikisha kuwa mawasiliano yote kati ya mtoto na familia yanaratibiwa.
Kukosekana huduma za rufaa/ Huduma zisizo na mtiririko mzuri	Kushughulikia mapungufu katika kutoa huduma kwa kushirikiaana na serikali, wafadhili na taasisi nyingine (kwa kutumia stadi za utetezi).
Kukosa mrejesho katika rufaa iliyotolewa	Usitoe rufaa mpaka utakapo kuwa na uhakika kuwa mtoa huduma ana uwezo wa kutoa huduma hiyo. Mpigie simu mtoa huduma ili ujue lipilinalowezekana kabla ya kumpa taarifa kuhusu rufaa. Msindikize mtoto au familia kwenda kwenye huduma. Fanya mihadi na watoa huduma kwa ajili ya mtoto na familia na wasindikize kwenda kwenye huduma kwa mara ya kwanza. Kama wataamua kwenda wenyewe baadaye unaweza kupiga simu kujua walihudumiwaje na kuwasisitiza waendelee kuhudhuria.
Watoa huduma wanahitaji taarifa za siri kuhusu shauri (mfano: kuthibitisha hali ya mtoto/ kujiridhisha kwa huduma watakayo toa).	Hii mara nyingi si sahihi. Tengeneza mkataba wa huduma na taasisi mojamoja ili kuweka wazi kanuni za kusimamia mashauri ya watoto na kukubaliana ni taarifa gani zinazoweza kutolewa na ni zipi zitaendelea kuwa ni siri na ni huduma zipi zinazopatikana.
Hakuna mfumo wa kufuatilia rufaa zilizotolewa	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ana wajibu wa jumla wa kuhakikisha kuwa kuna ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa. Weka kumbukumbu kwa maadishi kwa rufaa zote zilizotolewa na idadi yake. Ongeza maelezo ya kukumbusha kufanya ufuatiliaji katika shajala yako/mfumo wa kutunza taarifa.

Kuwasaidia Watoto Katika Kupata Huduma Nyingine za Kijamii

Katika mchakato wa Usimamizi wa Mashauri, Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni lazima aendelee kuwezesha WWKMH wakiwemo vijana balehe wenye maambukizo ya VVU wote kuunganishwa na huduma za kijamii. Huduma za kijamii ni kiini cha majukumu ya Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii kwa sababu zinapunguza uhatarishi kwa WWKMH na zinasaidia katika kudhibiti VVU kwa kushughulikia masuala ya kijamii yanayochangia maabukizi. Huduma za kijamii ni pamoja na:

- Ulinzi kwa mtoto
- Huduma na msaada wa kisaikolojia
- Kuimarisha uchumi wa kaya
- Chakula
- Afya
- Elimu

Malezi na Ulinzi wa Mtoto

Ulinzi kwa watoto na vijana balehe wakiwemo wasichana wadogo ni kuzuia na kukabiliana na ukatili, unyonyaji, utelekezaji na unyanyasaji wa watoto. Watoto na vijana balehe hasa wenye maambukizi na walioathirika na VVU wapo katika hatari zaidi ya kunyanyaswa na kufanyiwa ukatili mwingine. Unyanyasaji usababisha kuongezeka kwa tabia hatarishi za kingono kwa vijana balehe na hatari kwa watoto wengine ukiwemo ugonjwa, matatizo ya afya ya akili, na kuishi mtaani. Vipengele muhimu katika huduma za ulinzi ni pamoja na unasihi, huduma za kisheria na matibabu, pamoja na rufaa nakuwaunganisha kwenye huduma nyingine za ulinzi.

Ukatili Dhidi ya Watoto

Ukatili dhidi ya watoto uhusisha tabia na vitendo vya makusudi vya kutumia nguvu katika kudhuru, kuumiza au hata kuua mtu.

- **Unyanyasaji wa kihisia**: Hii ni pamoja na kuitwa jina baya, kufanya mtu ajisikie hatakiwi au kitisho cha kuachwa pweke
- **Ukatili wa kimwili:** Ukatili wa kimwili kama kupigwa makofi, ngumi, kusukumwa, kupigwa mateke, kutiwa singi au kutishiwa kwa silaha kama buduki na kisu
- **Ukatili wa kingono:** Matendo yote ya kingono ambayo ni kinyume na matakwa ya mtu yakihusisha matendo ambayo ni kinyume na sheria ikiwemo ngono ya kulazimisha (ubakaji), kujaribu kubaka, kupapasa, vitisho vya kingono, kuonyesha picha za ngono na matusi
- **Kutelekezwa:** Huu ni wakati ambao mzazi/mlezi amemtelekeza mtoto na hana mawasiliano naye na hivyo hatoi huduma kwa mahitaji ya mtoto

Aina za Unyanyasaji Dhidi ya Mtoto

Unyanyasaji ni aina yoyote ya kitendo cha kumsababishia mtoto madhara ya kimwili, kihisia, ukatili wa kingono, utelekezwaji, unyonyaji na hivyo kuathiri afya, uhai, maendeleo na utu wa mtoto katika misingi ya uhusiano, majukumu, uwezo au kuaminiana (WHO, 1999 & 2002). Vitendo hivi vya unyanyasaji ni kama:

- Unyayasaji wa kimwili ikiwemo kupiga, kusukuma, kufinya, kupiga vibao.
- Unyanyasaji wa kihisia, uchokozi, kuita majina mabaya, kumfanya mtoto ajisikie vibaya.
- Kutelekeza, kushindwa kwa makusudi kumpatia mtoto mahitaji yake ya msingi ya kimwili na/au ya kisaikolojia kama vile kushindwa kutoa chakula cha kutosha, makazi na mavazi.

- Usafirishaji wa watoto - kuwaandaa, kuwasafirisha na kuwanyonya watoto kwa njia ya kuwatumikisha/kuwatumikisha nyumbani kama watumwa au kuwatumia kwa ngono. Wasafirishaji hutoa ahadi za uongo na hutumia fursa hiyo kujinufaisha wao binafsi.
- Ukeketaji - kuondoa sehemu ya kisimi au kisimi chote cha wasichana na wanawake walio katika umri mdogo kusikokuwa na malengo ya kimatibabu (mara zote hufanyika kwa sababu za kiutamaduni).
- Unyasasaji wa kingono na unyonyaji - kumlazimisha mtoto kushiriki katika ngono ya kimwili au isiyo ya kimwili. Tendo lolote au jaribio la kutumia mamlaka au kukubalika kwa lengo la kufanya ngono ili kunufaika na pesa, kijamii au kisiasa.

Utamtambuaje Mtoto Aliye Nyanyaswa au Ambaye Yupo Katika Hatari ya Kunyanyaswa

Ukiwa Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii, kama utaona dalili zifuatazo, itabidi ufungue shauri na kufanya tathmini ya awali itakayokusaidia kuamua kama shauri hilo lipo ndani ya uwezo wako au utahitaji kutoa rufaa kwenda kwa mtoa huduma mwingine kadiri ya mahitaji yalivyotambuliwa. Maeneo ya kupeleka rufaa yanaweza kuwa ni Afisa Ustawi wa Jamii, Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi, asasi za kiraia, hosipitali, Timu ya Ulinzi na usalama wa Mtoto, Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto n.k. Dalili hizo ni:

- Ushahidi kuwa kuna majeraha ya kimwili, majeraha kwa sababu ya ngono
- Mabadiliko ya tabia kama kutokutabirika, kukataa kwenda shule, kukojoa kitandani, kupatwa na majinamizi, kukosa hamu ya kula na kujitenga
- Mshtuko, kujitenga na jamii, kutoamini watu na woga

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii Wanaweza Kufanya Yafuatayo Wakati wa Kushughulikia Mashauri ya Unyanyasaji:

- Kutambua mashauri ya unyanyasaji
- Kuweka vipaumbele vya Mashauri ya Watoto
- Kutoa rufaa ya shauri kwenda kwa Afisa Ustawi wa Jamii/polisi/hospitali
- Kufuatilia mashauri baada ya masuala ya sheria kukamilika
- Kushirikiana na wadau wengine kuongeza uelewa kwenye jamii juu ya kuzuia na kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa mtoto

Mtoto kama ni mhanga wa unyanyasaji anaweza kuathiriwa na masuala mbalimbali kama mimba au kuacha shule ambayo inaweza kusababisha tabia hasi kama hasira, matumizi ya pombe na dawa, kufanya ngono hatarishi na kujiona kuwa thamani yake ni ya chini.

Huduma na Msaada wa Kisaikolojia

Msaada wa Kisaikolojia unalenga kuwajengea uwezo watu kutatua matatizo yao wenyewe. Kwa kutatua tatizo tu, mtu unayemsaidia hatajenga stadi ya kutatua tatizo hilo mwenyewe siku za mbele. Kwa hiyo ni vizuri kumjengea uwezo au kumsaidia mteja/familia kutafuta ufumbuzi wa tatizo wao wenyewe.

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anaweza kufanya yafuatayo katika kuwasaidia WWKMH kupata msaada wa kisaikolojia.

Hatua ya 1: Baini tatizo

- Muombe mteja afafanue tatizo au changamoto
- Uliza kuhusu taarifa mahususi ili kwa pamoja mlenge katika tatizo moja kwa wakati mmoja

Hatua ya 2: Lielewe tatizo

- Uliza maswali yatakayo kusaidia wewe na mteja kulielewa tatizo
    - Hili limekuwa tatizo kwa muda gani?
    - Tatizo linasababishwa na nini?
    - Kuna mizizi ya tatizo?
    - Wahusika katika tatizo hili ni akina nani?

Hatua ya 3: Fikiria njia za utatuzi zinazowezekana

- Msaidie mteja afikirie kuhusu njia zote za utatuzi zinazowezekana
- Kadiri utakavyoweza mfanye mtu unayemsaidia afikirie mwenyewe njia za utatuzi zinazowezekana
- Ongeza njia za utatuzi pale ambapo utaona kuwa mtu ameelezea njia zote anazozijua

Hatua ya 4: Zichambue njia za utatuzi na chagua iliyo nzuri kuliko zote

- Tafakari njia zote za utatuzi na msaidie mteja kutambua faida na hasara ya kila njia ya utatuzi
- Tambua njia ya utatuzi ambayo haitegemei msaada wanje pekee
- Kupitia majadiliano, msaidie mtu achague njia ya utatuzi iliyo bora kuliko zote
    - Njia bora ya utatuzi kuliko zote ni lazima iwe na faida zaidi, hasara kidogo na ni kitu ambacho mteja ataanza kukifanyiakazi mara moja.

Hatua ya 5: Tengeneza mpango wa huduma ya kisaikolojia

- Kwa kuzingatia njia ya utatuzi iliyochaguliwa, msaidie muhusika kutengeneza mpango wa huduma ya kisaikolojia.
- Ugawanye utatuzi katika hatua ndogo ndogo na kukubaliana juu ya muda wa ufuatiliaji wa kila hatua.

Hatua ya 6: Fuatilia

- Fuatilia mara kwamara ili kujua mhusika anaendeleaje
- Kama ufumbuzi hautaleta matokeo yanayotarajiwa, chagua njia nyingine ya utatuzi kutoka kwenye orodha ya utatuzi unaowezekana ya awali.

ZINGATIA: Ni muhimu kusisitiza kuwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Kwenye Jamii wanaweza kuwasaidia WWKMH kupata huduma na msaada wa kisaikolojia kwa kupitia rufaa na kuwaunganisha kwenye vilabu vya watoto, makundi ya kusaidiana n.k pia rufaa za Ulinzi na usalama wa Mtoto.

Kuimarisha Uchumi wa Kaya

Kuwasaidia walezi, hususan wanawake na vijana balehe kukidhi mahitaji yao naya watoto wao, kuimarisha uwezo wa muda murefu wa familia wa kuhudumia WWKMH na vijana balehe. Kwa hiyo ni muhimu kuwezesha kaya kujitegemea kwa kupitia fursa zilizoboreshwaza kujipatia kipato, mali na njia bora za kutunza pesa na rasilimali nyinginezo.

Shughuli hizi zinawezesha uboreshaji wa kiuchumi wa wanakaya na hali za WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU na watoto wenine kwenye familia. Uchumi wa familia ukiwa imara unawezesha hata upatikanaji wa dawa na huduma za kufubaza virusi vya UKIMWI na ufuasi mzuri wa dawa.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii wanaweza kufanya yafuatayo:

- Kufanya tathmini ya kipato kabla na baada ya afua ili kutambua afua stahiki kwa kaya mojamoja; programu zingine zinaweza kujumuisha hili katika tathmini ya mradi mahususi.
- Kufuatilia matokeo ya afua ili kuhakikisha kuwa uwezo wa kaya unaboreka katika kukidhi mahitaji ya wanakaya wakiwemo WWKMH na vijana balehe.
- Kuunganisha kaya zenye WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU na Maafisa Ugani wa Kilimo na Mifugo kwa ajili ya msaada wa kitaalam wa kuongeza tija katika mashamba yao.
- Kushirikiana na maafisa ugani (mfano: Maafisa Kilimo wa Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Elimu wa Kata, Maafisa Ustawi wa Jamii, n.k) na kaya ili kutambua fursa za kuingiza kipato katika kaya.
- Kuwawezesha vijana balehe na walezi wa WWKMH kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa na taasisi za kutoa mikopo midogo midogo.
- Kuwaunganusha wanakaya na shughuli zinazoboresha stadi za utunzaji wa fedha na elimu juu ya fedha.
- Kuwaunganisha WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo zikiwemo kaya ambazo wakuu wake ni watoto na wanaoishi na wazee au walezi wagonjwa wa muda mrefu, na TASAF na miradi mingine ya ulinzi kwa ajili ya uwezeshaji kiuchumi na kuboreka kijamii.
- Unganisha wanakaya kwenye mafunzo ya msingi ya ujasiliamali yaliyopo katika jamii (mfano juu ya kuandaa bajeti, kupanga, kuweka akiba, kutunza kumbukumbu na masoko).
- Unganisha kaya zenye watu wenye VVU wakiwemo WWKMH, vijana balehe, wanawake waliozaa katika umri mdogo na kaya za watu walio katika makundi maalum kwenye shughuli za kuingiza kipato zinazoongozwa na soko na pia kwenye soko la bidhaa zao.

Uhakika wa Chakula na Lishe

Uhakika wa chakula si suala la msingi tu kwa kuondoa uhatarishi bali pia katika kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI. WWKMH na walezi wenye chakula cha kutosha na kinachotakiwa wana uwezekano mkubwa wa kuwa na afya bora na pia kuwa wafuasi wazuri wa matibabu. Upatikanaji wa vyakula vya aina mbalimbali ni muhimu kwa watu wote, hususani kwa watoto waliochini ya miaka mitano, WWKMH wenye maambukizi ya VVU, vijana balehe, wanawake wajawazito, na wanawake wanaonyonyesha wenye maambukizi ya VVU kwa ajili ya kuboresha afya zao na kuboresha kinga kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa nyemelezi.

Kwa sababu hiyo, huduma muhimu kwa ajili ya msaada wa kijamii inajumuisha utoaji wa huduma zinazowezesha upatikanaji wa chakula wa uhakika kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi pamoja na familia zao. Jamii na walezi ni lazima kupata chakula cha kutosha, salama na chenye virutubisho vinavyokidhi viwango vya mahitaji ya lishe kwa watoto na vijana balehe wenye maambukizoya VVU na walezi wao.

Ili kuwasaidia WWKMH na vijana balehe, hasa wenye maabukizi ya VVU kubaki na hali nzuri ya lishe, Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni lazima afanye yafuatayo:

- Afanye kazi na Muhudumu wa Afya kwa Jamii kwa kushauriana na Mtaalam wa Lishe ili kufanya tathmini ya lishe, unasihi na huduma; kufatilia rufaa ili kuhakikisha kuwa watoto wenye utapiamlo wanapata huduma inayostahili.
- Unganisha na fanya kazi na wataalam wa afyana lishe katika kuwaelimisha WWKMH wakiwemo vijana balehe, wanawake waliozaa katika umri mdogo Wenye Maambukizo ya VVU na walezi juu ya tabia ya ulaji sahihi na mtindo wa maisha wenye afya ikiwemo matumizi ya vyakula vinavyolimwa katika eneo lao.

- Toa maelekezo ya jinsi ya kuandaa chakula kwa usafi na jinsi ya kukiifadhi kwa matumizi ya baadaye.
- Fanyakazi na wataalam wa lishe na watoa huduma wengine kwenye jamii waliopatiwa mafunzo katika kutathmini, kufanya unasihi na kuwahudumia WWKMH, vijana balehe na wanawake waliozaa katika umri mdogo wenye maabukizi ya VVU kwa kutumia jukwaa la Lishe la kutathmini, kufanya unasihi na kuhudumia.
- Shirikiana na serikali ya mtaa na wadau wengine katika kuhamasisha wanajamii ili kusaidia WWKMH, vijana balehe na kaya zenye uhaba chakula pale walenzi wanaposhindwa kujisimamia wenyewe.
- Hamasisha na unganisha kaya zenye uhaba wa chakula za WWKMH na vijana balehe kwenye taasisi zinazoweza kusaidia (mfano: mashirika ya kijamii, mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za serikali).
- Zishawishi familia kuanzisha kilimo mchanganyiko cha mboga na matunda, bustani ndogo ndogo, ufugaji wa kuku wa mayai na mifugo mingine ili kuhakikisha kuwa uhakika wa upatikanaji wa chakula wa kudumu unaongezeka.
- Toa elimu kuhusu mila na desturi zinazokataza ulaji wa vyakula vyenye virutubisho fulani kwenye jamii.

Afya ya Mtoto

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ana jukumu muhimu katika kuhudumia afya za Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi.

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anaweza kufanya yafuatayo:

- Kusaidia kaya zenye Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kunufaika na huduma za afya kwa kuwaunganisha na mifuko ya afya iliyopo kwenye jamii. Ni vizuri kuanzia katika ngazi ya mwanzo ya jamii kwa sababu kila halmashauri ina njia yake ka kushughulikia masuala ya afya ya watu wake katika jamii.
- Saidia wanakaya wanaotoka kwenye kaya zenye WWKMH kujisajili katika Mfuko wa Afya wa Jamii ili waweze kupata huduma za afya kwa mwaka mzima kwa gharama nafuu.
- Wasaidie WWKMH wenye umri chini ya miaka mitano kupata huduma bure za afya zilizopo kupitia serikali kama za chanjo.
- Waunganishe WWKMH na vijana balehe na taasisi za afya kama vile tiba ya kifua kikuu, afya uzazi ikiwemo uzazi wa mpango.
- Wasaidie WWKMH na vijana balehe pamoja na famila zao kupima VVU, unasihi na matibabu pamoja na kutoa rufaa kadiri ya mahitaji na kufuatilia rufaa hizo.

ZINGATIA: Watoto wengine wanaweza kuwa na maambukizo ya VVU lakini hawana dalili. Ni muhimu kutoa rufaa kwa watoto walio katika hatari ya kupata maabukizo ya VVU kwenda kupima VVU na kupata unasihi. Siyo WWKMH wote watatakiwa kupewa rufaa kwenda kwenye huduma ya upimaji wa VVU na unasihi, bali WWKMH walio wahi kulazwa hospitalini siku za nyuma, wana ugonjwa wa ngozi unaojirudia, wamefiwa na mzazi mmoja au wote wawili, wamekuwa na afya mbaya kwa miezi mitatu, wenye wazazi au mwanafamilia mwenye magonjwa ya kusendeka, wenye utapiamlo, waliopimwa na kukutwa na kifua kikuu, wanoishi katika kaya ambazo wakuu wake ni watoto au wanaoishi mtaani, walionyanyaswana wenye viashiria vingine vya hatari vya VVU.

Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Elimu ni haki ya msingi kwa watoto wote. WWKMH au vijana balehe wanaopata elimu bora na mafunzo ya ufundi stadi wanapata fursa zaidi ya kuboresha stadi za maisha, kujiamini na kuvunja mduara wa umaskini. Kwenda shuleni kunapunguza uwezekano wa kujihusisha na tabia za ngono hatarisha zinazoweza kusababisha maambukizi ya VVU, hasa kwa vijana balehe na wasichana walio katika shule za msingi na sekondari.

Ongezeko la WWKMH na vijana balehe wakiwemo waliothirika na wenye maambukizo ya VVU wanahitaji kusaidiwa kupata elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Jamii ni lazima wasaidie WWKMH na vijana balehe kupata fursa za elimu kwa kuwaunganisha na wadau mbalimbali wanaotoa huduma za elimu.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Wanaweza Kufanya Yafuatayo:

- Kutathmini mahitaji ya elimu ya WWKMH na vijana balehe walioathirika/wenye maambukizo ya VVU ambao walistahili kuwa shuleni lakini kwa sasa hawapo shuleni.
- Wasaidie walezi ili wawaandikishe shule WWKMH na waendelee kuhudhuria na kuwa na maendeleo mazuri shuleni.
- Wawezeshe WWKMH wenye umri kati ya miaka 2-4 kuandikishwa katika vituo vya malezi ya awali ya watoto kwa ajili ya kupata malezi changamshi ya awali.
- Wawezeshe WWKMH wenye umri wa miaka 5 na zaidi kuandikishwa katika shule ya msingi. Zingatia umbali ambao watoto watatembea kwenda shule kwa ajili ya usalama na kupunguza uwezekano wa watoto kuacha shule.
- Kuwaunganisha kwenye fursa za mafunzo ya ufundi stadi yanayozingatia mahitaji ya soko WWKMH na vijana balehe wenye maabukizi ya VVU wenye umri mkubwa pale inapostahili.
- Fanyakazi na wataalam ili kuwawezesha WWKMH kuweza kupata huduma sawa za makuzi ya awali ya watoto ikiwemo chanjo, ufuatiliaji wa makuzi, lishe na uchangamshi wa awali.
- Tafuta rasilimali kwa kushirikiaana na wadau wengine (mfano: viongozi wa kijiji/mtaa, mashirika ya kijamii, mashirika ya kidini, watu mbalimbali, sekta binafsi) ili kukidhi gharama za elimu kwa ajili ya WWKMH na vijana balehe hasa wale wenye maambukizo ya VVU, wanaoishi kwenye kaya ambazo wakuu wake ni watoto au wazee, walezi wenye ugonjwa wa kusendeka na wenye ulemavu.
- Kufanya utetezi kwa ajili ya huduma ya chakula shuleni ili kuhakikisha kuwa watoto wenye maambukizo wanabaki shuleni na wanapata lishe. Kwa kushirikiana na wazazi, walimu na walezi kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni na kwenye vyuo vya ufundi stadi na kujadili taarifa zilizopatikana wakati wa ufuatiliaji.
- Waunganishe WWKMH ili wajiunge na programu za baada ya kumaliza shule ya msingi ili kuwawezesha kujiunga na sekondari.
- Shirikiana na wadau kujenga uelewa juu ya masuala ya ubaguzi na unyanyapaa shuleni kwa WWKMH na vijana balehe wenye maambukizo ya VVU.
- Toa taarifa juu ya ubaguzi na unyanyapaa kwa mamlaka husika (mfano walimu, viongozi wa kijiji/mtaa, Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto, kamati ya shule, huduma za VVU kwenye Jamii
- Shirikiana na wadau wengine (Mashirika ya Kijamii, Mashirika yasiyo ya serikali na Mashirika ya Dini) katika kuondoa vikwazo vya kupata elimu kwa wasichana.

Huduma na Matunzo ya Kifamilia na Makazi

Kupata matunzo katika familia ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mtoto anastawi na kulindwa. Watoto wanakua vizuri kimwili, kiakili, kihisia, kiroho na kijamii wakilelewa kwa upendo na wazazi au walezi. Kwa hiyo ni muhimu kwa WWKMH na vijana balehe hasa waliothiriwa na wenye maambukizo ya VVU kulelewa katika familia salama na yenye mazingira wezeshi, kwa kulelewa na walezi wenye umri mkubwa wanaotimiza wajibu wao na kuangalia masuala mazima ya ustawi na ulinzi wa mtoto.

Mazingira hayo yanasaidia mtoto kupata huduma muhimu za kutosha kwa mahitaji, ulinzi na huduma ya matibabu ya kufubaza VVU na ufuasi wa dawa, taasisi kama makao ya kulelea watoto iwe suluhisho la mwisho.

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Wanaweza Kufanya Yafuatayo:

- Kuwatambua na kuwahamasisha wadau waliopo (mfano: wanajamii, mashirika yasiyo ya Serikali, mashirika ya dini) kusaidia upatikanaji wa huduma ya kuboresha makazi kwa WWKMH na vijana balehe waliathirika na wenye maambukizo ya VVU
- Hamasisha wanajamii kuhakikisha kuwa WWKMH na vijana balehe walioathirika na wenye maambukizo ya VVU wanapata huduma sahihi za mavazi na malazi.
- Waunganishe walezi na huduma ya usajili wa vizazi na vifo.
- Waunganishe WWKMH na vijana balehe waliothirika na wenye maambukizo ya VVU kwenye taasisi za kisheria kwa msaada mahususi unaohusiana na masuala ya VVU kama vile yanayohusiana na urithi, ukatili wa kijinsia na waliowahi kunyanyaswa.
- Shirikiana na wataalam (Maafisa Ustawi wa Jamii) kuwatambua Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi walio katika hali ya hatari kama wale wanaoishi kwenye kaya zinazosimamiwa na watoto, watoto wanaoishi na kufanyakazi mitaani, wasichana wadogo wanofanya biashara ya ngono.
- Waunganishe na watoa huduma ili kukidhi mahitaji mahususi na dalili za uhatarishi zilizopo hususani zinazochangia maambukizi ya VVU.
- Shirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii wa Kata kuwatambua watoto ambao hawana malezi ya kifamilia (kama vilewaliotelekezwa, waliotenganishwa, wasio na watu wa kuambatana nao, watoto wanaoishi na kufanyakazi mtaani).
- Tathmini na shughulikia mahitaji mahususi ya WWKMH na vijana balehe na waunganishe kwenye huduma sahihi zilizo tathminiwa za malezi ya kambo na pale itakapokuwa sahihi na salama warejeshe kwenye familia zao.
- Shirikiana na wataalam kuwaunganisha tenawatoto na famila zao au kuwaunganisha na walezi wengine mbadala.
- Kwa kushirikiana na Afisa Ustawi wa Kata, wahudumu wa afya na wadau wengine kuwezesha mafunzo juu ya malezi kwa walezi wa WWKMH na vijana balehe walioathirika na wenye maabukizi ya VVU kwa kulenga kupima na unasihijuu ya VVU, huduma, ufuasi wa dawa, kupunguza unyanyapaa na ubaguzi.

Changamoto Unazoweza Kukutana nazo kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Katika kipindi cha kufanyakazi kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi Jamii unaweza kukutana na changamoto nyingi. Ni vizuri kujiandaa kwa ajili ya changamoto hizo na kujua jinsi ya kuzishughulikia.

Kama familia inamlinda mnyanyasaji na itatishia maisha yako.

Katika hali hii unatakiwa kufanya nini?

- Toa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii kuhusiana na shauri hilo kadiri ya taratibu za utoaji taarifa zilivyo.
- Usigombane na familia; badala yake toa taarifa juu ya unyanyasaji na vitisho kwenye kituo cha polisi kilichopo karibu. Pia toa taarifa kwa kiongozi wa mtaa (mwenyekiti/mtendaji wa mtaa).

Mtuhumiwa aliyetolewa taarifa baada ya muda anaonekana huru anatembea mitaani na jamii inaanza kuhoji juu ya uwezo wako katika kuwahudumia watoto.

Katika hali hii unatakiwa kufanya nini?

- Ni lazima kufanya ufuatiliaji na polisi pamoja na Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya na kutoa mrejesho kwenye kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto.
- Shirikiana na wadau wengine katika eneo lako hususan taasisi zinazoshughulika na haki za binadamu/watoto.

Umeitwa kutoa ushaidi kwenye shauri la unyanyasaji.

Katika hali hii unatakiwa kufanya nini?

- Unatakiwa kutoa taarifa katika kituo cha polisi cha karibukwa madhara na usumbufu kama shahidi.
- Pia epuka kutembea peke yako usiku hasa kunapokuwa na tishio la maisha yako.

Familia inahisi unaingilia mambo yao ya ndani na hawaitaji msaada wako.

Katika hali hii unatakiwa kufanya nini?

- Jitambulishe kwa unyenyekevu na eleza kwa ufasaha malengo ya kuwatembelea na majukumu yako kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Katika Ngazi Jamii.
- Kama familia itazidi kuonyesha haihitaji msaada wako, haina haja ya kuwalazimisha au kuwatisha, ila toa taarifa kwa Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea.
- Zingatia muongozo wa majukumu yako kuwa upo kwa ajili ya kuwalinda watoto na endelea kutoa taarifa za shauri kwa kuzingatia taratibu za kazi.

ZINGATIA: Ni muhimu kujitambulisha/kumtembelea kiongozi wa mtaa wa eneo unalofanya kazi (mjumbe wa nyumba kumi) kabla ya kufanya mahusiano na kaya yoyote au familia.

Mambo Ambayo Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Anatakiwa Kufanya na Asiyotakiwa Kufanya

Anayotakiwa Kufanya

- Mara zote tunza kwa usiri taarifa zote zinazohusiana na mashauri ya watoto unayoyashughulikia.
- Heshimu utu wa watoto na usipige au kudhuru au kunyanyasa watoto.
- Toa taarifa bila woga juu ya shauri la ukatili wowote utakaouhisi, kusikia au kuletewa
- Usijihusishe na uhusiano wa kingono na wateja wakiwemo watoto wanaonyonywa kwa kufanya biashara ya ngono.

Asiyotakiwa Kufanya

- Usitumie nafasi yako moja kwa moja au kupitia njia nyingine kuwanyonya watoto au kuwaweka katika hali itakayowaweka katika uhatarishi wa njia yoyote ya unyonyaji.

Matunzo Binafsi (Kwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii)

Kwa aina ya mashauri utakayoyashughulikia, kuna uwezekano wa kupata uchovu na itakupunguzia nguvu. Wakati mwingine utachanganyikiwa kwa sababu mashauri yanaweza yasishughulikiwe kwa kasi uliyotarajia. Ifuatayo ni mikakati unayoweza kutumia kwa ajili ya matunzo binafsi:

- Nenda taratibu: Unatakiwa ujilazimishe kwenda taratibu na kupumzika. Katisha mihadi na shughuli ulizokuwa unazifanya. Jipe muda wa kupumzika.
- Pata msaada: Mshirikishe Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea, hasa wakati wa usimamizi na wenzako na jadili changamoto za kazi, kwa hiyo shiriki mikutano yote na kumbuka unafanyakazi katika timu.
- Pima tena malengo yako na vipaumbele: Angalia kama unakuwa na muda wa kutosha wa kukaa na familia yako na pia muda wa kufanya kazi.
- Shirikisha wenzako unaowaamini juu ya masuala yanayokutatiza au mawazo yako juu ya kuboresha hali yako.
- Kubali kusaidiwa: Usione aibu kusaidiwa na wengine hata kama ni kazi nyepesi kwenye shauri.

Michoro Inayoonyesha Makuzi ya Utotoni




Mawasiliano
anatoa sauti
na ishara
anageuza kichwa kuangalia
sauti ilipotoka
Kiakili
anaweka
vitu
mdomoni
anacheza na
midoli
anavutiwa na
vitu tofauti
tofauti
Miezi
6
anaogopa
watu
wageni
anatambaa kwa tumbo
anakaa kwa
kushika badhi
ya vitu
anatambua
baadhi
ya sura
anarusha miguu
na mikono
Kijamii
Kimwili


Mawasiliano
Kiakili
Baba.
Baba.
Mpatie.
Anaanza kusema neno moja moja au ishara
anaelewa lugha nyepesi na ishara
ba-ba ga-ga
ananza kuigiza sauti za vitu mbalimbali na vitendo
anafahamu uwepo wa kitu hatakama hakioni
anaweza kutatua changamot o rahisi
anaanza kuelewa sababu na matokeo
Miezi 12
anatumia lugha ya ishara
analia anapoachwa na mlezi
anaanza kucheza miano. kupiga makofi
anakaa bila kusaidiwa
anatambaa
anasimama kwa kutegemea vitu
Kijamii
Kimwili


Mawasiliano
Kiakili
Kijamii
Kimwili
Miaka 2
anacheza mpira
Anafaha maneno 5 hadi 20 au ishara
anatumia sentensi zenye maneno 2 na 3 au ishara
Kukomba
anatumia maneno rahisi na ishara
anawezakulinganisha vitu
anaweza kutumia vitu vinavyohusiana
anatumia mwingi k shughuli
anamuiga miezi
anacheza na watoto wenzake
anaweza kuomba msaada anabohifajj
anaweza kupanga vitu
anatembea
anaweza kuchuchuma a


Mawasiliano
Kiakili
Miaka 3
Kijamii
Kimwili
Biskuti yako iko wapi?
anaelewa lugha nyingi rahisi
anaweza kutumia maneno kati ya 500
anaweza kuweka vitu mahali husika kulingana na maumbo
nga vitu
kukusanya vitu na kuviweka pamoja
nataka kwenda na baba
anawasiliana vizuri
anafurahia kusaidia kazi za nyumbni
Asante kwa kunisaidia
kupenda kusifiwa anapofanya jambo zuri
kuambua hisia za watu
kuruka, kukimbia, kupanda
kutumia mikono kufanya kazi ngumu zaidi



Utoto wa kati miaka 6-11: Umri wa kwenda shule ya msingi unatambulika kwa uwezo wa mtoto katika michezo, mchakato wa kufikiri wenye mantiki; stadi za msingi katika kusoma; kujitambua, maadili na urafiki; na ushiriki katika makundi rika.

Hatua za Ukuaji bora Kwa Kijana Balehe

Hatua	Mawasiliano	Akili	Kijamii	Kimwili
Balehe ya awali, miaka 10-14	Huzingatia wakati uliopo, "Hapo hapo" Hakuna uhakika wa kuelewa kama nikifanya jambo hili kutatokea nini au kuelewa chanzo na matokeo Chini ya msongo, mara nyingi huwa na jazba kuliko kuwa na uwezo wenye mantiki. Ni imara katika kutambua nafsi kuliko jamii.	Huuliza nafsi Mimi ni wa kawaida? Ndoto za mara kwa mara za mchana Hawana uhakika na wanachokitaka kiweledi; malengo hubadilika mara kwa mara Huanza kujitengenezea mfumo wa thamani Hisia za ngono zinaaza na kuchunguza masuala ya ngono Hadhira ya kufikirika Kuhitaji faragha Kuyakuza matatizo yake "Hakuna anayenielewa"	Kupingana na mamlaka, familia; Kuwa kinyume na wazazi, (ingawa hatua hii ni muhimu katika sehemu ya makuzi ya mtoto, lakini inaweza kuwa ngumu kwa wazazi kuelewa) Upweke Mabadiliko makubwa kihisia Wanaweza kuvikataa vitu vinavyo wakumbusha utoto Wabishi na siyo watiifu Wanakuwa na urafiki mkubwa na wenzao wa jinsi moja Wanakutana na watoto wa jinsi tofauti wakiwa katika makundi	Ubalehe. Wanakua haraka. Mtindo wa kulala hubadilika (kukaa sana na kuchelewa kulala). Kukua haraka kunahitaji masaa ya kulala 9 au zaidi kwa siku. Viungo vya uzazi vinakua
Umri wa kati wa kubalehe, miaka 15-17	Mgongano na familia unatawala; Kijana anakuwa na wasiwasi wa kuwa mtu mzima anyejitawala	Kuwa na Uwezo zaidi wakufikiria nadharia na matokeo yake Uelewa vizuri zaidi chanzo cha jambo na matokeo yake Anatawaliwa na kuzama katika nafsi	Muungwana kwa wana rika na mara nyingi huambizana wanachokipenda na wasichokipenda Hisia za ngono na kuanza kuchunguza uwezo wa kutongoza na kumvutia mwenza Kujaribu ngono, dawa za kulevya, marafiki, kazi tofauti, tabia hatarishi	Tabia za kingono karibia zote zimekamilika 95% ya urefu wa utu uzima imefikiwa

Aina ya Malezi

Aina ya Malezi	Maelezo	Matokeo
Ukali/udhibiti	Katika aina hii ya malezi watoto wanatarajiwa kufuata taratibu zilizowekwa na wazazi. Wakishindwa kufuata huo utaratibu wanaadhibiwa. Wazazi wenye malezi ya namna hii wanategemea watoto wao wafanye mambo makubwa lakini wao hawatekelezi wajibu wao kwa watoto. Wazazi haya ni watiifu na wanapenda hadhi yao, wanategemea maelekezo yao yafuatwe bila maelezo.	Aina hii ya malezi ya ukali/ udhibiti kwa ujumla huwafanya watoto kuwa watiifu na wenye uwezo lakini wanakuwa na kiwango kidogo cha furaha, kushirikiana na jamii na kujithamini.
Miongozo	Kama ilivyo kwa malezi yenye ukali/udhibiti, wanaotumia aina ya malezi ya mwongozo wameweka taratibu na miongozo ili watoto waifuate. Wanatekeleza wajibu wao kwa watoto na wapo tayari kuwasikiliza maswali yao, njia zao za kutoa adhabu ni za kujenga kuliko kuumiza. Wanahitaji watoto wao wajiamini na kuwajibika kijamii, waweze kujiongoza na wenye ushirikiano.	Aina ya malezi yenye miongozo huwafanya watoto kuwa wenye furaha, uwezo na mafanikio.
Kuruhusu	Wazazi wenye malezi ya kuruhusu wakati mwingine wanaitwa wazazi wapole, hawatarajii mambo mengi kutoka kwa watoto wao. Wazazi hawa hawatoi adhabu kwa watoto wao kwa sababu hawatarajii watoto wao wawe wakomavu na wanaojiongoza wenyewe. Wanawajibika kwa watoto wao zaidi kuliko kutegemea uwajibikaji wa watoto. Wazazi wenye malezi ya kuruhusu kwa ujumla wanawezeshwa na kuwasiliana na watoto wenzao, mara nyingi upande wa rafiki unatawala zaidi ya mzazi.	Malezi yenye kuruhusu mara nyingi huwafanya watoto kuwa na kiwango kidogo cha furaha na kujiongoza. Mara nyingi watoto hawa wana uwezekana wa kukinzana na mamlaka na hafanyi vizuri katika masomo shuleni.
Kutojali	Aina ya malezi ya kutojali huambatana na uwajibikaji mdogo wa wazazi kwa watoto na mawasiliano kidogo. Pamoja na kuwa wazazi hutimiza huduma kwa mahitaji ya watoto, kwa ujumla hawajihusishi na maisha ya mtoto. Wakati wmingine wazazi wanaweza kutaa au kupuuza kukidhi mahitaji ya watoto.	Malezi ya kutojali yanapelekea viwango vya chini katika Nyanja zote za maisha. Watoto wanshindwa kujitawala, kiwango cha chini cha kujithamini na uwezo mdogo katika kufanya mambo ukilinganisha na wanarika wenzao.

Aina za Ukatili Dhidi ya Watoto

Ukatili dhidi ya watoto unahusisha tabia na vitendo vya makusudi vya kutumia nguvu vya kuumiza, kuharibu au hata kuua mtu.

Aina za ukatili zinazohusiana na kazi yako kama Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea au Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni pamoja na:

- Unyanyasaji wa kihisia: Hii ni pamoja na kuitwa jina baya, kufanya mtu ajisikie hatakiwi au kitisho cha kuachwa pweke
- Ukatili wa kimwili: Ukatili wa kimwili kama kupigwa makofi, ngumi, kusukumwa, kupigwa mateke, kutiwa singi au kutishiwa kwa silaha kama buduki na kisu
- Ukatili wa kingono: Matendo yote ya kingono amabyo ni kinyume na matakwa ya mtu yakihusisha matendo ambayo ni kinyume na sheria ikiwemo ngono ya kulazimisha (ubakaji), kujaribu kubaka, kupapasa, vitisho vya kingono, kuonyesha picha za ngono na matusi
- Kutelekezwa: Huu ni wakati ambao mzazi/mlezi amemtelekeza mtoto na hana mawasiliano naye na hivyo hatoi huduma kwa mahitaji ya mtoto

Maelezo Kuhusu Huduma ya Simu kwa Mtoto - Namba 116

Huduma ya Simu kwa Mtoto – 116 ni nini?

- Namba 116 ipo kwa ajili ya huduma kwa mtoto ikiwa ni pamoja na kulinda, kuzuia na kuelimisha juu ya ukatili dhidi ya mtoto.
- Namba 116 ilianzishwa ili kupokea taarifa za ukatili/unyanyasaji wa watoto. Namba 116 hutoa ushauri nasaha na muongozo kwa watoto, wazazi, walezi na wanajamii wanaopiga simu. Namba 116 pia husaidia kuwapa wazazi elimu na ushauri ya njia sahihi za kumuongoza mtoto katika ukuaji na maendeleo yake. Vilevile kupitia huduma hii wanajamii hufahamishwa na kuunganishwa na huduma za watoto zitolewazo na halmashauri zote nchini.

Nani apige simu ya 116 – Huduma kwa Mtoto?

Watoto na watu wazima nchini kote wanaweza kupiga 116 bila malipo na kutoa taarifa pale haki za watoto zinapokiukwa.

Kupitia 116 Watoto Wanaweza:

- Kupiga simu namba 116 bila malipo na kutoa taarifa za vitendo vya kikatili anavyotendewa yeye au rafiki yake.
- Kuongea kwa uhuru kuhusu maisha yao ya kila siku na vikwazo wanavyokumbana navyo kama watoto.
- Kupata Ushauri nasaha kutoka kwa wataalamu waliopata mafunzo maalum ya maswala mbali mbali.
- Kupewa muongozo juu ya mambo ambayo hawawezi kuongea na familia zao au marafaiki kwa sababu mbalimbali ikiwemo uoga.
- Kufahamu na kutimiza wajibu wao kama watoto.

Kwanini upige 116?
Kutoa taarifa juu ya:

- Ukatili wa kimwili kwa mtoto
- Ubakaji/ Ukatili wa kingono kwa mtoto
- Ukatili wa kisaikolojia/ kihisia kwa mtoto
- Utekelezwaji wa watoto
- Migongano ya kifamilia ambayo humuathiri mtoto kwa namna moja au nyingine
- Vitendo vya kimila kama vile ukeketaji ambao hukiuka haki ya mtoto
- Kunyimwa haki ya kusoma na mengine mengi.

Ukipiga simu nini hufanyika?
Huduma ya simu kwa mtoto inahamasisha watoto (na wanajamii) kupiga simu namba 116 ambapo wataongea na wataalam washauri wanaowaamini na kuwapenda watoto na wako tayari kuwasikiliza, kuwahudumia na kuwashauri.

Baada ya kusikiliza tatizo lako, mshauri atakusaidia kwa kukupa ushauri, kutoa taarifa hizo kwa vyombo husika ikiwemo Ustawi wa Jamii, Polisi: Dawati la Jinsia na Watoto, Mashirika yanayojihusisha na ulinzi wa mtoto na kufuatilia ili kujua ni hatua gani zimechukuliwa.

VIAMBATANISHO KWA AJILI YA REJEA

Kitini cha 1: Maelezo ya Msingi Kuhusu Haki za Watoto

Tafsiri ya **"Mtoto":** Mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18. [Mkataba wa Kimataifa wa haki za Watoto (UNCRC); Sheria ya mtoto ya Tanzanaia, (2009)].

MUHTASARI WA SHERIA NA SERA

Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Kimataifa kuhusu haki za watoto na kanuni zake za hiari na kuingiza mkataba huu katika Sheria ya Mtoto ya Tanzania ya mwaka 2009, ambayo imeunganishwa na maagano na mikataba ya Kimataifa.

Sheria ya Mtoto ya Tanzania ya mwaka 2009, sehem ya (1) inasema kwamba maslahi mapana ya mtoto ndiyo msingi wa kuzingatia katika suala lolote linahusu mtoto.

Haki za watoto ni haki za binadamu za watoto zinazokazia hasa haki ya ulinzi maalum na malezi yanayowezekana kwa watoto.

Haki za watoto ni pamoja na:

1. Haki ya kuishi: kila mtoto ana haki ya kuishi na kuendelezwa (UNCRC kifungu na. 6 & 24 na Sheria ya Mtoto ya Tanzania 2009 kifungu na. 9).
2. Mahitaji ya msingi ya kulindwa, chakula, elimu, huduma za afya na kuendelezwa (UNCRC kifungu na. 24 & 29 na Sheria ya Mtoto ya Tanzania (2009), kifungu na. 8).
3. Haki ya ulinzi: [mamlaka ya serikali za mtaa zina jukumu la kulinda na kuendeleza ustawi wa mtoto katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na ulinzi wa raia (Sheria ya Mtoto ya Tanzania (2009) kipengele III, VIII & IX].

4. Haki ya kulindwa na unyonyaji kiuchumi (CRC kifungu na. 32).
5. Haki ya kushiriki katika maamuzi yanayoathiri ustawi wake (UNCRC kifungu na. 12).
6. Haki ya kuishi na wazazi wake: "mtoto asitenganishwe na wazazi wake bila idhini yake au wazazi wake isipokua inapobidi kwa ajili ya maslahi ya mtoto" [UNCRC kifungu na. 9 & Sheria ya Mtoto ya Tanzania (2009) kipengele na. 7 (1-2)].
7. Haki ya kuwa huru dhidi ya ubaguzi wa rangi, jinsia, mwelekeo wa kingono, ulemavu, utaifa, dini, kabila na sifa nyinginezo [Sheria ya Mtoto ya Tanzania (2009) kipengele na. 5].

Agizo la 5 linalotekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 inaelekeza bodi za uma kuhakikisha kwamba elimu ya sekondari inatolewa bure kwa watoto wote. Hii ni pamoja na kufuta aina zote za ada na michango.

Kitini cha 2: Maana ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania Kutokana na Mpango wa Taifa wa Pili wa Kuhudumia Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (2013-2017)

Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (WWKMH): "Ni watoto walio chini ya umri wa miaka 18 waliokosa mahitaji ya msingi kabisa hali inayowafanya wawe kwenye mazingira yanayohatarisha afya zao, ustawi na maendeleo yao kwa muda mrefuna hatari yakukosa mahitaji yao."

Sifa za watoto walio katika mazingira hatarishi:

Kwa kuzingatia tafsiri ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi, zifuatazo ni sifa za WWKMH:

a. Ni yatima au ametelekezwa na ndugu zake;
b. Ametelekezwa au ametendewa visivyo na mtu anayemlea na kumtunza au na mlezi wake au wazazi;
c. Ana mzazi au mlezi asiyetoa malezi sahihi;
d. Ni maskini;
e. Analelewa na mzazi au mlezi ambaye kutokana na tabia za kihalifu au ulevi, hawezi kumlea mtoto;
f. Ni mzururaji na hana makazi au sehemu ya kuishi;
g. Ni ombaomba au anaishi kwa kutegemea misaada, ama kwa kisingizio cha kuimba, kucheza, kufanya maonyesho, kuuza kitu chochote au vinginevyo, au anakutwa katika mtaa wowote, jengo, au mahali pengine kwa madhumuni ya kuomba au kupata misaada;
h. Anaambatana na mtu yeyote ambaye anaomba au anayeishi kwa kisingizio cha kuimba kucheza kufanya maonyesho au kuuza kitu chochote au vinginevyo;
   (i) Analelewa na mzazi asiye na uwezo au mzazi fukara;
i. Mara kwa mara anaambatana na mhalifu sugu au kahaba;
j. Anaishi kwenye nyumba au sehemu ya nyumba inayotumiwa na makahaba kwa lengo la kufanya ukahaba au vinginevyo anaishi katika mazingira yanayosababisha, au kuvutia au kuhamasisha ukahaba au kuathiri maadili ya mtoto;
k. Ni mtu ambaye kupitia kwake kosa limetendwa au jaribio la kosa chini ya Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu jaribio limefanywa;
l. Amekuwa akifanya jambo ambalo kwa namna ambayo inaaminika kuwa anashawishi au amekuwa akishawishi kufanya mambo yaliyo kinyume na maadili;
m. Yuko chini ya umri unaomfanya awajibike kijinai na amehusika kutenda kosa kubwa la jinai;
n. Kwa namna nyingine, yupo katika mazingira yanayomhatarisha kimaandili au kimwili;
o. Analelewa na mtu mwenye ulemavu ambaye ulemavu huo unamfanya asiweze kumpa mtoto malezi stahili;
p. Endapo mtoto huyo yupo katika mazingira mengine yoyotkama ambavyo Kamishna ataamua.

Kitini cha 3: Maelezo ya Msingi Kuhusu Ulinzi wa Mtoto

Ulinzi wa Mtoto

Ulinzi wa mtoto unahusu "njia rasmi na zisizo rasmi za kuzuia na kushughulikia unyanyasaji, ukatili, kutelekezwa na kunyonywa kwa watoto". Baadhi ya aina za ukatili kwa watoto ni kama ifuatavyo:

- Ukatili wa kimwili unaojumuisha kusukumwa, kufinywa, kupigwa kofi au kubamizwa;
- Ukatili wa kihisia unajumuisha kutukanwa, kuitwa majina mabaya, inamfanya mtoto ajisikie vibaya;
- Kutelekezwa.

Kushindwa kumpatia mtoto mahitaji ya msingi kwa maksudi na kwa muda wote; mahitaji ya kimwili/au kisaikolojia, kama vile kushindwa kwa makusudi kumpa chakula cha kutosha, nguo na malazi:

- Usafirishaji haramu wa mtoto: Utafutaji, usafirishaji na unyonyaji kwa ajiri ya kuwatumikisha/kazi ndani au kuwafanyisha ngono. Wasafirishaji haramu hutoa ahadi za uongo na kuwarubuni kwa fursa ya kujipatia kipato binafsi;
- Ukeketaji wa wanawake: Uondoaji kidogo au wote wa maeneo ya nje na ndani ya uke bila sababu zozote za msingi;
- Ukatili na unyonywaji wa kingono kumlazimisha mtoto kujishughulisha na ngono aidha au bila kukutana kimwili. Unyanyasaji wowote au jaribio la unyanyasaji kwa dhumuni la kingono kutokana na hadhi au kuaminiwa bila kusahau unyonyaji kingono wa mwingine kwa lengo la kibiashara, kijamii na kisiasa.

Aina ya Huduma za Ulinzi wa na Usalama wa Mtoto

Aina kuu za huduma za ulinzi wa mtoto ni pamoja na kuhakikisha watoto wana vyeti vya kuzaliwa, msaada wa kisaikolojia na kisheria wanaohitaji, unasihi, rufaa na kuunganishwa na huduma nyingine za ulinzi wa mtoto.

Kwa watoto walio nje ya malezi ya familia (mfano: watoto na vijana balehe walio mitaani) pia ni pamoja na huduma ya kuunganishwa na familia, na/au malezi yakambo na kuasili, mradi wamarekebisho katika maeneo salama, na malazi ya muda.

Afua zingine za ulinzi ni pamoja na kufanya kampeni dhidi ya ukeketaji wa wanawake na mila zingine hatarishi, uhamasishaji wa jamii dhidi ya ndoa za utotoni na kuzuia ukatili.

Kitini cha 4: Ushirikiano wa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii na Mifumo Mingine

Nani anawasaidia WWKMH katika ngazi ya jamii?

Katika ngazi ya kijiji/mtaa, zipo kamati ziitwazo Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto (ambazo zinasaidia kazi ya Afisa Ustawi na Msimamizi wa mashauri ya huduma).

Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto Ngazi ya Jamii zinawajumbe wafuatao:

i. Tabibu/Mtaalam wa afya;
ii. Mkunga wa Jadi;

iii. Msaidizi wa Kisheria;
iv. Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii wa kujitolea;
v. Mtaalam wa Usafi na Mazingira;
vi. Walimu wanasihi (Msingi na Sekondari);
vii. Polisi jamii;
viii. Viongozi wa dini;
ix. Maafisa Ugani;
x. Wawakilishi wa AZAKI;
xi. Wawakilishi wa Vikundi vya Vijana;
xii. Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;
xiii. Wawakilishi wawili watakaoteuliwa kutoka vikundi vya maendeleo ya wanawake;
xiv. Wawakilishi wawili wa Watoto (Mvulana na Msichana); na
xv. Watu mashuhuri mwanamke na mwanamme.

Wasimamizi wa Mashauri ya watoto watafanya kazi kwa karibu na Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya jamii. Mwongozo wa kitaifa kuhusu mafunzo ya usimamizi jumuishi wa Mashauri ya watoto kwa Wasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii, unaeleza kuwa kada za ngazi ya jamii zinazofanya kazi na WWKMH zimejumuishwa katika kamati. Hao ni pamoja na Wasimamizi wa Afya Ngazi ya Jamii, waratibu wa huduma za matunzo nyumbaniambao pia wanaweza kupewa mafunzo kama Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii.

Kitini cha 5: Hatua za Mzunguko wa Usimamizi wa Huduma za Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Mzunguko wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

- Ni mchakato wa kiutaratibu, uliopangiliwa wa kufanya utambuzi, tathmini, kupanga, kutoa msaada, rufaa na ufuatiliaji wa Mashauri ya Watoto.
- Ni mchakato wa hatua kwa hatua ambao Wasimamizi wa Mashauri hutumia kushughulikia mashauri katika njia ya aina moja, hata hivyo inampa nafasi Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii kushughulikia mashauri kibinafsi, kifamilia na kwa kutegemea suala lilivyo.
- Unatoa mwongozo kwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ngazi ya jamii kushughulikia mashauri katika hali inayofaa.
- Unahitaji utunzaji wa kumbukumbu mzuri, ufuatiliaji wa mashauri ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa muda muafaka na kufikia malengo mahususi.

Sifa kuu za Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

- Unazingatia watoto binafsi na familia.
- Unaratibu huduma kwa kuunganisha/katika mfumo wa rufaa.
- Uwajibishaji wa mchakato wa Mashauri ya Watoto katika mifumo rasmi na miundo. Kwa madhumuni ya uwajibikaji, msimamizi mmoja wa mashauri anajukumu kwenye kila shauri.
- Ukomo wa muda na unasisitiza kwamba, Usimamizi wa Mashauri ya Watoto utaendelea kutoewa mpaka pale ambapo mahitaji na malengo mahsusi yametimia.

Mzunguko wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto

Mzunguko wa hatua za usimamizi wa mashauri	Tafsiri/hatua muhimu/Maamuzi maalum	Fomu za Kitaifa	Vitendea kazi vya Kitaifa	Nini kinafanyika katika hatua hii
Hatua ya I: Usahili	**Usaili**: Hatua hii inaanzia pale mtu anapoona au kuhisi uwezekano wa kuwepo kwa hitaji la kiulinzi, afya au Ustawi wa mtoto na hivyo kutoa taarifa kwa Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii au Mjumbe wa kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto, au kiongozi wa mtaa, au jirani au mwana jamii yeyote anayehusika Hatua hii ni ya awali katika hatua za kukabiliana na tatizo. **Hii ni hatua ya msingi katika kufanya maamuzi kama Msimamizi wa Mashauri Ngazi ya Jamii atoe rufaa kwa mtoto kwenda kwa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto, au afungue shauri, au awasiliane na Afisa Ustawi Wa Jamii.**	Fomu ya Kitaifa ya Usajili wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na Kaya	Kitendea kazi cha kutambua kiwango cha uhatarishi wa ukatili	Msimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii anapopokea shauri kuna hatua 3 za kuchukua: 1. Ataamua kama anaweza kutataua tatizo mara moja bila kufungua shauri. Baada ya kutatua tatizo anajaza fomu ya usajili wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na Kaya lakini hafungui shauri. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anaweza kumpa mtoto rufaa kwenda kwenye Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto kwa msaada zaidi. 2. Wasimamizi wa Mashauri ya watoto ngazi ya jamii wanaamua kufungua shauri ili kuweza kutatua shauri la mtoto. Wanajaza fomu ya usajili wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi na kisha kuendelea na **hatua ya** pili ya tathmini ya mahitaji na uwezo wa mtoto na familia. 3. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anapotambua kwamba shauri ni la kiulinzi. Awasiliane na Afisa Ustawi wa Jamii na kama ikibidi polisi wa dawati la jinsia na watoto. Afisa Ustawi wa Jamii atafungua shauri na kulisajili katika Mfumo wa Kitaifa wa ulinzi na usalama wa mtoto. Shauri la kiulinzi linashughulikiwa na Afisa Ustawi wa Jamii. Hata hivyo anaweza kuwasiliana na Msimamizi wa Mashauri ngazi ya Jamii kama atahitaji msaada wake.

Hatua ya 2: Tathmini	"**Tathmini ya mahitaji na Uwezo"** Ni namna ambayo Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anapata kufahamu zaidi kuhusu hali ya mtoto na familia yake ili waweze kuandaa mpango wa huduma. Tathmini hii inaangalia uwezo/rasilimali za mtoto na kaya pamoja na mahitaji yao. **Swali la Msingi: Nini uwezo na rasilimali alizonazo mtoto na familia yake? Kuna changamoto zipi?**	Fomu ya tathmini ya Mahitaji ya mtoto na mpango wa huduma	Kitendea kazi cha tathmini ya mahitaji na uwezo wa mtoto	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anapata kujua zaidi kuhusu hali ya mtoto na familia yake. Hii ni pamoja na kuongea na mtoto na mlezi ana kwa ana pamoja na watu wengine wanaohusiana na hiyo familia.
Hatua ya 3: Kuandaa mpango wa huduma	Unaolezea huduma na rufaa ambazo mtoto na familia yake watapatiwa. **Swali la Msingi: Ni huduma gani mtoto na familia wanahitaji? Hizo huduma zinapatikana wapi? Ni kwa namna gani mtoto na familia wanaweza kufikia huduma hizo?**	Fomu ya Tathmini ya Mahitaji ya Mtoto na Mpango wa Huduma	Kitendea kazi cha tathmini ya mahitaji na uwezo wa mtoto Fomu ya Maelekezo ya Huduma Zinapopatikana	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anaandaa Mpango wa huduma. Baada ya Kuandaa mpango wa huduma, anapaswa kuongea na mtoto na familia yake ili kuhakikisha kwamba ana taarifa sahihi kuhusu nini kinapaswa kutokea baada kumaliza kuandaa mpango wa huduma.

Hatua ya 4: Kutekeleza mpango wa huduma	**Msimamizi wa mashauri ya watoto anatekeleza mpango wa huduma**. Rufaa zinatekelezwa kwa ushirikiano kati ya watoa huduma mbalimbali katika jamii na wasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii. **Vitu vya msingi vya kufanya: Mtembelee mtoto na familia mara kwa mara kuwasaidia kuweza kufikia huduma.**	Fomu ya Kufuatilia Utoaji wa Huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kwa Mwezi	Fomu ya Maelekezo ya Huduma Zinapopatikana	Wakati wa utekelezaji wa mpango wa huduma, Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anajitahidi kuhakikisha kwamba mtoto na familia wanapata huduma zote kama zilivyoainishwa katika mpango wa huduma. Utekelazi wa mpango wa huduma unahusisha huduma zinazoweza kutolewa moja kwa moja na Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii kama vile kuwatembelea watoto nyumbani, msaada wa kijamii na kisaikolojia, pamoja na huduma za rufaa kwenda kwa watoa huduma wengine kama vituo vya afya, vikundi vya kuweka na kukopa, vikundi vya stadi za malezi n.k Wasimamizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii wanatumia fomu ya maelekezo ya huduma zinapopatikana kutoa huduma ya rufaa. Fomu ni muhimu kufanyiwa mapitio mara kwa mara kama kuna maadiliko yoyote ili Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii waweze kutoa taarifa sahihi za huduma zilizopo kwa mtoto na familia. Wakati wa utekelezji wa mpango wa huduma, Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii anaendelea kumtembelea mtoto na familia. Kulingana na tatizo la mtoto anaweza kumtembelea mara chache kwa wiki au mara chache kwa mwezi. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ataandika katika fomu ya kufuatilia huduma zinazotolewa kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kwa mwezi kila anapotembelea kaya.

Hatua ya 5: Ufuatiliaji na mapitio ya mpango wa huduma	**Ufuatiliaji na mapitio ya mpango wa huduma** ni pamoja na kupitia kila mara mpango wa huduma kwa mtoto kupitia vikao vya mwezi vya kupitia mashauri. **Maamuzi ya Msingi: Je, hali ya mtoto na familia yake imekua bora?**	Fomu ya Mwezi ya Taarifa ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi	Kikao cha kupitia Mashauri ya Watoto	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii na wasimamizi viongozi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii wanakutana kujadili na kupitia mashauri yao. Wanasaidiana kuona kama wanahitaji kurekebisha mipango ya huduma za watoto waliowahudumia.
Hatua ya 6: Kufunga Shauri	Ni pale ambapo baada ya mapitio ya mpango wa huduma inaonekana kwamba masuala yote yanayohusu ustawi wa mtoto yameshafanyiwa kazi au shauri limehamishiwa eneo jingine au mtoto amefariki. **Maamuzi ya Msingi: Je lengo la mpango wa huduma limefikiwa?**	Fomu ya Kitaifa ya Kufunga Shauri	Kikao cha kupitia mashauri ya watoto	Wakati wa Kikao cha kupitia mashauri, kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii na Msimamizi Kiongozi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii wameridhika kwamba mahitaji ya mtoto na familia yametekelezwa basi shauri linaweza kufungwa.

1. **Utambuzi:** Mchakato wa utambuzi wa watoto na walezi wao wanaohitaji huduma ya usimamizi wa mashauri. Kufanya kazi na watoa huduma wengine na mifumo ya kijamii kuwatambua Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi au wapo katika hatari ya kupata madhara.

2. **Usahili:** Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wanaamua kama faili la shauri la mtoto lifunguliwe kwa niaba ya mtoto. Kama shauri la mtoto likifunguliwa, anaendelea na mchakato uliobakia wa usimamizi wa mahauri ya huduma.

3. **Tathmini kaya na hali ya mtoto:**

    - Kupata undani wa uwezo na mahitaji ya kaya.
    - Kupata undani masuala ya mtoto.
    - Kujua kama kuna hitaji la haraka au madhara kwenye maisha. Kama ni ndiyo, hatua huchukuliwa ndani ya masaa 24, na siyo baada ya masaa 48.
    - Hali ya mtoto inaweza kubadilika, kwa hiyo tathmini inahitajika kufanyika kila baada ya muda mrefu (yaani kila mwaka).
    - Tathmini ijumuishe kujua visababishi vya hatari na vizuizi vya hatari kwa mtoto.

4. **Kutengeneza mpango wa huduma:**

   - Tumia matokea ya tathmini kutengeneza mpango.
   - Wahusishe watoto na familia kutengeneza mpango.
   - Mpango wa huduma lazima uwe na malengo ya kufikika na yahusiane na ustawi wa mtoto.
   - Kwa ujumla rasilimali ni chache, kwa hiyo Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto lazima wafanya kazi na familia na jamii ili kujua rasilimali zilizopo.
   - Mpango uanishe:
     - Nini kitokee (kushughulikia mahitaji yaliyotambuliwa ya haraka, ya muda mfupi, ya kati na ya muda mrefu)
     - Nani afanyie kazi
     - Mpaka lini shughuli ziwe zimeisha.

5. **Kutekeleza mpango wa huduma** (Inaweza kuhusisha moja au yote yafuatayo):

   - **Kutoa huduma za moja kwa moja**: Kama vile taarifa na ushauri, kutoa msaada wa kisaikolojia, kufanya utetezi na/au kushawishi kwa niaba ya mtoto.
   - **Rufaa na ufuatiliaji:** Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto kuhakikisha kwamba watoa huduma wengine wanasaidia kushughulikia mpango wa huduma wa mtoto na kuchunguza kila baada ya muda kama shughuli zimefanyiwa kazi au huduma zimetolewa.

6. **Fuatilia na Tathmini kama:**

   - Shauri la mtoto linafanyiwa kazi kama lilivyo katika mpango wa huduma.
   - Mpango wa huduma unatakiwa kubadilika.
   - Fanya ufuatiliaji kwa vipindi kimkakati; hasa, Mpango wa huduma unatakiwa upitiwe kila baada ya miezi mitatu.

7. **Hitimisho la shauri la mtoto/Kuagana:**

   - Vigezo vya lini shauri la mtoto linaweza kuhitimishwa viwekwe pamoja na wahusika washaurine vihusiane na ustawi wa mtoto. Kwa mfano, kigezo kinaweza kuwekwa katika maeneo ya uimarishaji uchumi wa kaya na uhakika wa chakula, huduma ya afya, elimu ya mtoto, lishe na hali ya afya.
   - Mashauri ya watoto yaliyohitimishwa yatuzwe katika sehemu salama kwa kipindi maalum uliwekwa.

Kitini cha 6: Maelezo ya Msingi Kuhusu Mfumo wa Kitaifa juu ya Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto

Serikali ya Tanzania imedhamiria kuboresha na kulinda ustawi wa watoto wote Tanzania na kupunguza athari hasi zinazotokana na VVU, umasikini, vifo, ulemavu, utelekezaji wa watoto, ndoa za utotoni, na ukatili dhidi ya watoto. Mpango wa II wa Taifa wa kuhudumia Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi unakusudia kuboresha ustawi na ulinzi wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kwa kulinda haki zao na kuzuia/ na/au kupunguzo vitendo hatarishi na athari za matatizo. Mpango wa Utekelezaji wa Taifa wa kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto una Dira ya kuwa na Tanzania ambayo wanawake na watoto wako huru dhidi ya vitendo vya Ukatili. Mpango wa Afya ya Jamii, utaongeza idadi ya Wasimamizi wa Afya Ngazi ya Jamii na kuchangia moja kwa moja lengo la **90 - 90 - 90** (90% watu kujua hali zao, 90% kuingizwa katika matumizi ya Dawa za Kufubaza VVU, na 90% wapunguze kiwango cha VVU) na utasaidia Tanzania kufikia **hatua ya** kizazi kilicho huru dhidi ya UKIMWI. Sera hizi tatu za Taifa ni muhimu katika kuhakikisha kwamba WWKMH na wahanga wa ukatili wanapata huduma muhimu na msaada. Hata hivyo, kumekuwa na uwekezaji mdogo katika uratibu wa watoa huduma na mifumo ambayo hufanya kazi chini ya sera hizi tatu muhimu za taifa, Kukosekana kwa uratibu huu, kumepelekea kukosekana kwa mpango mzuri, mitandao hafifu ya rufaa, na ustawi wa jamii, ulinzi, na manufaa ya huduma ya VVU kwa watoto.

Ili kushughulikia masuala haya, Shirika la misaada la Marekani (USAID) kupitia Mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na maambukizo ya VVU (PEPFAR) limefadhiri Mpango wa "CHSS" (au Kuimarisha Mifumo ya Afya na Ustawi wa Jamii) ili kuisadia kuboresha uratibu na usimamizi wa utoaji huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi. Katika utekelezaji wa mpango huo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na OR – TAMISEMI zimewezeshwa kutengeneza Mfumo wa Kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya watoto ambao utaimarisha uratibu kwa kuunganisha watoa huduma za Ustawi wa Jamii, Ulinzi, na huduma zinazohusiana na VVU katika ngazi ya jamii. Mfumo wa Kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto unatumia mbinu ya Usimamizi wa Mashauri ya Watoto kuwaunganisha watoa huduma wote wanaofanya kazi na watoto katika nyanja mbalimbali za VVU/afya, ulinzi na Ustawi wa Jamii. Kitu muhimu katika Mfumo wa Kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto ni "kushughulikia Mashauri ya Watoto kulingana na aina ya tatizo na kipaumbele" ambapo Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto waliopata mafunzo watahakikisha kwamba mashauri ya dharura yanashughulikiwa haraka na mashauri yote ya kitaasisi yatapewa rufaa kwenda kwa Mtaalam wa ustawi. Rufaa za kuelekea sehemu mbambali na Mikutano ya kijamii kuhusu Mashauri ya kawaida kati ya watoa huduma ngazi ya jamii na watoa huduma kwenye vituo vya afya ni msingi wa Mfumo wa Kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto na utauboresha mfumo wa sasa na kuhamasisha ushirikiano kati ya wataalam wa VVU/afya, Ulinzi na Ustawi wa Jamii na kada za wanajamii wanaojitolea.

Kwa kuwaunganisha watoa huduma kutoka kwenye hizi nyanja tatu muhimu na kutafsiri majukumu yao na wajibu katika kufanya ufuatiliaji wa rufaa kupitia usimamizi wa Mashauri ya Watoto, mfumo wa kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto utaboresha ufanisi wa utoaji huduma katika ngazi ya serikali za mitaa na kupunguza mzigo wa Mashauri ya Watoto kwa wataalam wa ustawi wa jamii. Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni nguvu kazi muhimu katika Mfumo wa Kitaifa kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto, ambao watashughulikia Mashauri ya Watoto Katika Ngazi ya Jamii na kutumia usimamizi wa Mashauri ya Watoto na rufaa kuunganisha masuala ya VVU/afya, Ulinzi na kada ya ustawi wa Jamii na mifumo ya kijamii.

Kitini cha 7: Uratibu wa Mfumo wa Kitaifa Juu ya Usimamizi Jumuishi wa Mashauri ya Watoto Ya Watoto



Kitini cha 8: Mfumo wa Rufaa na Kuunganisha Huduma



Mchoro huo hapo juu unaonyesha jinsi gani Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anaweza kufanya kazi na mifumo na miundo iliyopo ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa WWKMH na Familia zao.

Mfano wa 1: Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anapokea shauri la mtoto kutoka kwa mjumbe wa Kamati ya Ulinzi wa wanawake na watoto kuhusu mtoto aliyenyanyaswa kingono. Halafu, Msimamizi wa Mashauri ya Watoto ametoa rufaa kwenye kituo cha afya au polisi na kumjulisha Afisa Ustawi wa Jamii nk. Au Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anapokea shauri la mtoto kuhusu mahitaji ya shule na anampa rufaa kwenda kwenye asasi za kiraia.

Mfano wa 2: Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anatambua shauri la mtoto la mtoto mwenye maambukizo wa VVU ambaye hajaanza kutumia matibabu ya kufubaza VVU. Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anampa rufaa mtoto kwenda kwenye kituo cha afya na pia anaweza kufanya kazi na Kamati inayosimamia, Ulinzi wa wanawake na watotoili kuona kama kamati hiyo inaweza kusaidia kuhamasisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya usafiri wa walezi wa watoto.

Kitini cha 9: Muundo wa Usimamizi na Utumiaji wa Kanuni

Msimamizi wa Mashauri ya Watoto	Anatambua shauri la mtoto Anatoa huduma za moja kwa moja kadiri awezavyo. Kutoa rufaa za watoto kwa ajili ya msaada na matunzo ya baadae. Kufuatilia ili kuhakikisha mtoto anapata matunzo yanayostahili.	Kuweka kumbukumbu za Mashauri ya Watoto.
		Kutoa taarifa.
Msimamizi wa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto	Usimamaizi Kutoa taarifa za Mashauri ya Watoto kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya.	Kusimamia na kusaidia.
		Kuhakiki mashauri yaliyofanywa na Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii.
		Kutoa msaada wa kitaalam kwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii. Kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya.
Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya	Kuwashauri Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ngazi ya Jamii. Kuwasaidia Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii. Kuwasismamia Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii. Na wao kuwa sehemu ya Rufaa.	Kuhakiki Takwimu
		Kupitia kumbukumbu
		Kuwasimamia Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii.
		Rufaa
KANUNI	**TAFSIRI**	**MIFANO**
Usidhuru	Shughuli na afua zimebuniwa kwa ajili ya kumsaidia mtoto (na familia) na zisiwaletee madhara zaidi.	Mtoto aliyenyanyaswa kingono na Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii wanamhukumu kwamba amevaa vibaya ndio maana amebakwa.

Kwa maslahi ya mtoto	Inamaanisha Ustawi wa mtoto na vitendo na maamuzi yanayochukuliwa, na namna ambavyo watoa huduma wanahusiana na watoto na familia zao, inafanyika kwa kuzingatia maslahi ya watoto.	Mwenendo wa kesi inayomuhusu mtoto mhalifu mahakamani inatakiwa kufanyika faragha ili kulinda utu wake.
Uwajibikaji	Uwajibikaji inamaanisha kukubali wajibu na mtu kuwajibika kwa matendo yake,	Kama ni Msimamizi wa Mashauri ya Watoto, na inatokea umesababisha madhara zaidi kwa mtoto kwa kutoa masuala yake ya siri kwa hiyo unatakiwa kuwajibika kwa hatua zozote zitakazochukuliwa dhidi yako. Au Utekelezaji wa majukumu na utoaji taarifa kama ilivyokubalika katika hadidu za rejea.
Kuzingatia uelewa wa makuzi na haki za mtoto	Tathmini na afua lazima zifanywe kwa kuzingatia uelewa kuhusu ukuaji wa mtoto katika familia yake na mazingira yake.	Tathmini ya msichana balehe ambaye amefanyiwa ukatili wa kingono lazima ufanywe na Msimamizi wa Mashauri ya Watoto wa kike.
Kutoa huduma na michakato inayozingatia tamaduni stahiki.	Wasimamizi wa Mashauri na taasisi lazima zitambue na kuheshimu mila na tamaduni na kuzingatia tofauti zilizopo miongoni mwa wanajamii (Kwa mfano kabila, Utamaduni, lugha na dini) katika jamii wanazofanya kazi.	Huwezi kugawa nguruwe kama mradi wa kujipatia kipato kwa familia za kiislam.
Kuridhia/au kukubaliana	Kuridhia ni kukubali kwa hiari kwa mtu mwenye uwezo wa kutoa ridhaa na ambaye hajashurutishwa. Ili kutoa "ridhaa", mtoto lazima awe na uwezo wa kuelewa na kufanya uamuzi kutokana na mazingira yake mwenyewe. Mtoto anaweza kujitoa au kuacha kupata huduma.	Msichana balehe mwenye umri wa miaka 16 ambaye anapaswa kupewa rufaa kwenda HTC.
Kuheshimu faragha na kubadilishana taarifa za mahitaji ili kujua msingi	Faragha huamua namna ya kubadilishana taarifa ya hitaji ili kujua msingi. Ni mchakato ambapo taarifa huzuiwa ili zisidondekee kwenye mikono isiyo salama na zinapatikana tu kwa wale wanaoruhusiwa kuzipata.	Umemhoji mtoto na amekuwa wazi kwamba ana maambukizo wa VUU hutakiwi kumweleza mtu mwingine yeyote kuhusu habari hizo.

Kufanya kazi bila ubaguzi	Epuka kuwahudumia watoto kwa utofauti kwa sababu ya tabia zao binafsi au kutokana na kundi alilopo (kwa mfano: jinsia, umri, hali ya kiuchumi, rangi, dini, kabila, ulemavu, kujitambua au muelekeo wa kingono).	Unapotoa elimu kuhusu masuala ya afya ya uzazi, wahusishe wasichana na wavulana balehe.
Zingatia mipaka ya weledi na elezea mgongano wa kimasilahi	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto na taasisi wafanye kazi kwa uaminifu kwa kutotumia uwezo wao vibaya au imani ya watoto na familia zao.	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto kutumia nafasi yake kumlaghai mtoto. Kama kufanya mapenzi ili wapewe huduma.
Tumia mfumo wa familia na mteja	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wazingatie rasilimali za wateja na familia katika kushughulika nao. Huduma zizingatie mahitaji yao ya pekee na malengo.	Familia ndio inatakiwa kuamua aina ya shughuli ya kujipatia kipato wanayotaka kama mbuzi na ulimaji wa bustani! Msichana wa miaka 15 anaweza kuamua aina ya mafunzo ya ufundi anayohitaji.
Zingatia lengo na tumia dhana ya uwezo	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wazingatie namna ya kufikia malengo yaliyoainishwa katika mpango wa huduma, ili kufanya hivyo zingatia uwezo wa mteja badala ya mapungufu yake.	Msimamizi wa Mashauri ya Watoto anaweza kupanga kumsaidia mtoto mahitaji ya shule na kuamua kuangalia familia kama ina rasilimali za kumsadia mtoto hata kwa kufuatilia maendeleo yake ya shule.

Kitini cha 10: Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto ni:

- Watetezi katika kuboresha hali za watoto na familia zao.
- Husukumwa na wateja, maamuzi na hatua wanazochukua hutegemea mahitaji na mazingira ya mtoto na familia zao.
- Umakini kuhusu tamaduni za mteja na jamii.
- Wahalisia na hufikiria mbele zaidi wakati wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto.
- Wapo katika jamii - Hufanya kazi katika jamii zao.
- Wanyumbufu - Waweze kutumia rasilimali zilizopo kwa ustawi wa watoto na familia zao

Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni watu wanaojitolea kufanya kazi moja kwa moja na Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi, vijana balehe, na vijana na familia zao. Majukumu ya Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii ni pamoja na lakini siyo pekee:

1. Kuwatambua Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi wanaohitaji huduma za Ustawi na Ulinzi kwa kutumia mifumo ya kijamii.
2. Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu mashauri yote yanahusu ulinzi wa mtoto kwa Afisa Ustawi wa Wilaya kwa ajili ya usimamizi wa mashauri zaidi.
3. Kuzuia na kushughulikia ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia na kihisia, unyonywaji wa kingono, biashara haramu ya usafirishaji watoto, kazi hatarishi kwa watoto, unyanyasaji nyumbani, shuleni, katika jamii pamoja na vitendo vya tamaduni hatarishi kama vile ukeketaji na ndoa za utotoni.
4. Kutambua na kutathmini hali za watoto na familia ambao wana mahitaji ya kiulinzi na kiustawi.
5. Kutunza kumbukumbu za watoto na familia zilizotambuliwa kama wanahitaji msaada na kuhuhisha taarifa za watoto kwa muda wote.
6. Kuhamasisha haki ya mtoto kwa kufanya kampeni ya kuhusu uelewa wa haki za mtoto katika jamii yako.
7. Kutambua rasilimali katika jamii husika na kujenga uhusiano mzuri wa kikazi na kada nyingine katika jamii na wadau.
8. Kutoa rufaa kwenye huduma stahiki.
9. Kufanya ufuatilaji wa kawaida wa Mashauri ya Watoto, pamoja na hali ya rufaa ili, kuangalia maendeleo.
10. Kuangalia utumiaji wa huduma zinazotolewa kwa watoto na kutoa taarifa kuhusu kikwazo chochote ambacho kinatakiwa kifanyiwe kazi katika utoaji wa huduma.
11. Kuwaunganisha walezi na familia katika huduma za jamii kama vile shughuli za kujipatia kipato na vikundi vya malezi.
12. Kutambua na kuhamasisha watoto, vijana balehe na vijana kujua hali zao kuhusu VVU kwa kwenda kupata unasahii kwa hiari na kupima VVU. Tumia maswali haya ili kutathmini kama kuna hitaji la unasihii na kupima VVU.
    i) Je, mtoto amewahi kupelekwa hospital?
    ii) Je, mtoto ana matatizo ya ngozi?
    iii) Je, mzazi mmoja au wote wa mtoto wamefariki?
    iv) Je, mtoto alikuwa amedhoofika kiafya miezi mitatu iliyopita?
13. Kuwasaidia WWKMH na familia zao kupata huduma za msingi za afya, ikiwa pamoja na upimaji wa VVU, unasihi na matibabu, as well as huduma za kijamii.
14. Kuwasaidia watoto walio kwenye dawa za kufubaza VVU kuwa wafuasi wa matibabu.

15. Kuziwezesha familia kutatua matatizo yao kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka.
16. Kutembelea familia za WWKMH mara kwa mara na taasisi zingine zinazohusiana na ustawi na ulinzi wa MVC ili kujua ustawi wa watoto.
17. Kutembelea kaya ambazo zipo katika hatari ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili.
18. Kusambaza taarifa rafiki kwa watoto katika jamii yako.
19. Kuandaa na kutoa taarifa kila mwezi kuhusu watoto waliopata msaada kwa kitengo cha Ustawi wa Jamii kupitia Msaidizi Ustawi wa Jamii wa Kujitolea.

Kitini cha 11: Kanuni za Usimamizi wa Mashauri ya Watoto ya Watoto

Kanuni	Tafsiri
Usidhuru	Shughuli na afua zimebuniwa kwa ajiri ya kumsaidia mtoto (na familia) na zisiwaletee madhara zaidi.
Kwa masilahi mapana ya mtoto	Inamaanisha Ustawi wa mtoto na vitendo na maamuzi yanayochukuliwa, na namna ambavyo watoa huduma wanahusiana na watoto na familia zao, inafanyika kwa kuzingatia masilahi ya watoto.
Uwajibikaji	Uwajibikaji inamaanisha kukubali wajibu na mtu kuwajibika kwa matendo yake,
Kuzingatia uelewa wa makuzi na haki za mtoto	Tathmini na afua lazima zifanywe kwa kuzingatia uelewa kuhusu ukuaji wa mtoto katika familia yake na mazingira yake.
Zisikilizwe haki za mtoto na mawazo yazingatiwe	Watoto wanahaki ya kuulizwa na kupata maoni yao na yazingatiwe katika maamuzi ya masuala yanayoathiri maisha yao kutokana na umri, ukomavu na uwezo.
Kutoa huduma na michakato ya inayozingatia tamaduni stahiki	Wasimamizi wa mashauri na taasisi lazima zitambue na kuheshimu tofauti zilizopo (kwa mfano: kabila, utamaduni, lugha na dini) katika jamii wanazofanya kazi.
Kuridhia/au kukubaliana	Kuridhia ni kukubali kwa hiari kwa mtu mwenye uwezo wa kutoa ridhaa na ambaye hajashurutishwa. Ili kutoa "ridhaa", mtoto lazima awe na uwezo wa kuelewa na kufanya uamuzi kutokana na mazingira yake mwenyewe. Mtoto anaweza kujitoa au kuacha kupata huduma.
Kuheshimu faragha/usiri na kubadilishana taarifa za mahitaji ili kujua msingi	Faragha huamua namna ya kubadilishana taarifa ya hitaji ili kujua msingi. Ni mchakato ambapo taarifa huzuiwa ili zisidondekee kwenye mikono isiyo salama na zinapatikana tu kwa wale wanaoruhusiwa kuzipata.
Kufanya kazi bila ubaguzi	Epuka kuwahudumia mtoto kwa utofauti kwa sababu ya tabia zao binafsi au kutokana na kundi alilopo (kwa mfano: jinsia, umri, hali ya kiuchumi, rangi, dini, kabila, ulemavu, kujitambua au muelekeo wa kingono).
Zingatia mipaka ya weledi na elezea mkinzano wa kimasilahi	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto na taasisi wafanye kazi kwa uaminifu kwa kutotumia uwezo wao vibaya au imani ya watoto na familia zao.
Kushughulika kwa kutumia familia na mteja mwenyewe.	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wazingatie rasilimali na mazingira ya familia na mteja. Huduma zizingatie mahitaji yao ya kipekee na malengo. Wasimamizi wa mashauri wahakikishe wanawashirikisha watoto kwa kuzingatia umri stahiki.
Kuzingatia lengo na mambo chanya	Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wazingatie kufikia malengo walioweka katika mpango wa huduma badala ya kuangalia mapungufu ya mteja, kuzingatia mambo chanya na uwezo wa mteja.

Kitini cha 12: Maadili ya Kufanya Kazi Kwa Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii

Mimi_____ najua jukumu langu kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii na kwa hiari yangu naahidi kufanya yafuatayo:

1. Kushughulikia kwa kujiamini kwa kiwango cha juu taarifa zote zinazohusiana na Mashauri ya Watoto ya ulinzi wa watoto ambayo yatanifikia.
2. Kuheshimu uadilifu wa watoto wote na usiwapige au kuwaumiza kimwili au kuwanyanyasa watoto.
3. Kutoa taarifa kuhusu tishio la tatizo lolote la ukatili, unyanyasaji au unyonywaji wa watoto na yeyote bila hofu au kupendelea.
4. Kutojihusisha kingono na mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18, ikiwa pamoja na watoto ambao wanaweza kuwa wananyonywa katika biashara ya ngono.
5. Kutomnyonya mtoto moja kwa moja au kumweka katika mazingira ambayo yatamfanya awe hatarini katika aina ya unyonyaji wowote.
6. Kutoajiri watoto wa umri chini ya miaka 18 kama wafanyakazi wa nyumbani.

Saini: _____

Kitini cha 13: Vigezo – Wakati wa Kufungua Shauri la Mtoto

- Kaya inayoongozwa na mtoto (chini ya miaka 18)
- Kaya inayoongozwa na mlezi mzee (miaka 60 au zaidi)
- Mtoto ambaye ni yatima wa mzazi mmoja au wote wawili na hana mahitaji ya msingi
- Mlezi mwenye maradhi sugu na ambaye hana mahitaji ya msingi
- Mtoto anayelelewa na mlezi mlevi
- Mlezi au kijana balehe katika kaya mwenye umri wa miaka 10 – 19 anayejishughulisha na biashara ya ngono
- Msichana balehe mmoja au zaidi wenye umri wa miaka 10-19 ambao wanafanya mapenzi
- Msichana balehe mwenye umri wa miaka 10 -19 katika kaya ambaye ana mimba au amezaa mtoto
- Mtoto ambaye ana uambukizo wa VVU
- Mtoto mmoja au zaidi katika kaya ambao wana utapiamlo mkali
- Mtoto aliyefanyiwa ukatili au yupo katika hatari ya kufanyiwa ukatili
- Mtoto anayefanya kazi mtaani/kuishi mitaani.

Kitini cha 14a: Fomu ya Usajiliwa Kaya zenye Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

Kitini cha 14b: Jinsi ya kujaza Fomu ya Usajili wa Kaya zenye Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

Kitini cha 15: Zoezi la Mazingira ya Usaili/Usajili

Soma zoezi la mazingira ya Usaili/Usajili Ulilopewa. Kwa kila zoezi, jadili na kujibu maswali yafuatayo:

1. Tendai ni mtoto wa kike wa miaka 8 na anaishi maisha ya furaha na baba yake pamoja na mama yake wa kambo na ameanza shule. Anafurahia kuwa na watoto wengine nani mwenye afya na furaha.

    - Je, ungefungua faili la shauri la huduma la mtoto huyu?
    - Kwa nini ndiyo/kwa nini siyo
    - Je, mtoto huyu anahitaji hatua za haraka?

2. Shungu ni msichana wa miaka kumi na tatu na anaishi na mjomba na marafiki zake wa kiume wawili. Shungu pamoja na mjomba wake na marafiki wawili wanalala kwenye chumba kimoja.

    - Je, ungeweza kufungua faili la shauri la mtoto/usajiri wa mtoto huyu?
    - Kwa nini ndiyo/kwa nini siyo
    - Je, mtoto huyu anahitaji hatua za haraka?
    - Kwenye miundo au watoa huduma gani ambako unaweza ukaona mashauri ya watoto mengine kama ya Shungu?

3. Federico ni mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka tisa kutoka kwenye kundi maalum katika jamii, ambalo linanyimwa huduma ambazo watu wengine wanapewa katika nchi yake. Hii inajumuisha kupata kwa urahisi ajira na makazi.

    - Je ungefungua faili la shauri la mtoto/kumsajili mtoto huyu?
    - Kwa nini ndiyo/Kwa nini hapana?
    - Mtoto anahitaji hatua za haraka?

4. Owen ni kijana wa kiume wa miaka kumi na tano na amekuwa anaishi peke yake jijini kwa miaka mitatu. Baba yake alimfukuza aktafute kazi. Mwanzoni aliomba omba mtaani. Kwa sasa anafanya ameajiriwa katika kiwanda cha chuma chakvu ambapo anafanya kazi siku nzima ya kukata vyuma kwa kutumia mashine kubwa. Anapenda kazi yake lakini hana sehemu maalum ya kulala na hajisikii salama usiku.

    - Je, ungefungua faili la shauri la mtoto/kumsaajiri mtoto huyu?
    - Kwa nini ndiyo/kwa nini hapana?
    - Je, mtoto huyu anahitaji hatua za haraka?

Kwenye miundo au watoa huduma gani ambako unaweza ukaona mashauri ya watoto mengine kama ya Owen?

Kitini cha 16: Kitendea Kazi cha Kutambua Kiwango cha Madhara ya Ukatili

Kiwango	Tafsiri	Maelezo	Muda	Mifano
Kiwango cha juu uhatarishi	Maisha ya mtoto yapo hatarini kwa kiasi kikubwa au mtoto amepata madhara makubwa kiasi cha kuathiri maendeleo na ustawi wake endapo hatua za dharura hazitachukuliwa.	Mtoto anahitaji huduma za dharura za afya au msaada wa kisheria. Mtoto yupo katika hatari ya kupata majeraha ya kimwili, kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono au anaendelea kufanyiwa vitendo hivyo, mtoto yupo katika hatari ya kupata ulemavu wa kudumu, kuingizwa katika biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu au pengine hata kufa endapo ataachwa katika mazingira aliyopo kwa sasa bila kuchukua hatua zozote.	Hatua lazima zichukuliweharaka iwezekanavyo. Toa taarifa haraka kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya au Kituo cha Polisi.	• Ndoa za utotoni • Ukatili wa kingono • Ukatili wa kimwili • Mtoto anaishi na VVU na ameacha kutumia dawa lakini anaumwa sana • Watoto wanaoishi nje ya mazingira ya familia • Wahanga wa vitendo vya Ukeketaji
Kiwango cha kati cha uhatarishi	Mtoto yupo katika hatari ya kupata madhara ya kiwango cha kati na hakuna mpango mahsusi wa kumlinda	Mtoto yupo katika hatari ya kupata madhara ya kiwango cha kati na hakuna mpango mahsusi wa kumlinda. Hatahivyo hakuna uthibitisho wowote kama mtoto yupo katika kiwango cha uhatarishi wa unaoweza kusababisha majeraha au kifo/Hakuna dharura.	Huduma itolewe ndani ya saa 72	• Utelekezwaji unaoweza kuathiri maendeleo ya mtoto kama hautashughulikiwa lakini hakuna athari kwa usalama na uhai wa mtoto • Ukatili wa kihisia • Ufuasi hafifu wa dawa za kupunguza makli ya VVU • Magonjwa sugu,kuchelewa kukua kulingana na umri au ulemavu • Ajira mbaya kwa watoto

Kiwango kidogo cha uhatarishi	Mtoto hayupo katika hatari kwa sasa na kama kuna hatari madhara yake ni madogo sana japo kuna viashiria kwamba endapo hatua hazitachukuliwa mtoto anaweza kupata madhara.	Nyumbani ni salama kwa watoto hata ivyo kuna viashiria kwamba mtoto anaweza kupata madhara kama huduma hazitatolewa Kuna umuhimu wa afua za ulinzi wa mtoto.	Huduma zianze ndani ya siku 14	• Watoto wasikwenda shule • Vyeti vya kuzaliwa • Watoto wanaofanya kazi nyingi za nyumbani zinazoweza kuathiri ukuaji wao • Mahitaji ya shule kama ada na sare za shule • Huduma za kawaida za afya

* Mashauri yote ya kisheria lazima yachukuliwe kuwa ni ya kiwango cha juu au cha kati kulingana na madhara aliyopata mtoto. Kama mtoto yupo katika madhara makubwa zaidi, muongozo wa kiwango cha juu cha uhatarishi utatumika

Kitini cha 17a: Kitendea Kazi cha Kutambua Vihatarishi vya VVU

Kitini cha 17b: Mwongozo wa Ujazaji wa Kitendea Kazi cha Kutambua Vihatarishi vya VVU

Kitini cha 18: Visa Mafunzo Muhimu (Usaili)

Kisa Mafunzo Muhimu cha Kito: Utambuzi/Usajili/Usaili

Umepata taarifa kwamba katika kijiji chako kuna mvulana wa umri wa miaka 7 ambaye muda wote anakaa nyumbani. Hata hivyo, wakati mama yake akiondoka nyumbani hufunga mlango na kumuacha peke yake. Muda wote analia.

Maswali:

1. Ungeichukulia/ungeifanya hadithi ya Kito kama shauri la mtoto?
2. Kama ndiyo, kwa nini? Na kama hapana, kwa nini?
3. Kama umeamua hili ni shauli la huduma utachukua hatua gani?
4. Kwenye miundo au watoa huduma gani ambako waweza kutambua Mashauri ya Watoto kama haya ya kito?

Kisa Mafunzo Muhimu cha Sinikiwe: Utambuzi/Usajili/Usaili

Majirani walioguswa wamekujulisha kuhusu Sinikiwe, mtoto wa kike waumri wa miaka 9 ambaye anakaa na baba yake (Robert) na anaonekana amedumaa na mwenye utapiamlo, na anavipele mdomoni. Inasemekana kwamba mama yake, aliyefariki miaka 2 iliyopita, alikuwa muathirika wa UKIMWI.

Maswali:

1. Ungeichukulia/ungeifanya hadithi ya Sinikiwe kama shauri la mtoto?
2. Kama ndiyo, kwa nini? Na kama hapana, kwa nini?
3. Kama umeamua hili ni shauli la huduma utachukua hatua gani?
4. Kwenye miundo au watoa huduma gani ambako waweza kutambua Mashauri ya Watoto kama haya ya Sinikiwe?

Kisa Mafunzo Muhimu cha Shole: Utambuzi/Usajili/usaili

Umepata taarifa kutoka kwa mwalimu wa shuleni kuhusu mtoto ambaye kuna uwezekano kafanyiwa ukatili:

1. Kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii, ungeichukulia/ungeifanya taarifa hii kama shauri la mtoto?
2. Kama ndiyo, kwa nini? Na kama hapana, kwa nini?
3. Kama umeamua hili ni shauli la huduma utachukua hatua gani?
4. Kwenye miundo au watoa huduma gani ambako waweza kutambua Mashauri ya Watoto kama haya ya Shole?

Kitini cha 19: Kitendea Kazi cha Tathmini ya Mahitaji na Uwezo wa Mtoto

Kitini cha 20: Vitu vya Kuangalia Wakati wa Kufanya Tathmini

Vitu vya kuangalia	Maswali ya kuuliza
Umuhimu wa mahusiano ya familia	• Nani ambaye ni/alikuwa mwanafamilia muhimu kwa mtoto? Hawa wanaweza kuwa walezi/ wanafamilia ambao wanaishi na mtoto au wanafamilia muhimu ambao mtoto amewapoteza (kutokana na kifo au kutelekezwa). Kama mtoto ni yatima, kipindi gani kimepita tangu amefiwa? Hii inauwezekano mkubwa wa kuchangia katika hisia na tabia za mtoto.
Maendeleo ya afya kwa ujumla, VVU na mahitaji ya msingi	• Je, familia inauwezo wa kumpatia mtoto chakula cha kutosha na malazi? Wanajilinganishaje na majirani zao? • Je, mahitaji ya afya ya msingi ya mtoto yanafikiwa, pamoja na chanjo na kuzuia malaria? Je, mtoto anaonyesha matatizo yeyote ya kiafya ambayo hayajashughulikiwa? • Je, mtoto anaonekana yuko sawasawa katika masuala ya kimo, uzito kulingana na umri wake? • Mlezi anafahamu kuhusu hali ya maambukizi ya VVU ya mtoto? - Je, mlezi amemueleza mtoto kuhusu hali yake ya maambukizi? Kama bado kwa nini? • Kama mtoto anaishi na VVU, je ameshaanza matibabu? • Kama bado hajaanza, kwa nini? Kama mtoto yupo kwenye matibabu, je, anazingatia ufuasi wa dawa? - Kuna changamoto zozote katikaufuasi wa dawa? • Kama hali ya maambukizi ya VVU ya mtoto haijulikani, je ana mojawapo ya vigezo vifuatavyo: - Mtoto anaishi na mwanafamilia ambaye ana VVU - Mtoto hanawiri - Mtoto hajapata matibabu kwa ajili ya ukatili wa kingono aliofanyiwa hivi karibuni **Zingatia: Kama majibu ni NDIYO kwa vigezo hivi vitatu, mtoto anapaswa kupelekwa kwenye huduma ya unasihi na kupima VVU.**
Tabia, maisha ya kijamii na elimu	• Je, mtoto anaonyesha tabia sawa na watoto wengine wa umri wake? • Kuna mabadiliko yeyote ya tabia kwa mtoto ambayo hayaelezekiau yanayohusiswha na tukio? Mfano: mtoto anayeonyesha woga au kukata tamaa • Mahusiano ya mtoto na watu wengine nje ya familia yakoje, kama marafiki, ndugu wengine, majirani na waalimu? • Mtoto napenda nini? • Mambo gani ambayo mtoto huyafanya vyema? Ana uwezo gani? Je, mtoto anajihusisha katika shughuli zinazoendana na umri wake? • Maendelo yake shuleni yakoje? Je, anahudhuria shule mara kwa mara? Anaendelea vizuri shuleni?

Dalili za unyanyasaji au kutelekezwa	• **Dalili za unyanyaswaji kingono** – stadi mbaya za mahusiano, tabia za utegemezi, anatabia za fujo za kingono, anajishika sehemu za siri mara kwa mara, ni mgumu kuamini watu wengine, ana woga usioelezeka • **Dalili za unyanyasaji kimwili** – vidonda vidogo au vikubwa, mikwaruzo, makovu, alama za kung'atwa, kuonyesha wasiwas au kutoamini wengine, kuwa na tabia ya kukimbia watu wazima, kuwa na tabia za ugomvi kwa wengine. • **Dalili za unyanyasaji kisaikolojia au kihisia** – kuwa mgomvi, kutojiamini, kujitenga, matumizi ya madawa ya kulevya na vilevi, tabia ya kudeka, kutokuwa na maendeleo mazuri shuleni na ugumu katika kujifunza, kuchelewa kukua kuhisia na kiakili, kuwa na wasiwasikupita kiasi, kuchelewa kuongea au kuwa na matatizo ya ghafla katika kuongea,woga wa mazingira mapya, kutoonyesha hisia kulingana na matukio ya kuogopesha, kutoroka shule au nyumbani, kushuka kitaaluma na kutozingatia masomo, anamawazo ya kujiua au ameshajaribu kutaka kujiua.
Stadi za mlezi, uwezo kiafya na msaada	• Mlezi anatoaje adhabu kwa mtoto? Je, mlezi ana stadi za malezi chanya? Kama mtoto ni chini ya miaka 5, mlezi anauelewa wa makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto? • Mlezi ana elimu kuhusu lishe na kuhakikkisha mtoto anakula vizuri ili aendelee na kukua vyema? • Kama mtoto ana maambukizi ya VVU, mlezi ana stadi za kumsaidia mtoto kuwa mfuasi mzuri wa dawa? • Je, mlezi anaelewa hali yake ya maambukizi ya VVU? • Kama mlezi ana maambukizi ya VVU, je, ameshaanza matibabu? o Kama bado kwanini? • Kama yupo kwenye matibabu, anazingatia matumizi ya dawa? • Kuna changamoto katika kuwa na ufuasi wa dawa? • Je, mlezi ana matatizo mengine ya afya? • Je, mlezi ana sonona au matatizo ya kihisia? Je, naye ni sehemu ya kikundi cha msaada?
Uwezo wa familia na mitandao	• Hali ya uchumi ya familia ikoje? Je, mlezi au mwanafamilia wanajihusisha katika vikundi vya kuweka na kukopa/ au kujihusisha na shughuli yeyote ya kujiingizia kipato? • Je, familia ina akiba ya chakula cha kutosha? • Je, wafamilia wana kadi za bima ya afya akiwemo na mtoto? • Je, familia ina uwezo (rasilimali) gani? Kuna ushirikiano ndani ya familia na jamii? • Nani antoa mahitaji kwa familia? Nani msuluhishi katika familia? • Wanaabudu wapi? Je, kuna vikundi au jumuiya zozote wanazojihusisha nazo? Je, jumuhiya/vikundi hivyo huwa vinawasaidia? • Je, kuna watu wengine (kama majirani, ndugu, huduma au taasisi) ambazo zinawapatia msaada?

Kitini cha 21: Tathmini ya Visa Mafunzo vya Msingi Sehemu ya Kwanza

KISA MAFUNZO CHA MSINGI KINACHOMUHUSU KITO;

TATHMINI, SEHEMU YA KWANZA

KUANDAA MAHOJIANO NA UCHUNGUZI

Mara baada ya kupata taarifa zinazomuhusu mtoto wa kiume ambaye mama yake amekuwa akimuacha nyumbani peke yake, unaamua kuitembelea familia hii nyumbani ili kupata taarifa zaidi kuhusu suala hilo.

1. Ukiwa kama muhudumu wa mashauri ya watoto unawezaje kushughulikia shauri hili?
2. Utauliza maswali gani?
3. Vitu gani muhimu vya kuchunguza?
4. Ukiacha suala la kumtembelea nyumbani, mbinu gani nyingine unayoweza kuitumia ili kupata taarifa zaidi?

KISA MAFUNZO CHA MSINGI KINACHOMUHUSU SINIKIWE;

TATHMINI, SEHEMU YA KWANZA

KUANDAA MAHOJIANO NA UCHUNGUZI

Unatembelea nyumbani kwa Robert kupata taarifa zaidi:

1. Utamkabili vipi Robert (ambaye ni baba)?
2. Je, unawezaje kufanya mazungumzo na Sinikiwe hasa ukizingatia mazingira anayoishi na hisia zake?
3. Utauliza maswali gani?
4. Vitu gani muhimu vya kuchunguza?
5. Ukiacha suala la kumtembelea nyumbani, mbinu gani nyingine unaweza kuitumia ili kupata taarifa zaidi?

KISA MAFUNZO CHA MSINGI KINACHOMUHUSU SHOLE;

TATHMINI, SEHEMU YA KWANZA

KUANDAA MAHOJIANO NA UCHUNGUZI

Mara baada ya kupata taarifa hii, unabaini kuwa hili ni shauri la kushughulikiwa. Kwa kuanzia unaamua kutembelea shuleni ambapo binti huyo anasoma.

1. Utaanzaje kushughulikia shauri hili linalomuhusu Shole?
2. Kwa nini unapaswa kufikiria kutembelea shuleni kwanza badala ya kutembelea nyumbani?
3. Utamkabili vipi Shole? Utauliza maswali gani?
4. Utachunguza vitu gani?

Kitini cha 22: Kisa Mafunzo cha Msingi cha Shole, Tathmini, Sehemu ya 2

KISA MAFUNZO CHA MSINGI

TATHMINI SEHEMU YA PILI

MATOKEO YA KUTEMBELEA MAJUMBANI NA MAHOJIANO YA KIJAMII:

Wakati wa kutembelea nyumbani na kufanya mahojiano na mama wa mvulana na majirani wengine, unagundua yafuatayo:

- Mvulana anaitwa Kito na ana umri wa miaka saba ila kwa muonekano anaonekana kama mtoto wa miaka miwili.
- Mtoto huyo anakuwa taratibu na hawezi kukaa mwenyewe kwa kujitegemea.
- Mwili wake umejaa vidonda vilivyosababishwa na kulala kwa muda mrefu na ana utapiamlo.
- Hawezi hata kuinua mikono, kitu pekee anachofanya ni kulia tu.
- Mama yake anasema kuwa alipozaliwa alionekana ni mtoto wa kawaida na mwenye afya.
- Alipofikisha umri wa miezi tisa aliugua sana na alilazwa hospitali kwa muda, lakini baadae waliruhusiwa kurudi nyumbani na kwamba watakuwa wanampeleka kiliniki kila mwezi.
- Tangu wameruhusiwa kutoka hospitali mama wa mtoto hakuweza tena kuendelea kumpeleka mtoto kiliniki kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha kwa ajili ya usafiri na kulipia huduma za kiliniki.
- Mama yake kito analea watoto wake peke yake, na pia ana watoto wengine wawili wanaomtegemea kwa kila kitu.
- Anafanya biashara ya kuuza matunda sokoni.
- Amekiri kwamba amekuwa akimuacha Kito peke yake nyumbani kwa sababu hana mtu wa kumuachia, kito anakula mlo mmoja kwa siku kwani ndicho kinachoweza kupatikana.
- Majirani pia wamethibitisha kuwa kito amekuwa akifungiwa ndani kwa muda mrefu wakati mama yake akipambana kutafuta mahitaji.
- Baadhi yao wanahisi kuwa huenda mtoto ana ulemavu, lakini kama mama yake angeendelea kumpeleka kiliniki huenda tatizo lingekwisha.
- Wengine wanahisi kuwa mtoto huyo ana ulemavu kwa sababu watoto wengine wa rika lake wapo shuleni.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kulingana na matokeo ya tathmini uliyofanya:

1. Ukiwa Kama Msimamizi wa Mashauri ya Watoto, tatizo ni nini hapa?
2. Nini sababu ya matatizo hayo?
3. Nini maoni yako kuhusiana na hali ya afya ya Kito?

KISA MAFUNZO SINIKIWE

TATHMINI: SEHEMU YA PILI

MATOKEO YA KUTEMBELEA NYUMBANI NA MAHOJIANO YA KIJAMII:

Wakati wa kumtembelea na kufanya mahojiano na baadhi ya watu wanaomfahamu Sinikiwe, unagundua yafuatayo:

- Sinikiwe, ambaye amezaliwa peke yake, anaishi katika chumba kimoja na baba yake tangu mama yake alipofariki. Analala kitanda kimoja na baba yake.
- Robert anaelezea kuwa, sababu inayomfanya alale kitanda kimoja na binti yake ni kwa sababu anamiliki mablanketi mawili yaliyochanika hali ambayo inampa ugumu wa kuandaa mahala pa kulala
- Nyumba wanayoishi inamilikiwa na wanandoa ambao wanaishi mji mwingine, na kumfanya Robert kupata makazi kwa kuwa yeye amekuwa ni mlinzi wa makazi hayo. Robert hana vyombo wala mifufo yeyote.
- Ingawa hana ulemavu wowote, Robert hana kazi na anategemea zaidi kipato kutoka katika vibarua visivyo na uhakika pamoja na kupewa msaada na wasamaria wema
- Robert na binti yake mara nyingi hupata mlo mmoja kwa siku
- Ndugu pekee anayejulikana ni ndugu wa upande wa mama yake Robert ambaye anaishi Arusha, ambaye ameolewa na mfanyabiashara tajiri. Robert amepoteza mawasiliano naye tangu miaka mitano iliyopita.
- Robert anaelezea kwamba, miaka miwili kabla ya kifo cha Soneni (mama yake Sinikiwe) walikuwa wametengana baada ya kuwa na mgogoro.
- Sinikiwe hana cheti cha kuzaliwa.
- Unagundua kuwa Sinikiwe yupo karibu sana na baba yake, na angependa kuishi naye muda wote. Inaonekana anamuamini baba yake kuliko mtu mwingine yeyote.
- Sinikiwe anaonekana amekata tamaa na hana damu, na hayupo huru ukiwepo. Na ni mkimya wakati wote. Mwalimu wake anakueleza kuwa mara nyingi Sinikiwe haudhurii masomo shuleni hali inayosababishwa na kuumwa mara kwa mara au anakuwa anamsaidia baba yake kazi za nyumbani.
- Mwalimu wake anakutaarifu kuwa Sinikiwe hajalipiwa ada kwa muda mrefu, na hana sare za shule.
- Sinikiwe huwa hajichanganyi na wanafunzi wengine anaosoma nao, na mara nyingi hupenda kukaa peke yake.
- Unapoongea na majirani wanakwambia wanahisi Robert anamfanyia ukatili wa kingono binti yake.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kufuatana na matokeo ya tathmini uliyofanya:

1. Ni yapi matatizo hapa?
2. Nini vyanzo vya matatizo hayo?
3. Nini maoni yako binafsi kuhusu mazingira ya Sinikiwe? Yanawezaje kuathiri mawazo yako ya jinsi unavyoichukulia familia hii?

MATOKEO YA KUTEMBELEA SHULENI NA KUFANYA MAHOJIANO:

Wakati wa kutembelea shuleni na kufanya mahojiano na binti pamoja na mwalimu wake, unagundua yafuatayo:

- Binti anaitwa Shole na ana umri wa miaka 13.
- Anaishi na shangazi yake na mjomba wake (mume wa shangazi yake).
- Shangazi yake Shole anafanyakazi hotelini na huwa anaondoka nyumbani asubuhi sana na kurudi usiku sana huku mumewe akishinda nyumbani muda mwingi.
- Watoto wa shangazi ni wakubwa na wanajitegemea. Shole ndiye mtoto pekee wanayeishi naye.
- Kwa muda mrefu sasa tabia ya Shole imebadilika na mwalimu wake anagundua hilo. Shole hazingatii masomo yake tena. Wala hajichanganyi na watoto wenzake kama hapo awali. Anaonekana mwenye huzuni muda wote na anakwepesha macho yake kuangalia watu usoni.
- Mwalimu wake alitaka kujua kinachomsibu lakini Shole hakuweza kumwambia chochote mwalimu.
- Unaamua kuongea na Shole ili kujua kinachomsibu. Siku ya kwanza hakuweza kukwambia chochote na unapanga kuongea naye siku nyingine.
- Unakubaliana kuonana naye siku nyingine lakini sio kwenye mazingira ya shule. Anapendekeza umwelekeze unaoishi ili akufuate huko.
- Baada ya muda mrefu, hatimaye Shole anaamua kufunguka na kukueleza kuwa amekuwa akifanyiwa ukatili wa kingono kwa muda mrefu sasa na mjomba wake, na hajawahi kumueleza shangazi yake kwa kuwa anakazi nyingi na shangazi hana muda wa kuongea naye kutokana na kazi nyingi alizonazo.
- Lakini pia amekuwa akitishiwa na mjomba wake kuwa kama ikitokea akamwambia mtu yeyote basi atamuua.
- Shole anakumbuka pia kuwa bibi yake aliwahi kumwambia ni aibu kwa binti ambaye hajaolewa kuanza kushiriki vitendo vya ngono.
- Haya yote yamemfanya apate ugumu wa kumueleza mtu yeyote matatizo anayoyapitia.
- Shole ameathirika na hali hii kiasi wakati wote unapozungumza naye amekuwa akilia tu, amefikia hatua anasema anawachukia sana wanaume.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo, kutokana na matokeo ya tathmini uliyoifanya:

1. Kuna matatizo gani katika shauri la Shole?
2. Ni nini chanzo dhahiri cha tatizo hili?
3. Nini maoni yako kuhusiana na hali ya Shole?

Kitini cha 23: Hatua za Ukuaji wa Mtoto Mpaka Ujana Balehe

Hatua	Kimawasiliano	Kiakili	Kijamii	Kimwili
Miezi 3	Huonyesha kuzitambua sauti na sura alizoanza kuzizoea Hustushwa na sauti za ghafla	Humtambua mlezi anayekuwa naye muda mwingi Analia anapohisi njaa au kutojisikia vizuri	Anaweza kubembelezwa kwa sauti au kumgusaouch Huanza kutabasamu anapocheza na mtu	Anatambua mikono Ananyonya Anainua kichwa anapolazwa kifudifudi
Miezi 6	Anaanza kutoa sauti na ishara Huwa anageuka anaposikia sauti ya mtu au kitu	Anachukua vitu na kutia mdomoni Anachezea midoli kwa njia tofauti tofauti Anapenda kuchezea vitu	Huonyesha hofu kwa watu asiowatambua Anafanya vitu ila aonyeshwe umakini Anatambua watu tofaututofauti	Anaweza kujibiringisha kwa kulalia tumbo au mgongo Anajifunza kukaa kwa kusaidiwa Anajiongelesha na kurusha miguu na mikono
Miezi 12	Anaelewa baadhi ya maneno na ishara Anaigiza baadhi ya maneno au ishara Anaanza kuzungumza maneno yasiyoeleweka	Anajifunza kuwa vitu vipo hata kama havioni kwa wakati huo Anajifunza kutatua baadhi ya mambo yanayomkwaza Anaanza kutambuaa baadhi ya matatizo na madhara yake	Anatumia ishara Analia mlezi anapomuacha Anaanza kufurahia baadhi ya michezo	Anaweza kukaa bila kusaidiwa Anatambaa Anajifunza kusimama
Miaka 2	Anaelewa maneno kati ya 50-200 au ishara Anatumia sentensi ya maneno 2-3 au ishara Anatumia maneno rahisi au ishara	Anaweza kuhusianisha vitu Anatumia vitu vinavyohusiana Anakuwa makini katika michezo kwa muda mwingi	Anamuiga mlezi Anacheza na watoto wenzie Anaomba saada kwa wenzie pale anapohitaji	Anaweza kupanga vitu vingi wakati wa kuchezo Anatembea Anaweza kuchuchumaa

Miaka 3	Anaelewa baadhi ya maneno rahisi Anajua na kutumia maneno 500-1000 au ishara Anawasiliana mapema	Anaweza kuhusianisha maumbo ya vitu mbalimbali katika mashimo Anachambua vitu Anaweza kutenganisha vitu na kuvirudishia tena	Anafurahia kusaidia kazi nyumbani Anapenda kupongezwa akifanya jambo Anatambua hisia za wengine	Anakimbia,kuruka na kupanda kwenye baadhi ya vitu Anatumia mikono katika kazi mbalimbali Anarusha mpira
Miaka 5	Anaongea au kutoa ishara kama amefanya kitu Anaweza kutumia maneno au ishara Anauliza maswali mengi	Anafuata maelekezo mepesi Anajua kuhesabu	Anacheza na watoto wengine Anaelewa baadhi ya taratibu Anaelewa kuonyesha hisia	Anaweza kuigiza baadhi ya maumbo Anatembea kwa mguu mmoja Anaweza kutembea kwa kurudi nyuma kwa urahisi

Kitini cha 24: Hatua za Makuzi za Ujana Balehe Yenye Afya

Hatua	Kimawasiliano	Kiakili	Kijamii	Kimwili
Miaka ya awali ya ujana balehe, miaka 10 -14	Wanatazama wakati uliopo "hapa na sasa hivi." Hawana uelewa wa kutambua" kama nikifanya hivi, kitu Fulani kitatokea" au kuelewa tukio na matokeo yake. Wanakuwa na msongo, mara kwa mara wanajibu kwa hisia zaidi kuliko kwa mantiki. "	Kujiuliza maswali, kujiuliza 'mimi wa kawaida?" Mfulilizo wa ndoto za mchana. Hawana uhakika wanataka nini kitaaluma, malengo yanabadilika mara kwa mara. Wanatengeneza mfumo wao wa amali. Anaanza kuwa na hisia za kingono na kuchunguza masuala yanayohusu ngono. Anakuwa na hadhira ya kufikirika. Anatamani faragha. Wanaelezea matatizo yao kama "hakuna mtu anayenielewa"	Wanakosoa mamlaka, familia, malezi yasiyofaa (ingawa hatua hii ni muhimu katika sehemu ya makuzi ya motto inaweza kuonekana ni sehemu yenye changamoto kwa wazazi kuielewa). Upweke Kuwa na mabadiliko makubwa ya kihisia. Wanapuuza matukio yanayowakumbusha utotoni. Wanapenda kubishana na kukosa utiifu. Wankuwa na urafiki na marafiki wa jinsi inayofanana. Mawasiliano na jinsi tofauti huanza katika vikundi.	Kipindi cha balehe kinaingia kwa kasi. Muda wa kulala unabadilika (wanachelewa kulala) Anakua haraka na kuhitaji masaa 9 au zaidi ya kulala kwa siku. Viungo vya uzazi vinakuwa.
Umri wa kati wa ujana balehe miaka 15-17	Migogoro na familia inaanza: kijana balehe anakuwa na hofu ya kujitegemea.	Uwezo wa kufikiri kwa mambo kiujmla na madhara yake. Dhana ya tukio na matokeo inaeleweka. vizuri Kujifikiria mwenyewe.	Anakuwa na uimara na utii kwa makundi rika, mabadiliko ya mara kwa mara ya vitu anavyopenda na kuvichukia. Kuwa na matamanio ya kingono na kuanza kuchunguza kuwa na mwenza na uwezo wa kuvutia mwenz. Kufanya uchunguzi: katika ngono, madawa ya kulevya, marafiki, kazi mbalimbali na tabia hatarishi.	Tabia zinazohusu ngono tayari zishakamilika. Asilimia 95 ya kimo cha mtu mzima inakuwa ishakamilika.

Kitini cha 25: Aina za Malezi na Matokeo Yake

Aina ya malezi	Maelezo	Matokeo
Malezi ya kutumia mamlaka	Katika aina hii ya malezi, watoto wanatarajiwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wazazi. Watoto wanaposhindwa kufuata maelekezo hayo mara nyingi hupelekea adhabu kwa mtoto. Wazazi wa aina hii wana mataraio makubwa kwa watoto wao lakini hawako tayari kuwaelekeza watoto wao. Wazazi wa aina hii ni wenye utii na wanaotaka kuheshimika, na wanatarajia maagizo wanayotoa kwa watoto wao yatekelezwe bila kutoa maelezo ya kutosha.	Aina hii ya malezi ya ukali, mara nyingi huwafanya watoto kuwa watiifu na ….lakini inawafanya watoto wawe na kiwango cha chini cha furaha, kiwango cha chini cha utashi katika jamii na kiwango cha chini cha kujiamini.
Malezi ya kuongoza	Kama walivyo walezi wenye ktumia mamlaka, wanaotumia aina ya malezi ya kuongoza huweka taratibu na miongozo ambayo watoto wanapaswa kufuata. Ni wasikivu na wapo tayari kuulizwa maswali. Njia zao za kurekebisha tabia ni zenye kuelekeza, na sio za kuadhibu. Wanataka watoto wao kuwa na msimamo, wenye kuwajibika kijamii, kujisimamia wenyewe na kuwa na ushirikiano na wengine.	Matokeo katika aina hii ya malezi ya kuongoza ni kuwa na watoto wenye furaha, wenye uwezo na mafanikio.
Malezi yenye kuruhusu	Wazazi wenye kuruhusu, wakati mwingine wanajulikana kama wazazi wenye huruma, wana mahitaji machache kwa watoto wao. Wazazi wa aina hii mara chache sana kurekebisha tabia za watoto wao kwa sababu wana matarajio madogo sana kwa watoto wao kwa kuwaona hawajapevuka na hawawezi kujitegemea. Ni wazazi wenye msimamo zaidi kuliko kuhitaji wazazi wenye kuruhusu kwa ujumla ni walezi na wanawasiliana na watoto wao. Mara nyingi wanakuwa kama marafiki zaidi kuliko kuwa kama wazazi.	Wazazi wenye malezi ya kuruhusu hupelekea watoto wao kuwa na kiwango kidogo cha furaha na uwezo wa kujisimamia. Watoto hao wanauwezekano wa kuwa na matatizo ya kutii mamlaka na kutofanya vizuri shuleni.
Malezi yakutojihusisha	Aina hii ya malezi ya kutojihusisha yana sifa ya kuwa na matarajio kidogo, usikivu wa chini na mawasiliano hafifu. Wakati wazazi wanawapatia mahitaji ya msingi mara nyingi huwa hawajihusishi na maisha ya motto. Katika hali iliyokitiri wazazi wanaweza kuwatelekeza watoto au kutowajali katika kuwapatia mahitaji ya msingi.	Aina hii ya malezi ya kutojihusisha ndiyo aina ya mwisho kwa ubora. Watoto wanaolelewa malezi ya aina hii wanashindwa kujimudu, kujiamini, na hawana uwezo wa ushindani kama watoto wa rika lao.

Kitini cha 26: Kuandaa Mpango wa Huduma
Kisa Mafunzo, Sehemu ya 1

KISA MAFUNZO CHA SINIKIWE

KUANDAA MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 1

Kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji na uwezo iliyofanyika ya kisa mafunzo cha Sinikiwe jibu maswali yafuatayo:

Maswali:

1. Je, ni uwezo/rasilimali gani zilizopo katika familia ambazo zinaweza kumsidia baba katika kumuhudumia mtoto?
2. Ni rasilimali zipi ambazo Robert na Sinikiwe wanaweza kuwanazo/kuhamasisha upatikanaji wake? Na rasilimali zipi ambazo jamii inaweza kuzihamasisha upatikanaji wake?
3. Orodhesha namna utakavyompa Sinikiwe msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuhakikisha anabaki kwenye dawa/matibabu.
4. Je, unafikiri Sinikiwe anahitaji msaada wa kukabiliana na hali ya majonzi? Ni kwa jinsi gani utamsaidia?
5. Andaa mpango wa huduma:
    a. Amua kulingana na lengo (nini madhumu uni ya shughuli utakayofanya kwa niaba ya mtoto?).
    b. Fikiria shughuli utakazozifanya kufikia lengo.
    c. Weka vipaumbele vya mahitaji kipi kitakuwa cha 1, 2, na 3. Hivi ndivyo vipaumbele vyako.
    d. Amua tarehe za utekelezaji kwa kila shughuli uliyopanga.
    e. Uwe na uhakika nani atahusika na utekelezaji wa shughuli iliyopangwa.
    f. Tambua rasilimali zinazohitajika kutekeleza shughuli husika.
    g. Tambua mahali ambapo rasilimali hizo zitapatikana.
    h. Tambua namna ufuatiliaji wa mtoto utakavyofanyika na ni kwa mara ngapi.
6. Unafikiri hilo bado ni shauri lako? Ndio, unafikiri majukumu yako ni yapi?

Kama unafikiri huu ni mpango mzuri, uweke kwenye fomu ya tathmini ya mahitaji na mpango wa huduma na katika bango kitita. Jiandae kuuwasilisha katika kundi kubwa.

KISA MAFUNZO CHA KITO

KUANDAA MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 1

Kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji na uwezo uliyofanya ya kisa mafunzo cha Kito; jibu maswali yafuatayo:

Maswali:

1. Je, ni uwezo/rasilimali gani zilizopo ndani ya familia ambazo zinaweza kumlea na kumuendeleza mtoto wake?
2. Ni rasilimali zipi ambazo mama yake Kito anaweza kutoa/kuhamasisha upatikanaji wake?
3. Ni hatua gani zichukuliwe kumsaidia Kito?
4. Kati ya mapendekezo yaliyo orodheshwa ni yapi ya haraka?
5. Andaa mpango wa huduma wakumsaidia Kito:
    a. Fanya maamuzi kulingana na lengo (nini madhumuni ya shughuli utakayofanya kwa niaba ya mtoto?).

b. Fikiria shughuli utakazo fanya kufikia lengo.
c. Weka vipaumbele vya mahitaji 1, 2, na 3. Hivi ndivyo vipaumbele vyako.
d. Amua tarehe za utekelezaji kwa kila shughuli uliyopanga.
e. Uwe na uhakika nani atahusika na utekelezaji wa shughuli iliyopangwa.
f. Tambua rasilimali zinazohitajika kutekeleza shughuli iliyopangwa.
g. Tambua mahali ambapo rasilimali hizo zitapatikana.
h. Tambua namna ufuatiliaji wa mtoto utakavyofanyika na ni mara ngapi.

6. Unafikiri hili bado ni shauri lako? Kama ndio, unafikiri majukumu yako ni yapi?

Mara utakapogundua kuwa mpango wako ni mzuri jaza katika fomu ya tathmini ya mahitaji ya mtoto na mpango wa huduma na kuuandika katika bango kitita. Jiandae kuwasilisha katika kundi kubwa.

KISA MAFUNZO CHA SHOLE

KUANDAA MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 1

Maswali:

1. Je, ni uwezo/rasilimali gani zilizopo katika familia ambazo zinaweza kumsaidia Shole na shangazi yake katika kukabiliana na hali hiyo?
2. Ni rasilimali zipi ambazo Shole na shangazi yake wanaweza kuzikusanya? Na ni rasilimali zipi ambazo jamii inaweza kuzihamasisha upatikanaji wake?
3. Onyesha jinsi utakavyo mpatia Shole msaada wa kisaikolojia na wa kijamii.
4. Ni mambo gani yanayohitajika katika kumsaidia Shole?
5. Kati ya mapendekezo yaliyotolewa yapi ni ya haraka na kwa nini?
6. Andaa mpango wa huduma wa muda maalum wa Shole:
   a. Amua kulingana na lengo (nini madhumuni ya shughuli utakayofanya kwa niaba ya mtoto?).
   b. Fikiria shughuli utakazozifanya kufikia lengo.
   c. Weka vipaumbele vya mahitaji 1, 2, na 3.
   d. Weka tarehe za utekelezaji kwa kila shughuli uliyopanga.
   e. Nani atahusika na utekelezaji wa shughuli iliyopangwa.
   f. Rasilimali zipi zinazohitajika kutekeleza shughul iliyopangwa.
   g. Wapi ambapo rasilimali hizo zitapatikana.
   h. Jinsi ufuatiliaji wa mtoto utakavyofanyika na ni mara ngapi.
7. Je, unafikiri hili bado ni shauri lako? Kama ndio, unafikiri majukumu yako ni yapi?

Mara utakapogundua kuwa mpango wako ni mzuri jaza katika fomu ya tathmini ya mahitaji ya mtoto na mpango wa huduma na kuuandika katika bango kitita. Jiandae kuwasilisha katika kundi kubwa.

Kitini 27: Fomu ya Tathmini ya Mahitaji ya Mtoto na Mpango wa Huduma

Kitini cha 28: Kuandaa Mpango wa Huduma kisa Mafunzo, Sehemu ya 2

KISA MAFUNZO CHA KITO

KUANDAA MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 2

Kwa kuzingatia tathmini ya awali ya mahitaji na uwezo, unaamua kumpa rufaa Kito kwenda kliniki ya karibu kwa uchunguzi wa afya yake. Aidha, wasiliana na taasisi inayojihusisha na kuwajengea uwezo watu katika masuala ya uchumi ngazi ya kaya katika kijiji chenu ili mama yake Kito apate msaada.

Ongozana na Kito kwenda kliniki na daktari anagundua Kito ana utapia mlo mkali ambao umesababisha kudumaa, na matatizo zaidi ya kimwili. Vile vile daktari anagundua kwamba matatizo ya Kito yamesababishwa na kutokufuata maelekezo ya kuhudhuria kliniki kila mwezi kwa miaka sita iliyopita.

Daktari anampatia lishe mbadala na kumtibu vidonda. Mama yake Kito anapewa msaada ya kujiunga na kikundi cha kusaidiana ili kuongeza mtaji wake, anefungua kioski chake cha kuuza mboga mboga na matunda, nje ya nyumba yake ili awe karibu na mwanae kila siku. Vile vile mama Kito anafuga kuku ambapo wanampatia mayai kwa ajili ya mwanae na mengine kwa ajili ya kuuza ili kupata pesa za ziada.

Panga kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa familia hii ili kuona kama kuna kuimarika kwa afya ya Kito.

KISA MAFUNZO CHA SINIKIWE

MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 2

Kwa kuzingatia tathmini iliyofanyika awali ya mahitaji na uwezo, mpe rufaa Sinikiwe kwenda kliniki ya karibu ili akafanyiwe uchunguzi na kupimwa afya yake na VVU. Pia, peleka ripoti kituo cha polisi kuhusu tuhuma za ukatili wa kingono na kumpa taarifa Afisa Ustawi wa Jamii. Matokeo ya vipimo vya VVU yameonesha Sinikiwe ana VVU na ananzishiwa tiba ya kufubaza VVU.

Baba yake Sinikiwe naye anapima VVU na ameonekana hana maambukizi VVU. Uchunguzi wa ki daktari unaonekana Sinikiwe hajawahi kuingiliwa kingono wala kufanya vitendo vya ngono kabla. Afisa Ustawi wa Jamii amsaili Sinikiwe ambaye anasisitiza kwamba hajawahi kufanyiwa ukatili wa kingono na baba yake. Robert, ambaye amekamatwa na polisi kwa ajili ya kumhoji, ameachiwa baada ya kubaini kuwa hakuna ushaidi wa kutosha kumtia hatiani.

KISA MAFUNZO CHA SHOLE

MPANGO WA HUDUMA, SEHEMU YA 2

Baada ya tathmini ya mahitaji na uwezo, amua kumpa rufaa Shole kwenda kliniki ya jirani kwa uchunguzi wa kiafya, hususani kuangalia kama zile tuhuma za ukatili wa ngono ni za kweli.

Vile vile wasiliana na Afisa Ustawi wa Jamii kuhusu suala hilo.

Ongozana na Shole kwenda hospitali na daktari anamfanyia uchunguzi na kuthibitisha kuwa kweli amefanyiwa ukatili wa kingono; na amepata maambukizo ya magonjwa ya zinaa. Kwa kushirikiana na msimamizi wa kata (Afisa Ustawi wa Jamii) ambaye amepewa jukumu na Afisa Ustawi wa Wilaya, peleka shauri kituo cha polisi na mjomba/baba mdogo wa Shole akamatwe.

Amua kumfuata shangazi/mama mdogo wa Shole kazini kwake na kumpa taarifa zote za kilicho tokea. Anapata mshtuko na kumkasirikia sana Shole, kwa kutokumwambia nini alikuwa anafanyiwa.

Shole anasajiliwa kwenye matibabu ya magonjwa ya zinaa na ameanza kufanyiwa unasihi. Ongea na mwalimu wa Shole na amuombe kumhamishia katika shule nyingine. Kwenye mahojiano na shangazi/mama mdogo umegundua kuwa bibi yake Shole anaishi kijiji jirani, hivyo mnakubaliana mtoto ahamie kwa bibi yake.

Hatimaye, Shole anaishi na bibi yake na anaendelea vizuri na masomo. Aidha amejiunga na klabu ya kuwajengea stadi za maisha wasichana kijijini kwa bibi yake. Kupitia kwa msimamizi wako wa kata unaletewa taarifa na Afisa Ustawi wa Wilaya kuwa mjomba/baba mdogo amekutwa na hatia ya kubaka.

Kitini cha 29: Kuandaa Mpango wa Huduma na Familia

Chunguza tatizo
- Rejea kwenye tathmini inasemaje kuhusu tatizo.
- Saidia mtoto na wazazi/walezi kutambua tatizo na kulikubali.
- Baini msaada ambao familia inaweza kutoa. Kubaliana kuhusu tatizo na lengo.

Makubaliano
- Kubaliana lengo la jumla la kushughulikia tatizo
- Kubaliana hatua zipi zichukuliwe kuhakikisha lengo linatimia
- Kubaliana muda uliopangwa kwa ajili ya mabadiliko kwa kila tatizo.
- Matatizo gani ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka na mengine yanayohitaji kushughulikiwa katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu?

Hatua
- Chukua tatizo moja baada ya jingine na, gawanya katika hatua ambazo mtoto, familia, Msimamizi wa shauri la mtoto au wengine wamekubaliana kuzitekeleza.
- Inaweza kuwa na manufaa kukabiliana na tatizo unaloweza kulitatua kwanza, kwani huleta mafanikio na kujiamini katika mbinu. Hata hivyo, matatizo ambayo yanahitaji utatuzi wa haraka yanapaswa kushughulikiwa kwa haraka, hasa pale ambapo hubeba madhara makubwa kwa mtoto.
- Tambua rasilimali zote zinazohitajika – na uwe na uhakika wa mahali zinapoweza kupatikana.

- Jadili njia mbadala kama baadhi ya hatua hazitawezekana. Uliza, "nini kitakachotokea kama hatua hii haita chukuliwa?"

Andaa mpango kwa ajili ya ufuatiliaji na mapitio:

- Amua nini kitakuonesha kwamba mpango wa huduma unatekelezeka.
- Amua nini kitakuonesha kwamba mpango wa huduma hautekelezeki.
- Panga tarehe ya kikao cha mapitio ya mpango wa huduma kitakachofanyika baada ya kufanya ufuatiliaji kwa muda kadhaa. Usisubiri hadi mwisho wa muda uliopangwa – kwani itapelekea kuchelewa kufanya marekebisho!

Kawaida ni vizuri kufanya ufuatiliaji kila baada ya miezi mitatu, (kama mpango ni wa muda mrefu zaidi ya miezi mitatu), fanya mabadiliko yanapo hitajika kila baada ya ufuatiliaji. Hata hivyo, kesi za dharura zinatakiwa kufuatiliwa mara kwa mara kwenye mpango wa huduma.

Kitini cha 30: Kisa Mafunzo cha Adila

Adila ambaye ana umri wa miaka 8 anaishi na shangazi yake na mjomba wake. Baba yake mzazi alifariki mwaka mmoja uliopita, na mama yake mwaka mmoja kabla ya baba yake kufariki kwa ugonjwa wa Ukimwi. Kabla ya kuanza kuishi na shangazi yake aliishi kwa bibi yake. Akiwa anaishi na bibi yake walikuwemo watu wengine kama kaka yake Adila mwenye umri wa miaka 9. Vile vile shangazi yake alikuwa na watoto wanne na binamu yake ambaye ambaye mama yake alifariki miaka 2 iliyopita. Mwalimu aligundua kuwa Adila alianza kujiingiza katika matatizo akiwa shuleni. Alikuwa akipigana na watoto wenzake akiwapiga mateke na kuwarushia ngumi. Baadhi ya watoto walianza kulalamika kwamba Adila alikuwa anachukua chakula chao kwa nguvu. Hivyo mwalimu aliamua kumchukua Adila na kukaa naye kitako ili azungumze naye habari zake binafsi na za familia yake. Aidha Mwalimu kugundua kuwa Adila alikuwa akiishi na watoto wenzake wengi sana nyumbani na wakati mwingine alikosa chakula cha kuwatosheleza wote kuna wakati shangazi yake alikuwa mkali sana na kuanza kuwagombeza. Adila alimwambia mwalimu kuwa hata mama yake hakuwahi kumkaripia hivyo. Aidha watoto wenzake shuleni walimkasirisha sana kwa sababu walimuita majina ya kila namna na kumtania kwa sababu wazazi wake walishafariki na hakuwa na sare nzuri za shule wala kalamu ya kuandikia. Hatimaye mwalimu aliwasiliana na muhudumu wa kujitolea ili amsaidie mtoto.

Kitini cha 31: Visa Mafunzo Muhimu – Sinikiwe & Shole

KISA MAFUNZO CHA MSINGI CHA SINIKIWE: Ongeza taarifa hizi zifuatazo kwa kile ambacho tayari unakifahamu juu ya Sinikiwe. Ni binti mwenye umri wa miaka 9, alipatwa na msiba wa mama yake miaka 2 iliyopita. Sinikiwe alikuwa akimtizama mama yake ambaye alikuwa anaugua mara kwa mara huku akizidiwa kwa kadiri ya mwaka mmoja hivi. (Umri wa miaka 6-7) japokuwa alikuwa mdogo lakini alisaidia katika huduma kwa mama yake.

- Alikuwa karibu kweli na mama yake ambaye alikuwa mpole na mwenye mapenzi mema na alipenda kumsaidia.
- Si mama yake wala baba yake aliye wahi kumweleza Sinikiwe juu ya ugonjwa wa mama yake na hakutegemea kama angefariki.
- Kabla mama yake hajaanza kuumwa, mama yake alikuwa ni mchuuzi na kipato chake kilisaidia sana katika familia. Waliishi katika eneo kubwa. Baadaya mama yake kufariki ndipo yeye na baba yeke waalipohamia katika chumba wanachoishi sasa.

KISA MAFUNZO CHA MSINGI CHA SHOLE

Ongeza taarifa zifuatazo kwa kile unachokifahamu hadi sasa juu ya kisa cha Shole. Shole ana umri wa miaka 13. Mama yake alifarikia akiwa na umri wa miaka 10, ambapo alipelekwa kuishi na shangazi yake. Shole ana wadogo zake wadamu wawili, mdogo wake wa kike mwenye umri wa miaka 2 pungufu ya umri wake na mdogo wake wa kiume mwenye umri wa miaka 5. Amekuwa karibu sana na ndugu zake hawa wa damu ambao kwa pamoja wanamtegemea yeye. Mama yake alipofariki, wadogo zake wawili walichukuliwa na ndugu ili wakalelewe huko kijijini na palikuwa mbali sana. Kiuhalisia ni kama hana mawasiliano na ndugu zake tokea kipindi hicho. Baba mzazi wa Shole alifariki akiwa na umri wa miaka 4 kabla ya mama yake, Shole alipokuwa na umri wa miaka 6. Shole anamkumbuka baba yake jinsi alivyokuwa ana mbeba kwenye mabega na wakati mwingine akiwa anacheza naye. Pia anakumbuka jinsi alivyokuwa anamwogopa kwani alishamwona baba yake akiwa anarudi nyumbani akiwa amelewa, akipiga kelele na kumgombeza mama yake mara nyingi.

Shangazi yake Shole amekuwa akiishi na na mama yake. Wanawake hawa wawili wamekuwa wa tofauti sana kwa uzoefu wa Shole. Mama yake Shole alikuwa ni mtu wa kumlinda sana Shole na alikuwa akimtizama sana kwa lengo la kumlinda, tofauti na shangazi yake ambaye hamjali.

Kitini cha 32: Mwongozo wa Rufaa kwa MMWJ

Kwa mwongozo, MMWJ anapaswa kutoa rufaa kama:

- Shauri linahusu ulinzi wa mtoto na linahitaji msaada wa kisheria mfano, ukatili wa kingono.
- Hawana uhakika na uwezo wa kulishughulikia shauri hilo.
- Mtoto anahitaji taarifa maalum na za kitaalamu.
- Kuna wasi wasi juu ya hali ya mtoto kimwili, kijamii, kihisia na hali ya afya ya mtoto.
- Kuna mabadiliko ya mtoto kimwili, kihisia, kijamii na kunahitajika ufuatiliaji wa kitaalamu kupata taarifa za kina, huduma tofauti au zaidi. Hii ni maalumu kwa watoto walio katika matumizi ya dawa za kufubaza VVU.
- Mtoto anapohama kwenda sehemu nyingine anatakiwa aunganishwe na MMWJ au taasisi nyingine iliyoko katika eneo alilohamia.
- Wana wasiwasi na suala la kimaadili katika kumhudumia mtoto na wanaamini mtu mwingine anaweza kutoa huduma sahihi.

Rufaa ya Huduma ya Unasihi na Kupima VVU

Baadhi ya watoto wanaweza kuwa na VVU lakini hawajapimwa. Ni muhimu rufaa ya unasihi na kupima VVU kufanyika kwa WWKMH ambao wanaweza kuwa katika hatari ya kuambukizwa VVU, hususani WWKMH ambao:

- Waliwahi kulazwa hospitali
- Wanaugua magonjwa ya ngozi mara kwa mara
- Wana wazazi ambao wote au mmojawapo amefariki kwa VVU
- Wamekuwa na afya mbaya/dhaifu katika kipindi cha miezi mitatu
- Wana ugonjwa wa kudumu, mzazi au yeyote ndani ya kaya anakokaa mtotoamepima na kukutwa na maambukizo ya VVU
- Wana utapiamlo
- Wamepimwa na kugundulika kuwa na kifua kikuu
- Wanaishi kwenye kaya ya watoto wanaojilea wenyewe au wanaishi mitaani
- Wamefanyiwa ukatili wa kingono
- Wana tatizo lingine linalohusiana na VVU

Kitini cha 33: Fomu ya Maelekezo ya Huduma Zinakopatikana

Jina la Mtaa/Kijiji:					
Jina la taasisi/Mtu	**Anuani ya eneo/makazi**	**Shughuli ya taasisi/Mtu**	**Mtu wa kuwasiliana naye**	**Taarifa za mawasiliano**	**Muda wa kazi/siku/saa**

Kitini cha 34: Mfano wa Mazingira ya Kutoa Rufaa

Kisa mafunzo namba 1:
Caroline ni msichana mwenye umri wa miaka 7 ambaye anaishi na ndugu zake katika moja ya kijiji nchini Tanzania. Wazazi wake wote walifariki mwaka mmoja uliopita baada ya kuugua kwa muda mrefu. Msimamizi wa shauri la mtoto amepewa taarifa na wanajamii kwamba inawezekana Caroline anajisikia vibaya nyumbani kwao na pia hajawahi kuonekana anacheza na watoto wenzake kwa muda mrefu sasa. Wakati msimamizi wa shauri la mtoto alipoenda kumtembelea Caroline nyumbani, akakuta kwamba Caroline ni mgonjwa sana. Wakati msimamizi wa shauri la mtoto akijadiliana na ndugu zake Caroline, alitambua wazi kwamba familia bado haijampeleka kliniki.

- Ni nini utafanya vizuri? Je, utaboresha nini?
- Ni nini majukumu ya msimamizi wa shauri la mtoto katika kila shauri?
- Ni nini kitatokea kama msimamizi wa shauri la mtoto hana uwezo wa kusimamia shauri? Ni nini atafanya?

Kisa mafunzo namba 2:
Sam ana umri wa miaka 8. Amekuwa na matatizo ya maambukizi ya kawaida ya ngozi, kuhara na anakohoa sana. Yeye pia ni mdogo kwa umri wake. Sam anaishi na mama yake mdogo kufuatia kifo cha wazazi wake alipokuwa mtoto mdogo. Sam hajawahi kupima VVU.

- Ni nini ulichofanya vizuri? Je, nini unaweza kuboresha?
- Ni nini majukumu ya msimamizi wa shauri la mtoto katika kila shauri?
- Ni nini kitatokea kama msimamizi wa shauri la mtoto hana uwezo wa kusimamia shauri hilo? Ni nini atafanya?

Kisa mafunzo namba 3:
Sheilla ana umri wa miaka 17. Yeye alizaliwa na virusi vya UKIMWI na amekuwa akitumia ARVs tangu alipozaliwa. Mama yake amekuwa akimwambia kuwa ARVs ni nyongeza ya 'vitamini', na hivyo hadi sasa, Sheilla hatambui kwamba yeye ana VVU. Sheilla sasa ameanza kuwa na mahusiano ya kingono na idadi ya wavulana tofauti tofauti wa jirani na maeneo anakoishi, na wakati mama yake akimshauri juu ya madhara ya mahusiano hayo, yeye daima anajibu kwa ukali na ukaidi.

Maswali kwa visa mafunzo vyote (Caroline, Sam na Sheilla):

- Ni nini ulifanya vizuri? Je, nini waweza kuboresha?
- Ni nini majukumu ya msimamizi wa shauri la mtoto katika kila shauri?
- Nini nini kitatokea kama msimamizi wa shauri la mtoto hana uwezo wa kusimamia shauri hilo? Ni nini atafanya?

Kitini cha 35a: Fomu ya Rufaa

Kitini cha 35b: Maelekezo ya Kujaza Fomu ya Rufaa

Kitini cha 36a: Fomu ya Mwezi ya Ufuatiliaji wa Huduma

Kitini cha 36b: Maelekezo ya Kujaza Fomu ya Mwezi ya Ufuatiliaji wa Huduma

Kitini cha 37a: Fomu ya Muhtasari wa Taarifa za Mwezi za Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

Kitini cha 37b: Maelekezo ya Kujaza Fomu ya Muhtasari wa Taarifa za Mwezi za Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

Kitini cha 38: Visa Mafunzo Muhimu – Kuhitimisha Shauri la Huduma

KISA MAFUNZO CHA SINIKIWE

KUHITIMISHA SHAURI LA HUDUMA

Sinikiwe alihitaji kuanzishiwa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI, alihitaji msaada wa elimu, alihitaji cheti cha kuzaliwa kwa ajili ya msaada wa ulinzi wa kisheria, alihitaji msaada wa lishe. Nimemuunganisha na kliniki, ofisi ya usajili wa vizazi na vifo (RITA) na kumuunganisha na wafanyabiashara wadogo wadogo kwa ajili ya kupata msaada wa ada ya shule.

Kwa Ufuatiliaji:

- Nimemuunganisha na watoa huduma wa afya kujadili na kupanga kwa ajili ya kumpa dawa na ufuasi wa dawa kwa mtoto. Nimejadili na wadau wa maendeleo yanayohusiana na shauri hili na tumekubaliana kumpa msaada.
- Nimewasiliana na walimu juu ya maahudhurio na mabadiliko ya tabia walioyaona wakati mtoto anapokuwa shule, kupitia ziara za mara kwa mara.
- Nimejadiliana na viongozi wa kijiji na kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto juu ya utaratibu wa malazi.
- Kwa baba yake (Robert), Nimeangalia kama kuna vikundi vya malezi ambavyo vipo katika jamii ambavyo vinaweza kumsaidia. Nimeangalia ni namna gani vikundi vimeundwa na wanachangia kiasi gani ambacho kitafaa zaidi kabla ya kumtambulisha. Ninafahamu kwamba inahamasisha zaidi kujiunga katika kikundi walezi wenye hali sawa (wagane wanaolea watoto wa kike). Nilihakikisha kwamba Robert anaelewa kikundi gani anategemea kuwa mwanachama kabla ya kumtambulisha kwenye kikundi.

- Kwa kuhitimisha shauri la huduma la Sinikiwe, nitalifunga wakati Sinikiwe amepata huduma zote anazozihitaji (mfano: amepata dawa na ni mfuasi mzuri,ameboreka kiafya kutokana na msaada wa lishe, ada yake ya shule imelipwa na anahudhuria shule mara kwa mara, malazi yake yameandaliwa, baba yake ameunganishwa na vikundi vya malezi pamoja na vikundi vya kiuchumi).

Hatua gani za kuchukua kufunga shauri?

- Kupitia mazingira hatarishi: Zungumza na Sinikiwe na Baba yake kuhusu mafanikio maalumu, kusisitiza mabadiliko chanya ya tabia na masharti/vikwazo.
- Pitia shughuli kama zimekamilika: Jadili kama kuna vikwazo vyovyote ulivyokutana navyo na angalia mafanikio na maarifa uliyoyapata.
- Pitia hatua za jumla katika kutatua tatizo: Ikumbushe familia mwendelezo uliofanya na njia ambazo wanaweza kuzitumia wakati wa kutatua matatizo baadaye yatakapo jitokeza.
- Ainisha kama kuna mahitaji au changamoto: Wasaidie wanafamilia kupanga namna ya kudumisha mabadiliko waliyoyafikia. Jadili kama kuna kikwazo ambacho kinachoweza kujitokeza na nmna ya kukabiliana nacho.

KISA MAFUNZO CHA KITO

KUHITIMISHA SHAURI LA HUDUMA

Mama yake Kito ameunganishwa na huduma za kujiingizia kipato pamoja na vikundi vya kijamii vya kuweka na kukopa. Sasa ana genge la kuuza matunda jirani na nyumbani kwake kwa hiyo yupo karibu na mtoto wake. Msimamizi wa mashauri ya jamii aliendelea kumtembelea nyumbani kwake na kumpeleka mtoto kituo cha afya kila mwezi. Pale ustawi wa mtoto ulipoimarika, mtoto ametibiwa, vidonda vimepona na hali yake ya lishe imeimarika. Mama yake hamuachi tena mtoto peke yake, pia ana uwezo wa kumtunza wakati huo huo akifanya kazi ya genge. Aidha, mtoto ameandikishwa shule kwenye mpango wa mwaka mmoja.

KISA MAFUNZO CHA SHOLE

KUHITIMISHA SHAURI LA HUDUMA

Mjomba wa Shole ameshitakiwa kwa kosa la ubakaji, Shole amehamishiwa kwa bibi yake na ameimarika kwa sababu amepata msaada wa kisaikolojia kutoka kwa msimamizi wajamii aliyeshughulikia shauri la huduma yake. Msimamizi wa Shole amewasiliana na msimamizi wa jamii katika kijiji alichohamia Shole, ili kuhakikisha kuwa bibi yake Shole amenufaika na shughuli za kujipatia kipato na vikundi vya kijamii vya kuweka na kukopa.

Ninaweza kuwasiliana na msimamizi mwenzangu ili awasiliane na wasimamizi wa jamii wengine. (Inapotokea sifahamiani na msimamizi wa jamii wa kijiji alichohamia Shole).

Nimekuwa nikifanya kazi kwa ukaribu na kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya ya kijiji na pamoja viongozi wa kijiji namna ya kutetea na kuzuia ukatili wa watoto kwa kutoa elimu.

Nimekuwa nikifikiria shule ni sehemu muhimu ya kutoa elimu kwa wanafunzi na walimu kuhusu huduma ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi.

Nimelihamisha shauri la huduma la Shole huko alikohamia kijiji kingine, ingawa nitaendelea kumfuatilia kupitia Msimamizi wa mashauri ngazi ya jamii wa kijiji alichohamia Shole.

Kitini cha 39: Fomu ya Kuhitimisha Shauri la Huduma

Kitini 40: Kushughulikia Msongo

AINA ZA MISONGO:

- **MSONGO WA MSINGI:** Hutokea kwa mtu binafsi, kwa familia na katika mahusiano. Msongo wa msingi waweza kuongezeka kutokana na mabadiliko ya mazingira kwa kawaida hali hii hupungua baada ya wiki chache mara mtoa huduma wa jamii anapoanza kutekeleza majukumu yake.

- **MSONGO WA MUDA MREFU**: Unatokana na msongo wa msingi unaodumu kwa muda mrefu. Hali hii inaweza kuleta mtazamo hasi, hasira, huzuni, kujiskia hufai nk. Vyanzo vya msongo unaoongezeka ni kazi nyingi na ngumu, mawasiliano hafifu, kukaa mahali unapojiskia huna mamlaka /sauti, maisha ya kazi yenye misuguano, kushindwa kuongea/kutotoa maoni/kupata ububu, kusoma mambo mengi kwa muda mfupi, upweke, kukosa usingizi na hali ya ugonjwa.

- **MSONGO WA DHARURA:** Msongo wa namna hii hii hujiziilisha wazi pale ambapo mtu anaona maisha yake yapo hatarini. Pia pale ambapo mtu anashuhudia, anakumbana na mambo makubwa yanayoumiza moyo, wakati mwingine hali inaweza kusabisha "post-traumatic stress disorder." Maumivu yanaendelea baada ya tukio ambalo litahitaji rufaa kwenda kumuona mtaalam.

- **MSONGO WA HURUMA:** Msongo wa aina hii hutokea katika menejimenti ya kesi kwani menejimenti ya kesi inahusisha ufanyaji kazi moja kwa moja na watu wanaoteska na mateso yao kutia huruma. Hii hutokea haswa na watu waliokumbwa na madhara ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Isitoshe mara kwa mara mtaskia taarifa za kufiwa, za kuhuzunisha, na za watu wenye majonzi wakati wote.

NJIA ZA KUSHUGHULIKIA MSONGO UNAOHUSIANA NA KAZI ZA MHUDUMU WA MASHAURI YA WATOTO:

- Jitambue kwa kufahamu nini kinatarajiwa toka kwako. Ni sawa kusema "hapana" kama unafahamu kwamba hutaweza kumudu kile unaombwa kufanya. Tafuta njia zingine za kusaidia.
- Kuwa muwazi kwa jamii, nini watarajie toka kwako.
- Tafiti nani anaweza kuwa msaada kwako katika jamii kwa masuala ya watoto na familia.
- Mudu shughuli zako. Tathmini kwa makini kama shauri linahitaji kufunguliwa. Hitimisha mashauri yote ambayo yamefikia muda wa kufanya hivyo.
- Kuwa na mahusiano mazuri na msimamizi wako. Yule mtu anaweza kuwa msaada mkubwa.
- Jenga mahusiano mazuri na MMWJ wenzako na wasaidizi ustawi jamii. Katika baadhi ya jamii wameunda makundi madogo ya kusaidiana jinsi kukutana na kubadilishana mawazo kuhusu mashauri na msongo.
- Furahi – usisahau watu wengine ambao ni msaada kwako, mathalani familia, marafiki, kuabudu, kuimba, kazi za bustani, na shughuli zingine ambazo ambazo zinaweza kuwa msaada kwako katika kumudu msongo.

RATIBA YA MAFUNZO

Siku ya 1: Kinachofanyika kwa sasa na misingi ya uratibu wa Mashauri ya Watoto	Siku ya 2: Tathmini	Siku ya 3: Kutengeneza na kutekeleza mpango wa huduma	Siku ya 4: Rufaa na ufuatiliaji	Siku ya 5: Kutengeneza mpango wa utekelezaji na kufunga warsha
03:00 - 04:00 Ukaribisho, Utambulisho, Malengo	02:30 (Dakika 15) Mrejesho wa siku iliyopita; Mapitio ya siku inayofuata	02:30 (Dakika 15) Tafakari: Nawezaje kutumia mbinu ya Usimamizi wa Mashauri ya Watoto katika shughuli zangu?	02:30 (Dakika 15) Mrejesho wa siku iliyopita; Mapitio ya siku inayofuata	02:30 (Dakika 15) Mrejesho wa siku iliyopita; Mapitio ya siku inayofuata
04:00 - 06:00 **MODULI YA 1: Misingi ya uratibu wa Mashauri ya Watoto**	04:00 – 04:30 **MODULI YA 3: Utambuzi/Usajili/ Usaili**	03:00 - 04:30 **MODULI YA 5: Kuandaa mpango wa huduma**	02:45 - 04:30 **MODULI YA 7: Rufaa na ufuatiliaji**	02:45 - 04:30 **MODULI YA9: Kukabili changamoto**
Mapumziko ya Chai (Dakika 30)	**Mapumziko ya Chai** (Dakika 30)	**Mapumziko ya Chai** (Dakika 30)	**Mapumziko ya Chai** (Dakika 30)	**Mapumziko ya Chai** (Dakika 30)
05:00 - 07:00 **MODULI YA 2: Sehemu ya 1 (Endelea baada ya chakula cha mchana)**	05:00 - 07:00 **MODULI YA 4: Tathmini**	05:00 – 06:00 **MODULI YA 5: Kuandaa mpango wa huduma** (Inaendelea) 06:00 – 07:00 **MODULI YA 6: Kutoa huduma za moja kwa moja na msaada**	05:00 - 07:00 **MODULI 7: Rufaa na ufuatiliaji** (Inaendelea)	04:30 – 06:00 **MODULI YA 10: Kuwahudumia watoa huduma /walezi (kujihudumia)** 06:00 – 06:30 **Kutengeneza mpango wa utekelezaji** Kufunga/Tathmini Mafunzo
Chakula cha Mchana 07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana** 07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana** 07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana** 07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana /Kuondoka**
08:00 – 09:30 **MODULI YA 2: Jukumu na wajibu wa Wahaudumu wa Mashauri ya Watoto Ngazi ya Jamii Katika Usimamizi wa Mashauri ya Watoto** 09:30 – 11:00 **MODULI YA 3: Utambuzi/Usajili/ Usaili**	08:00 – 11:00 **MODULI YA 4: Tathmini** (Inaendelea)	08:00 - 11:00 **MODULI YA 6: Kutekeleza mpango wa huduma -utoaji wa msaada na huduma**	08:00 – 10:00 **KUHITIMISHA SHAURI LA HUDUMA**	
Kufunga/Tathmini ya siku	Kufunga/Tathmini ya siku	Kufunga/Tathmini ya siku	Kufunga/Tathmini ya siku	

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

PEPFAR

bantwana
WORLD EDUCATION


JSI